

# Uinukaji kwa Kuhudumu



Taasisi ya Ruhi





Kitabu cha 2

# Uinukaji kwa Kuhudumu

Taasisi ya Ruhi

Vitabu katika Mlolongo huu:

Hapo chini yapo majina ya vitabu vilivyopo kwa sasa katika mlolongo ulioandaliwa na Taasisi ya Ruhi. Vitabu hivi vinakusudiwa kutumika kama mlolongo mkuu wa kozi katika juhudi ya hatua kwa hatua ya kuongeza uwezo wa vijana na watu wazima kuhudumia jumuiya zao. Taasisi ya Ruhi pia ina kuza seti ya kozi zinazochepuka kutoka kitabu cha tatu katika mlolongo kwa ajili ya kuwafunza walimu wa madarasa ya watoto ya Kibahá'í, hali kadhalika seti nyingine kutoka kitabu cha tano kwa ajili ya kuinua wahuishaji wa vikundi vya vijana chipukizi. Hizi, pia, zimeoneshwa katika orodha hapo chini. Inapashwa kukumbukwa kwamba orodha hii inaweza kubadilika kadiri uzoefu ugani uendeleavyo, na majina ya ziada yataongezwa kadiri idadi ya vipengele vya kimtaala vinavyoendelea kukuzwa vifikiapo hatua ambapo vinaweza kusambazwa kwa upana.

| | |
|---|---|
| Kitabu cha 1 | *Mawazo Juu ya Maisha ya Roho* |
| Kitabu cha 2 | *Uinukaji kwa Kuhudumu* |
| Kitabu cha 3 | *Kufundisha Madarasa ya Watoto, Daraja la 1* |
| | *Kufundisha Madarasa ya Watoto, Daraja la 2* (kozi ya mchepuo) |
| | *Kufundisha Madarasa ya Watoto, Daraja la 3* (kozi ya mchepuo) |
| | *Kufundisha Madarasa ya Watoto, Daraja la 4* (kozi ya mchepuo) |
| Kitabu cha 4 | *Wadhihirishaji Pacha* |
| Kitabu cha 5 | *Uachiliaji wa Uwezo wa Vijana Chipukizi* |
| | *Msukumo wa Awali: Mchepuo wa kwanza wa kozi ya Kitabu cha 5* |
| | *Duara Lipanukalo: Mchepuo wa pili wa kozi ya Kitabu cha 5* |
| Kitabu cha 6 | *Ufundishaji Hoja* |
| Kitabu cha 7 | *Kutembea Pamoja katika Njia ya Huduma* |
| Kitabu cha 8 | *Ahadi ya Bahá'u'lláh* |
| Kitabu cha 9 | *Kupata Mtazamo wa Kihistoria* |
| Kitabu cha 10 | *Kujenga Jumuiya Hai na Zenye Kupuma* |
| Kitabu cha 11 | *Nyenzo za Kimwili* |
| Kitabu cha 12 | *Familia na Jumuiya* |
| Kitabu cha 13 | *Kujihusisha katika Shughuli za Kijamii* |
| Kitabu cha 14 | *Kushiriki katika Mijadala ya Umma* |

Haki miliki © 1997, 2021 na Taasisi ya Ruhi, Colombia
Haki zote zimehifadhiwa. Toleo 2.1.2.PE Zilizochapishwa Aprili 2021
ISBN 978-958-53332-0-8

Kilichapishwa awali kwa Kihispania kama *Levantémonos a servir*
Haki miliki © 1987, 1996, 2020 na Ruhi Msingi, Colombia
ISBN 978-958-52941-0-3

Taasisi ya Ruhi
Cali, Colombia
Barua pepe: instituto@ruhi.org
Tovuti: www.ruhi.org

# Yaliyomo

Mawazo Machache kwa ajili ya Mkufunzi .............v

Furaha ya Ufundishaji .............................................1

Mazungumzo Yainuayo ........................................17

Dhima za Kujiongezea Elimu Zaidi .......................37

# Mawazo machache kwa ajili ya Mkufunzi

Kitabu hiki, cha pili katika mlolongo mkuu wa kozi zinazotolewa na Taasisi ya Ruhi, kinahusiana na uwezo ambao hutuwezesha kuchangia kwenye mazungumzo ya maana na yainuayo. Kitendo maalum cha huduma ambacho kitabu kimekazia kimeelezwa katika kitengo cha tatu. Katika ulimwengu ambamo nguvu zenye uwezo zinapasulia mbali mafundo ya kijumuiya, tabia ya kuwatembelea marafiki na majirani katika nyumba zao kwa ajili ya kuchunguza dhima kuu za maisha ya kijamii, kama itakuwa desturi muhimu ya utamaduni, inaweza kuwa tiba kwa baadhi ya magonjwa yanayoletwa na utengano unaoendelea kuongezeka. Mafundo ya udugu yanayojengwa kwa njia hii, kitengo hiki kinapendekeza, yanaweza kutumika kuimarisha mchakato wa ujengaji jumuiya hai na zenye upatano.

Programu iliyodumishwa ya ziara kwenye nyumba katika ujirani au kijiji huhitaji kiwango fulani cha mpangilio, unaohusisha kiini cha marafiki ambao wamejifunga wakisaidiwa na asasi na mawakala wa kiutawala wanaohitajika. Katika kukiongoza kikundi kupitia kitabu hiki, mkufunzi anapaswa akumbuke kwamba washiriki wanaandaliwa kujiunga na juhudi endelevu kama hiyo. Ziara zilizoandaliwa kwa ajili yao kama kipengele cha ujifunzaji wao, zinapaswa zipelekee kwenye kujizatiti kushiriki katika juhudi hii mwaka hadi mwaka, ambayo ni sura muhimu ya maisha ya huduma.

Desturi ya kutembelea nyumba kwa ajili ya kusudi maalum la kuchunguza dhima muhimu za kiroho na kijamii hutajirisha kwa uwazi utamaduni wa jumuiya. Vilevile muhimu katika suala hili ni mazungumzo mengi yasiyo rasmi yanayofanyika nyumbani na katika mahala pa kazi, shuleni na sokoni. Kutambulisha kanuni za kiroho katika mazungumzo ya kila siku mara kwa mara, kwa hiyo, ni uwezo unaostahili umakini. Ukuzaji wake ni lengo la kitengo cha pili, na kuweka msingi kwa namna hii kwa ajili ya masomo yatakayofanyika katika kitengo cha tatu.

Kama mazungumzo yetu na marafiki na majirani yanatakiwa kuwa yainuayo, lazima tuweze kuleta furaha kwenye mwingiliano wetu nao. Hii ni mada inayoongelewa katika kitengo cha kwanza,“Furaha ya Ufundishaji”. Vitendo vyote vya huduma vilivyopendekezwa na Taasisi ya Ruhi kimsingi vinahusu kushirikiana na wengine lulu za busara takatifu ambazo tunagundua katika bahari ya Ufunuo wa Bahá’u’lláh. Usomaji wa kitengo cha kwanza umekusudiwa kuongeza utambuzi wa furaha iliyomo kiasili katika wajibu huu. Washiriki wanaombwa katika sehemu kadhaa, kufikiria juu ya Neno la Mungu na, ni baraka iliyoje kuweza kushirikiana na watu wengine Neno hilo. Kutoka kitendo hiki, kitengo kinapendekeza, kuinua furaha ambayo huhuisha hatua zetu kadiri tutembeavyo kwenye njia ya huduma. Walakini, hata baada ya kuwa na uhakika kamili kuhusu ukweli huu wa kina wa kiroho, tunaweza kupoteza furaha ya ufundishaji kama tutashindwa kufikiria sifa na mielekeo ambayo lazima ipambanue huduma. Sifa na mielekeo hii ndiyo malengo ya mjadala katika vitabu vingi vinavyofuata katika mlolongo huu, na ni chache tu ambazo zinachunguzwa hapa, zikianza na kujitenga katika Sehemu ya 7. Makusanyo ya vifungu kutoka Maandiko ya Kibahá’í huunda msingi kwa ajili tafakari juu ya sifa hii, sifa ya lazima kama hatutaki vigezo

vya nje vipunguze furaha ya huduma. Jambo muhimu ni kwamba washiriki wasiondoke kwenye masomo na wazo potofu kwamba kujitenga humaanisha kutokujali au kutokuwa makini. Lazima tuendelee kujitahidi kuongeza juhudi zetu na kuongeza ufaaji wa huduma yetu kadri tunavyojitahidi kupata matokeo mazuri zaidi na zaidi. Hii inahitaji uelewa wa kutosha wa tabia ya juhudi, mada ambayo inaongelewa katika Sehemu ya 8. Matumaini na shukrani, mielekeo miwili ya msingi kwenye njia ya huduma, inaongelewa kwa kifupi katika sehemu inayofuata na ya mwisho.

Kitengo cha pili cha kitabu hiki, "Mazungumzo Yainuayo", hulenga juu ya uwezo wa kuinua kiwango cha mazungumzo yasiyokuwa rasmi kwa kurejea kwenye kanuni za kiroho wakati nafasi inaporuhusu. Kina jumuisha idadi ya kauli fupi juu ya mada mbalimbali, ambazo, ingawa siyo vifungu kamili, zinatokana na matamshi ya 'Abdu'l-Bahá na yanajumuisha maneno mengi na vifungu vya maneno Alivyotumia. Zikiwa zenye mvuto wa ujumla, kauli zinaongelea matumaini na masuala ya watu wa usuli wote. Inategemewa kuwa kwa kusoma kauli hizi, washiriki wataweza kuchota uvuvio kutoka namna ambavyo 'Abdu'l-Bahá alieleza kanuni za kiroho na watajenga tabia ya kumtazama Yeye kadiri wajitahidivyo kugundua lulu zilizomo katika bahari ya Ufunuo wa Bahá'u'lláh, kuelewa maana na matarajio ya mafundisho ya Baba Yake, na kushirikiana kwa ukarimu na wengine.

Ili kufanikisha malengo ya kitengo hiki, washiriki wanapaswa kupewa fursa ya kupitia kila kauli mara kadhaa, kuainisha mlolongo wa mawazo, na kufanya zoezi la kuyasema hadi wameyaingiza mawazo hayo akilini kwa kiwango kitakacho waruhusu kuyasema kama jambo la kawaida. Baadhi, mwanzoni, kimsingi wataweza kukariri kauli na kuzirudia karibu sawa na zilivyo katika kitengo. Hili linapaswa kutarajiwa. Kadiri ujuzi wao wa Imani unavyoongezeka na uzoefu unavyokua, ndivyo watakavyoweza kuyafikia maudhui mapana zaidi na misamiati tajiri zaidi, ambayo itatafakariwa katika mwingiliano wao na wengine. Mkufunzi anapaswa kutambua kwamba kwenye hatua hii, kinachotafutwa ni cha pande mbili: kiwango cha urahisi katika kuelezea mafundisho na kuendana na fikra za 'Abdu'l-Bahá.

Baada ya wajumbe wa kikundi kujifunza jinsi ya kuwasilisha maudhui ya kila kauli, wanaendelea kwenye shughuli nyingine ambamo wanatiwa moyo kulinganisha mawazo waliyojifunza na masuala yanayohusiana na familia zao, marafiki, na wafanyakazi wenza. Hadi hapa, wanaombwa kufikiria juu ya baadhi ya mada na maswali yaliyoibuliwa katika mazungumzo na kuamua ni yapi yangewapa fursa ya kutambulisha mawazo katika mjadala. Kwa kauli chache, mfano mmoja au miwili imetajwa ili kuonesha jinsi kanuni za kiroho zilizofundishwa na 'Abdu'l-Bahá zinavyoangazia masuala yanayowahusu watu kila mahali. Zoezi hili litazaa matunda mazuri zaidi ikiwa, wakati usomaji wa kitabu ukiwa unaendelea, mkufunzi ataweza kumsaidia kila mjumbe katika kuchagua mojawapo ya kauli, na idadi kadhaa ya watu wa kuzungumza nao juu ya mawazo yaliyomo katika kauli hiyo. Kwa njia hii, muda unaweza kutengwa kwa ajili ya washiriki, pale wanapokutana pamoja, kwa ajili ya kuelezea mmoja kwa mwingine mwenendo wa mazungumzo ambamo wameshiriki.

Kwa kila kauli katika kitengo hiki, vifungu vichache kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh vimejumuishwa kwa ajili ya kukariri. Mkazo ambao Taasisi ya Ruhi huuweka kwenye kukariri, ambao tayari ni dhahiri katika kitabu cha kwanza katika mlolongo huu, unawekewa mkazo zaidi katika Kitabu cha 2. Inasadikika kwamba, hadi sasa, washiriki wanautambuzi wa chakula cha kiroho wakipokeacho pale wanapokumbuka vifungu kutoka Maandiko mara na tena. Katika kitabu hiki, basi, watatafakari zaidi juu ya athari za Neno la Mungu kwenye moyo wa mwanadamu, na katika kitengo cha tatu, sawa na katika kile cha

pili, watajifunza kuwasilisha kanuni na mawazo yanayopatikana katika Maandiko katika kauli zao na, pale panapofaa, wananukuu vifungu moja kwa moja. Kueleza mafundisho kwa usahihi, kuyatoa kwa wengine kama yalivyo, ni miongoni mwa uwezo ambao sote tunajitahidi kukuza kadri tunavyotembea kwenye njia ya huduma. Ya kwamba mahali pazuri kabisa pa kuanzia ni kusoma maelezo ya 'Abdu'l-Bahá na kujaribu kuyaelezea kama Alivyofanya Yeye, ndiyo dhana ya msingi wa muundo wa kitengo cha pili.

Kama ilivyooneshwa hapo juu, kitengo cha tatu, kiitwacho "Dhima za Kujiongezea Elimu Zaidi", hugeukia kwenye kitendo cha huduma kinachoshughulikiwa katika kitabu hiki — kwa maneno mengine, kufanya ziara kwa marafiki na majirani kwa ajili ya kusudi dhahiri la kushiriki majadiliano ambayo ni muhimu kabisa kwa maisha ya jumuiya. Aina tatu za mazungumzo yanatazamiwa katika kitengo hiki na, kwa kila mojawapo, maudhui mahsusi yamependekezwa. Aina ya kwanza yanazungukia mlolongo wa dhima zinazotakiwa kuchunguzwa pamoja na wakazi wa kijiji au ujirani katika programu ya ziara zenye mpangilio. Ingawa maudhui yaliyoainishwa yangeweza kuchunguzwa pamoja na hadhira yenye shauku katika njia mbalimbali, kusudi la msingi la dhima hizi — kuwapa wajumbe wa kaya fursa ya kuongeza kwa kina ujuzi wao wa Imani — linaendelea kuwa lenye kuhusika kabisa. Sehemu kubwa zaidi ya kitengo, kwa hiyo, imetolewa kwa ajili ya aina hii ya mazungumzo.

Hata hivyo, desturi ya kutembelea nyumba imepata sura mpya katika miaka ya hivi karibuni, hususani katika maeneo madogo madogo zaidi na zaidi ya kijiografia, hadi kufikia ngazi ya kijiji na ujirani wa mijini, yameshuhudia uibukaji wa idadi ya watu binafsi wanaoweza kutenda kama wakufunzi, wahuishaji wa vikundi vya vijana chipukizi, na walimu wa madarasa ya watoto. Haswa, desturi imejionesha kuwa ya muhimu siyo tu kwa ajili ya kusudi la kusambaza ujuzi wa Imani; pia ni ya lazima kwa ukunjukaji wenye mafanikio wa programu kwa ajili ya uwezeshwaji wa kiroho wa vijana chipukizi na kwa ajili ya elimu ya kiroho ya watoto. Katika hili, kilichodhihirika ni kwamba ziara za kila mara zinapaswa kufanywa na wahuishaji na walimu kwa wazazi wa vijana chipukizi na watoto waliomo katika programu hizi mbili ili kujadiliana dhana na mbinu zinazozipa umbo. Majadiliano kama hayo hujumuisha aina ya pili ya mazungumzo, ambayo yanachunguzwa katika Sehemu ya 14 na ya 15. Maudhui yanayoongelewa katika sehemu hizi siyo mapana asilani, kwa kuwa washiriki watajifahamisha zaidi na programu hizi mbili za kielimu katika kozi zijazo. Lakini ili waweze kutambua umuhimu wa aina hii ya mazungumzo, na ili kuambatana na walimu wa watoto na wahuishaji wa vikundi vya vijana chipukizi kwenye ziara zao kwa wazazi kinaweza kuwa kitendo chenye mafanikio na kuzaa matunda katika hatua hii ya awali.

Aina ya tatu ya mazungumzo inayotazamiwa katika kitengo hiki inasaidia kusudi maalum kabisa. Vijana wengi wa kike na wa kiume wanatafuta njia ambamo kupitia humo azma yao kuu ya kuchangia katika uboreshaji wa ulimwengu inaweza kutimizwa. Wanawakilisha akiba kubwa sana ya uwezo wa kubadilisha jamii inayosubiri, lakini, inayotamani sana kuchotwa. Mazungumzo miongoni mwa wanarika ambamo wao hutafakari juu ya fursa na majukumu ya kipekee kwa kipindi hiki cha ujana, pamoja na nguvu zake zote na uwezo usiokuwa wa kawaida uliojificha humo, mara nyingi inaweza kupelekea kwenye mjadala wa kuzungukia huduma na kuwasha shauku katika kazi inayoendelea kufanyika katika vijiji na ujirani duniani kote. Kama matokeo, wengi wao, watafurahia mwaliko wa kujiunga na kozi za Taasisi kama njia ya kupata uwezo wa kutoa elimu ya kiroho kwa vizazi vinavyoendelea kukua vya walimu wa madarasa ya watoto na wahuishaji wa vikundi vya vijana chipukizi. Sehemu ya 9 na ya 10 zimeweka mawazo machache ambayo yanaweza kuchunguzwa katika aina hii ya mazungumzo.

Ili kuimarisha uwezo unaowawezesha watu binafsi kuanzisha na kudumisha mazungumzo ya maana, kitengo hiki lazima bila shaka kitaenda mbele zaidi ya kupendekeza mada pana na maudhui yanayowiana. Mbali na uwezo wa kuelezea mawazo kwa ufasaha, washiriki wanahitaji kukuza mielekeo na sifa za kiroho zihitajikazo. Hizi zinashughulikiwa kwa sehemu kubwa ya maelezo yanayokunjuka katika kitengo hiki, lakini umuhimu wake kwa uwezo husika unawekwa wazi katika Sehemu ya 4, ambapo washiriki hufikiria kuhusu aina gani ya hisia na fikra zinazopaswa kujaza mioyo na akili zetu katika kujiandaa na ziara, na katika Sehemu ya 5, ambapo wanatafakari juu ya sifa ya unyenyekevu. Mkufunzi atataka kuhakikisha kuwa sehemu hizi zinapokea umakini wa kutosha wa washiriki, kwa sababu, haidhuru kiasi gani cha ujuzi tuupatao, haijalishi tunaweza kuelezea mawazo kwa ufasaha kwa kiasi gani, ufanisi wa mazungumzo yetu utategemea juu ya sifa na mielekeo tunayoileta kwayo.

Inapaswa kukumbukwa kwamba vitendo vya huduma vilivyoelezwa katika mlolongo huu wa vitabu, ingawa ni muhimu kwa ukuaji na maendeleo ya jumuiya, juu ya yote ni vipengele vya mchakato unaotafuta kuinua uwezo binafsi kupitia mafunzo na utendaji. Kile ambacho kila mkufunzi anapaswa kutambua ni kwamba vitendo hivi hujengwa kimoja juu ya kingine, vikiongezeka katika utata kutoka kitabu kimoja hadi kingine. Kujifunza kutekeleza kila kitendo cha huduma ipasavyo huthibitisha kuwa muhimu kwa uwezo unaohitajika kutekeleza yale yanayofuata. Ili kudumisha mazungumzo yanayoendelea katika kipindi cha ziara kadhaa kwenye nyumba moja, kama ilivyopendekezwa katika kitabu hiki, ni dhahiri kuwa vigumu zaidi kuliko shughuli iliyohamasishwa katika Kitabu cha 1, ile ya kukaribisha mkutano wa ibada wa mara kwa mara, kama ni mtu binafsi mwenyewe au kwa ushirikiano pamoja na wengine wachache. Na sio vigumu kuona jinsi gani, kutekeleza vitendo vya huduma vyenye utata zaidi katika siku za usoni, itakuwa ya lazima kwa washiriki kuendelea katika uwezo uliyoelezwa hapa.

Kama ilivyotajwa katika maelezo ya utangulizi katika Kitabu cha 1, washiriki katika kozi za Taasisi duniani kote huja kutoka usuli anuai na, mwanzoni, wana kuwa na viwango tofauti vya ufahamivu wa mafundisho ya Kibahá'í. Watakapoanza kitabu hiki cha pili, bila shaka kila mmoja na wote atakuwa, ameanza kutembea kwenye njia ya huduma inayofunguliwa na kozi. Walakini tofauti chache hubakia. Kuhusu vijana kwa mfano, kama hawajapitia programu za kielimu kwa ajili ya watoto na vijana chipukizi, kauli nyingi na dhima zilizowasilishwa katika kitabu hiki zitakuwa mpya kwao, na usomaji wake utatumika kama njia kwa ajili yao kuongeza kwa kina ujuzi wao wenyewe wa Imani. Mkufunzi anapaswa kuwa tayari katika suala hili kuonesha unyumbulifu na ubunifu unaohitajika kwa ajili ya kulea uelewa katika kila mjumbe wa kikundi, huku akihakikisha kuwa lengo kuu la kozi, kuwawezesha washiriki kujihusisha katika mazungumzo ya maana na yainuayo, linafikiwa. Zaidi ya hivyo, katika maelfu ya maeneo ambako kitabu hiki kinatumiwa, mchakato wa ujenzi wa jumuiya ambamo vitengo hivi vitatu vinataka kuchangia haupo katika hatua sawa ya maendeleo. Kuweka katika vitendo kile wanachojifunza, hivyo, kunaweza kuchukua sura tofauti kutoka sehemu moja hadi nyingine, na hili pia, hutoa ishara ya kujali na umakinifu ambao mkufunzi lazima aitikie kwenye mahitaji ya kila mjumbe wakati wa kukipitisha kikundi katika kurasa hizi.



# Furaha ya Ufundishaji

## Kusudi

Kuthamini kwamba furaha ya Ufundishaji imo katika kitendo chenyewe cha kushirikiana na wengine Neno la Mungu

## SEHEMU YA 1

*Uinukaji kwa Kuhudumu* ni kitabu cha pili katika mlolongo wa kozi zinazotolewa na Taasisi ya Ruhi ambacho kinatafuta kuunganisha mafunzo na vitendo. Lengo lake ni kuwasaidia ninyi kuendelea mbele zaidi katika njia ya huduma ambayo mmeingia kadiri mjitahidivyo kutimiza kusudi lenye pande mbili: kufuatilia ukuaji wenu wenyewe wa kiroho na wa kiakili na kuchangia kwenye mabadiliko ya jamii. Kutoka kwenye ushiriki wenu katika kozi ya kwanza, lazima mtakuwa mmekwisha tambua kuwa njia tunayoiongelea inaainishwa kwa mlolongo wa vitendo vya huduma, vitendo ambavyo huwa tunavitekeleza huku macho yetu yakiwa yamekaziwa kwenye lengo la utaratibu mpya wa ulimwengu kama ulivyotazamiwa katika maandiko ya Bahá'u'lláh. Hivyo sehemu kubwa ya kile tunachokiita, "kutembea kwenye njia ya huduma" hujumuisha juhudi zetu za kutumia mafundisho Yake katika maisha yetu wenyewe na kwenye maisha ya jamii ya binadamu. Yeye mwenyewe huongea juu ya ufunuo wake katika maneno haya:

> **"Enyi watumishi Wangu! Ufunuo Wangu mtakatifu, ulioamriwa na Mungu unaweza kufananishwa na bahari ambayo katika vina vyake zimefichwa lulu zisizohesabika za thamani kuu, za mg'ao wa kuzidi. Ni wajibu wa kila mtafutaji kujiamsha mwenyewe na kujitahidi kufikia fuko za bahari hii, ili aweze, kulingana na shauku ya utafutaji wake na jitihada ambayo ameifanya, kujitwalia manufaa yale ambayo yameamriwa mbele katika Nyaraka za Mungu zisizo batilika na zilizofichwa."[1]**

Katika kitengo hiki cha kwanza, fikra zetu zinageukia kwenye furaha ambayo huijaza mioyo yetu kadri tunavyogundua lulu za busara zilizomo katika bahari ya Ufunuo wa Bahá'u'lláh na kushirikiana na wengine. Tayari kutoka ujifunzaji wenu wa Kitabu cha 1 mmeona jinsi gani zilivyo zenye uzuri wenye unadhifu lulu za mwongozo mtakatifu zinazopatikana katika Maandiko Yake. Hebu tufikirie zaidi juu ya baadhi ya nukuu:

> **"Matamshi ya Mungu ni taa, ambayo mwanga wake ni maneno haya: Ninyi ni matunda ya mti mmoja, na majani ya tawi moja."[2]**

> **"Kipenzi kabisa kuliko vitu vyote mbele ya macho Yangu ni Haki; usiikwepe haki ikiwa unanihitaji Mimi, na wala usiipuze, ili Mimi nipate kukufanya kuwa msiri Wangu."[3]**

> **"Jalini sana kuhusu mahitaji ya zama hizi mnamoishi, na kazieni majadiliano yenu kwenye mahitaji na matakwa yake."[4]**

> **"Watu wote wameumbwa kuendeleza mbele ustaarabu uendeleao daima."[5]**

> **"Ulimwengu unapita, na kile ambacho hudumu milele ni upendo wa Mungu."[6]**

> **"Wewe ni taa Yangu na nuru Yangu imo ndani mwako. Pata mng'ao wako kwayo na usitafute mwingine zaidi Yangu. Kwa maana Nimekuumba tajiri na kukupa baraka Zangu kwa wingi."[7]**

Pengine mngependa kukariri vifungu hivi vifupi kadri muda unavyopita.

## SEHEMU YA 2

Ili kuanza majadiliano yenu juu ya dhima kuu za kitengo hiki, someni tena kifungu cha kwanza kilichonukuliwa katika sehemu iliyotangulia na fanyeni mazoezi yafuatayo.

1. Kamilisheni sentensi zilizopo hapo chini:

   a. Ni wajibu wetu ku ___________________ wenyewe na ____________________ ___________________ za bahari ya Ufunuo wa Bahá'u'lláh.

   b. Tunapaswa kujitahidi kufikia fuko za bahari ya Ufunuo wa Bahá'u'lláh ili tuweze kujitwalia _____________________ ambayo yameamriwa mbele katika Nyaraka za Mungu zisizo batilika na zilizofichwa.

   c. Manufaa tunayojitwalia ya bahari ya Ufunuo wa Bahá'u'lláh yatakuwa yenye uwiano na ________________________________________________________ ___________________ .

2. Nini maana ya "kujiamsha" mwenyewe? __________________________________
   ____________________________________________________________________

3. Nini maana ya "kujitahidi kufikia" kitu fulani? ______________________________
   ____________________________________________________________________

4. Kila mtafutaji anapaswa kujitahidi kufikia kitu gani? _________________________
   ____________________________________________________________________

5. Inamaanisha nini kwa kitu kimoja kuwa na "uwiano" na kingine? ______________
   ____________________________________________________________________

6. Bahá'u'lláh hutuambia kwamba tutapokea manufaa ya bahari ya Ufunuo Wake kulingana na juhudi tuzifanyazo.

   a. Toeni baadhi ya mifano ya juhudi tuzifanyazo ambazo hutufanya kuwa wapokeaji wa manufaa haya: ____________________________________________
   _________________________________________________________________
   _________________________________________________________________
   _________________________________________________________________
   _________________________________________________________________
   _________________________________________________________________

   b. Toeni baadhi ya mifano ya manufaa tuyapokeayo: ________________________
   _________________________________________________________________

____________________________________________________

____________________________________________________

____________________________________________________

____________________________________________________

## SEHEMU YA 3

Kufahamu kuwa Ufunuo wa Bahá'u'lláh ni kama bahari ambamo katika vina vyake zimo lulu zenye thamani isiyokadirika, kila mmoja wetu anafanya juhudi kubwa ili kujitwalia manufaa yake na kuwasaidia wengine kufika kwenye fuko zake. Lakini, tunaweza kujiuliza, fuko za bahari hii ziko umbali gani kutoka kwetu? Bahá'u'lláh hutangaza:

> **"Enyi watumishi Wangu! Mungu mmoja wa kweli ni shahidi Yangu! Bahari hii kuu kabisa, bahari ya kina kisichopimika na isukasukayo iko karibu, karibu mno kwenu, ishangazavyo. Tazama kama ipo karibu zaidi nanyi kuliko mshipa wa uhai wenu ! Haraka kama kufumba na kufumbua kwa jicho mnaweza, kama tu mkipenda, kuifikia na kujitwalia fadhili yake isiyopotea, neema hii itolewayo na Mungu, zawadi hii isiyoharibika, baraka hii ya nguvu kuu mno na tukufu isiyosemeka."[8]**

1. Kifungu cha maneno "bahari hii kuu kabisa, bahari hii ya kina kisichopimika isukasukayo" hurejea kwenye nini? ______________________________________

2. Bahari hii ipo karibu nasi kiasi gani? ______________________________________

   ________________________________________________________

3. Ni kwa haraka kiasi gani tunaweza kuifikia bahari hii? ________________________

   ________________________________________________________

4. Kamilisheni sentensi zifuatazo:

   a. Bahari kuu kabisa ya Ufunuo wa Bahá'u'lláh ipo karibu, karibu mno kwenu, ______________________________ .

   b. Bahari ya Ufunuo wa Bahá'u'lláh ipo _____________ nasi kuliko mshipa wa uhai wetu.

   c. Haraka kama _____________________________________ tunaweza, kama tu tunapenda, _______________ na ______________________ ya bahari ya Ufunuo Wake.

   d. Haraka kama kufumba na kufumbua kwa jicho tunaweza, _____________________ , kuifikia na kujitwalia kutoka bahari ya Ufunuo Wake.

## SEHEMU YA 4

Baada ya kufika kwenye fuko za bahari ya Ufunuo wa Bahá'u'lláh, tunachota kutoka hazina zake na kushirikiana kwa uhuru na bila masharti na wengine lulu za mwongozo mtakatifu, ambazo tunaendelea kuzigundua katika ujifunzaji wetu wenyewe, sala na tafakari na katika juhudi zetu kuhudumia Hoja Yake na jamii ya binadamu. Pengine mngependa kuchukua muda kidogo kukariri kifungu kinachofuata, ukumbusho endelevu wa utakatifu wa jukumu hili:

> **"Ee Msafiri katika njia ya Mungu! Twaa sehemu yako ya bahari ya neema Yake, na usijinyime mwenyewe vitu vile ambavyo vimefichwa katika vina vyake. Uwe miongoni mwa wale ambao wameshiriki katika hazina zake. Tone moja la umande kutoka bahari hii, kama lingemwagwa juu ya vile vyote vilivyomo mbinguni na duniani, lingetosheleza kuwatajirisha kwa baraka ya Mungu, Mweza, Mjua yote, Mwenye hekima kabisa. Kwa mikono ya kujikana teka kutoka maji yake yatiayo uzima, na unyunyizie kwayo viumbe vyote, ili viweze kutakaswa kutoka vizuizi vyote vya kibinadamu na viweze kukaribia kiti cha nguvu cha Mungu, Mahali hapa palipotukuzwa na angavu."**[9]

## SEHEMU YA 5

Kadri tunavyoendelea kupitia Kozi za Taasisi, tukitekeleza mafunzo na vitendo vihitajikavyo, uwezo wetu kwa ajili ya huduma utakua, na tutaweza kufanya vitendo vya huduma ambavyo vinaleta furaha kubwa kwenye mioyo yetu na vinatusaidia katika kutimiza kusudi letu lenye pande mbili — vitendo kama vile kufundisha madarasa kwa ajili ya elimu ya kiroho ya watoto, kuwahusisha vijana chipukizi katika programu kwa ajili ya uwezeshwaji wao wa kiroho, kusaidia kikundi cha marafiki kujifunza vitabu vya mlolongo mkuu. Katika safari nzima, Neno la Mungu, ambalo tutakuwa tunashirikiana na wengine, vijana na wazee, litakuwa chanzo chetu endelevu cha hamasa. Ni sawa tu basi, kuwa tunapaswa kutafakari mara kwa mara juu ya nguvu yake na athari yake kwenye moyo wa binadamu. Katika kifungu kifuatacho, Bahá'u'lláh huongelea juu ya nguvu hii:

> **"Neno la Mungu laweza kufananishwa na mmea mchanga, ambao mizizi yake imepandikizwa katika mioyo ya watu. Imewapasa kusaidia ukuaji wake kwa maji ya uzima ya hekima, ya maneno yaliyo takasika na matakatifu, ili kwamba mizizi yake iweze kuwa imewekwa imara na matawi yake yaweze kutanda hadi juu mbinguni na zaidi."**[10]

1. Neno la Mungu linaweza kulingalishwa na nini? ______________________________

   ________________________________________________________________________

2. Mizizi ya mti wa Neno la Mungu imepandwa wapi? ___________________________

   ________________________________________________________________________

3. Tunapaswa kuleaje ukuaji wa mti huu? ______________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

4. Mti huu unaweza kukua hadi kufikia kimo gani? ______________________________

______________________________________________________________________

5. Elezeeni katika sentensi chache kwa nini kushirikiana Neno la Mungu na watu wengine ni jambo lenye umuhimu mkubwa kabisa.

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

## SEHEMU YA 6

Hebu tufikirie shughuli mbalimbali tunazojishughulisha nazo katika maisha yetu ya kila siku. Tunailisha miili yetu. Tunajifunza ili tupate ujuzi mpya na kupanua uwezo wetu wa kiakili. Tunafanya kazi na tunakuza stadi zinazotuwezesha kuishi kama wajumbe wenye manufaa kwa jamii. Tunajihusisha katika michezo na burudani. Shughuli lukuki kama hizi, zote muhimu kwa ajili ya maendeleo yetu ya kiakili na ustawi wa kimwili, huchukua sehemu kubwa ya muda wetu. Lakini hata hivyo, kuna zile nyakati maalum kwa kila siku, ambazo zimejazwa na hali ya kiroho, tunapojihusisha katika sala; tuponajiimarisha, peke yetu au pamoja na marafiki, juu ya ufahamu wetu wa mafundisho matakatifu; au katika njia nyingi, tunapowasaidia wale wanaotuzunguka kugundua lulu zilizofichika katika bahari ya Ufunuo wa Bahá'u'lláh. Je, hizi siyo nyakati zenye thamani kubwa isiyoweza kupimika? Kuna furaha kubwa zaidi kuliko kuweza kujitwalia baraka hizi za mbinguni?

Tunapaswa kila mara tukumbuke jinsi 'Abdu'l-Bahá alivyotutia moyo kujitolea wakfu kwa ajili ya uinuaji jamii ya binadamu:

> **"Sisi sote tumeungana kwa kusudi moja Takatifu, hatuna haja na anasa, na matakwa yetu hasa ni kueneza Mapenzi ya Mungu kote duniani!"[11]**

Endapo fursa imejitokeza kwa ajili yenu kushirikiana pamoja na rafiki mmoja mojawapo ya vifungu kutoka Sehemu ya 1 ambacho mmekikariri. Ile furaha mnayohisi katika mioyo yenu inatoka wapi? Kiasilia, mnatarajia kuwa rafiki yenu atainuliwa kwa maneno ya Bahá'u'lláh. Lakini itakuwaje kama yeye haoneshi shauku kama mlivyokuwa mnatarajia? Je, furaha iliyomo katika mioyo yenu itapotea kirahisi tu? Kwa nini haitapotea?

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

## SEHEMU YA 7

Wakati tunapotambua kuwa, kati ya vitu vyote tuvifanyavyo katika maisha yetu, nyakati tunazotumia kushirikiana Neno la Mungu na wengine zimejaliwa baraka maalum, tunafikia kwenye hitimisho lenye umuhimu kabisa: kwamba furaha tunayoipata inatokana na huduma iliyomo katika kitendo chenyewe. Tunatarajia, bila shaka, kuwa vitendo vya huduma tunavyofanya vitaleta matokeo stahiki, lakini ikiwa tunajiambatanisha mno na matokeo, ikiwa tunaathiriwa zaidi na sifa au ukosoaji tunaoupata, tutapoteza furaha ya ufundishaji. Kile ambacho kinapaswa kutupa shauku ya kuhudumia ni upendo wa Mungu, wala siyo shauku ya kupata mafanikio, kupata manufaa, au kutambulika. Kujitenga kutoka vyote hivi ni kigezo cha huduma yenye furaha. Usomaji wa mateuzi yafuatayo kutawasaidia kutafakari juu ya dhima hii.

> **"Ewe Mwanadamu Mwenye Peo Mbili! Fumba jicho moja na kulifumbua lingine. Fumba moja kwa dunia na yote yaliyomo humo, na fumbua lingine kwa uzuri uliotukuka wa Mpendwa."[12]**

> **"Enyi Rafiki! Msiutupe hata uzuri wa milele kwa ajili ya uzuri ambao hauna budi ufe, na msiweke shauku yenu katika dunia hii ya kufisha ya vumbi."[13]**

> **"Ewe Mwana wa Neno! Geuza uso wako kuelekea uso Wangu na kuwakana wengine wote ila Mimi, kwa maana enzi Yangu hudumu na Ufalme Wangu haupotei kamwe. Ikiwa utajitafutia mwengine zaidi Yangu, naam, kama ukitafuta daima katika ulimwengu mzima, utafutaji wako utakuwa bure."[14]**

> **"Ewe mgeni Uliyefanywa rafiki! Mshumaa wa moyo wako huwashwa kwa mkono wa uwezo Wangu, usiuzime kwa pepo za upinzani za nafsi na shauku. Mponyaji wa maradhi yako yote ni kunikumbuka Mimi, usisahau jambo hilo. Ufanye upendo Wangu kuwa hazina yako na uutunze kama macho yako mwenyewe na uhai."[15]**

> **"Kujitenga ni kama vile jua; ndani ya moyo wowote ule ambamo huwaka huzima moto wa tamaa na nafsi. Yeye ambaye kuona kwake kumeangaziwa na mwanga wa ufahamu kwa hakika atajitenga mwenyewe kutoka ulimwengu huu na mambo yake yasiyofaa. . . . Usiache ulimwengu na uchafu wake vikuhuzunishe. Ni mwenye furaha yule ambaye utajiri haumjazi majivuno, wala umaskini huzuni."[16]**

1. Je kujitenga kutoka ulimwengu huu unamaanisha kuishi kama mtawa? ___________

2. Inawezekana kujitenga kutoka ulimwengu huu na wakati huo huo kumiliki mali? ___________

3. Je, yule mtu ambaye anajitolea takribani kila saa ya maisha yake kwa kazi zake amejitenga kutoka vitu vya ulimwengu huu? ________________________________

4. Je, mtu ambaye hufanya kazi kiasi tu kutosheleza mahitaji yake ya kimsingi na hutumia wakati wake uliobaki bila kufanya chochote amejitenga kutoka ulimwengu huu? ________________________________________________________________

5. Je, mtu ambaye hawezi kuvumilia shuruba katika uwanja wa huduma amejitenga kutoka ulimwengu huu? ________________________________________________

6. Kuna vitu vingi ambavyo tunaweza kujiambatanisha navyo mbali na kumiliki mali. Ni kwa kitu gani mtakuwa mmejiambatanisha nacho ikiwa ninyi ni watu ambao

   – Hutaka kukata tamaa pale unapofanya kitendo cha huduma na hakuna mtu aliyekithamini? ____________________________________________________

   – Huhisi kuvunjika moyo wakati mtu mmoja hakubali mawazo anayoshiriki? _________________________________________________________________

   – Huficha imani yake kwa hofu ya kukataliwa na wengine? __________________ _________________________________________________________________

7. Kujitenga haimaanishi kutojali au kukosa umakini. Ni yapi miongoni mwa yafuatayo ambayo yanaweza kuwa ishara ya mtu ambaye hajajitenga?

   _____ Kupata furaha kwa kuona maendeleo ya wengine.

   _____ Kuacha kufundisha darasa, wakati watoto wachache wanapoonesha tabia mbaya.

   _____ Mtu kujigamba juu ya mafanikio yake.

   _____ Kusoma kwa bidii na kujihisi mwenye kuridhika na maendeleo uyafanyayo.

   _____ Kufanya kazi kwa bidii ili kukuza uwezo wa mtu kwa ajili ya kuhudumia ustawi wa wote.

   _____ Kujitahidi kufikia ubora katika kazi yake.

   _____ Kufanya usafi na kuwa na nyumba safi na yenye mpangilio.

   _____ Kujali vitu vyako.

   _____ Kujali ustawi wa watu wengine.

   _____ Kuvunjika moyo anapokuwa hasifiwi kwa juhudi anazofanya.

8. Kujitenga ni muhimu kwa ajili ya kila mmoja wetu kiasi kwamba inapendekezwa mkariri mateuzi yote yaliyomo katika sehemu hii.

## SEHEMU YA 8

Ili tuweze kupokea fadhila za maisha yenye furaha ya huduma kwa binadamu, lazima tukubali kufanya juhudi, na juhudi zetu pengine zitahitaji kiwango fulani cha dhabihu. Tunatumia neno "dhabihu" mara kwa mara katika maisha yetu ya kila siku. Kama rafiki anarudi kutoka safarini wakati wa alfajiri, tunaweza kuamka mapema kwenda kumpokea. Tunaweza kusema kwamba tumejitoa dhabihu saa chache za usingizi. Mtu fulani tumpendaye anapokuwa anaumwa, tunajitolea saa chache za muda wetu wa thamani ili kumuangalia. Kuna nyakati katika maisha ambapo lazima tufanye kazi kwa bidii sana, na tunaweza kufikiria kuwa tunajitolea dhabihu starehe ili tuweze kufikia lengo.

Sote tuna shauku kubwa ya kuhudumia Hoja, tukitoa kwa ukarimu muda wetu na nguvu zetu na, kadri iwezekanavyo, sehemu yetu ya rasilimali za kimwili. Tunapofanya hivyo, tunapaswa kukumbuka kwamba kwenye njia ya huduma tunaachana na vitu vya ulimwengu huu, lakini kile tupokeacho ni furaha ya kweli kadri tukuavyo kiroho. Tutapata fursa ya kutafakari zaidi juu ya asili ya dhabihu katika kozi zijazo. Cha muhimu kutambua toka mwanzoni kabisa ni kwamba inahusiana na kukana kile ambacho ni cha chini zaidi kwa ajili ya kile ambacho ni cha juu zaidi, sawa na ambavyo mbegu hujitoa dhabihu yenyewe ili mti uweze kuota. Dhabihu ni mchukuzi wa furaha, na furaha hii haitakuwa yetu isipokuwa kama tuko radhi kufanya juhudi endelevu.

Bahá'u'lláh husema:

> **"Jitihada inahitajika, kama tunahitaji kumtafuta Yeye; shauku kali inahitajika, kama tunataka kunywa asali ya muungano pamoja Naye; na kama tutaonja kikombe hiki, tutautupilia mbali ulimwengu huu."[17]**

Na 'Abdu'l- Bahá hutushauri:

> **". . . msipumzike, msitafute utulivu, msijifungamanishe na anasa za ulimwengu huu wa mpito, jiwekeni huru wenyewe kutoka kila mfungamano, na jitahidini kwa moyo na roho kuwekwa imara katika Ufalme wa Mungu. Pateni ninyi hazina za mbinguni. Siku hadi siku muwe mliyoangaziwa zaidi. Sogeeni karibu zaidi na zaidi katika kizingiti cha umoja."[18]**

Sote tunaamini kwamba, ili tuweze kufanikisha malengo yetu, lazima tufanye jitihada. Lakini itikadi hii ya kawaida ina matokeo fulani katika vitendo ambayo hatupaswi kuvisahau. Ni muhimu kwa mtu kukumbuka kwamba, kuna uwiano kati ya kiasi cha nguvu ihitajikayo na kiwango cha ugumu wa lengo au kazi inayofanyika. Tunajidanganya wenyewe kama tunafikiria kuwa inaweza kutimizwa kwa juhudi kidogo. Lakini ukubwa wa jitihada siyo jambo pekee la kufikiria. Lipo hitaji la uendelevu wa ustahimilivu. Umakinifu unahitajika. Tabia ya kukamilisha kazi, bila kurukaruka kutoka moja hadi nyingine na kutoiacha kazi bila kuikamilisha ni muhimu. Jitihada za shingo upande hazizai matunda. Fikiria darasa la kila juma kwa ajili ya elimu ya kiroho ya watoto. Mwalimu lazima ajitolee idadi fulani ya masaa kujiandaa kwa ajili ya kila darasa, kubakia makinifu kabisa wakati wote wa kipindi kuwasaidia wanafunzi kuelewa maudhui ya somo, kufanya ziara za mara kwa mara kwa wazazi wa watoto, na kufuatilia maendeleo ya kila mmoja, juma baada ya juma. Ni ipi hatima ya darasa ambalo mwalimu huandaa mara moja moja tu, husitisha mapema na ghafla mara achokapo, na hushindwa kutoa muda wa kutosha kwa ajili ya kufikiria juu ya kila mtoto na kujadiliana maendeleo yake pamoja na wazazi? Itakuwaje kama darasa litasitishwa

kirahisi tu wakati wowote mwalimu ajisikiapo kufanya wajibu mwingine, tuseme, kuwa pamoja na rafiki ambaye amemtembelea kutoka nje ya mji ?

Maoni haya machache yanatuthibitishia kuwa lazima tuweke umakini kwenye yote mawili kiasi na ubora wa juhudi ambayo kila shughuli tuifanyayo huhitaji. Hii ni kweli siyo tu kwa ajili ya vitendo vya huduma ambamo tunahusika; vilevile inahusika kwenye maendeleo yetu wenyewe. Hata tabia za kiroho tulizozifikiria katika kitabu cha kwanza cha mlolongo — kusali mara kwa mara, kusoma Maandiko kila siku, kutafakari jinsi ya kuyafanya maisha yetu yaendane na mafundisho, kushiriki kwa moyo wote katika mikusanyiko ya ibada — hutegemea juu ya bidii endelevu. Hapo chini zipo idadi ya kauli zihusianazo na juhudi. Kuamua zipi ni za kweli itawasaidia kutafakari zaidi juu ya jambo hili:

_____ Kama wewe ni mwerevu, huhitaji kufanya kazi kwa bidii.

_____ Kwa nini upite njia ndefu, mara zote tafuta njia ya mkato.

_____ Bila maumivu, hakuna mafanikio.

_____ Ota ndoto kubwa na matakwa yako yatakuwa kweli.

_____ Ukubwa wa tuzo huakisi ukubwa wa jitihada.

_____ Kadri juhudi inavyokuwa kubwa zaidi ndivyo zawadi inavyokuwa ya thamani.

_____ Kama mara ya kwanza hujafanikiwa, jaribu tena na tena.

_____ Kwa nini ufanye kazi ikiwa wengine wanaweza kufanya kazi kwa ajili yako?

_____ Kama juhudi nyingi zinahitajika, pengine haikumaanisha kuwa hivyo.

_____ Hatua ndogo — za mara nyingi na endelevu — zinaweza kwenda mbele.

_____ Chochote ambacho ni stahiki hakipatikani kwa urahisi.

_____ Ubora unadai kujitolea kwa moyo wote.

_____ Safari ya maili elfu moja huanza na hatua moja.

_____ Kufanya kazi ya kijuujuu haitoshi.

_____ Hatupaswi kusubiri hadi mambo yajitokeze; tunapaswa kuyatafuta.

_____ Mafanikio ni jambo la bahati tu.

_____ Hatutofikia kusudi letu la pandembili kwa muujiza.

_____ Lazima tujifanye hesabu wenyewe kila siku.

Twatembea kwenye njia ya huduma, tukijitahidi kufanikisha ukuaji wetu wenyewe wa kiroho na kiakili na kuchangia kwenye mabadiliko ya jamii. Ni dhahiri kuwa utafutaji wa kusudi hili la pande mbili hudai juhudi kubwa sana kutoka kwetu. Bahá'u'lláh hutuambia:

> **"Muumba asiye na kifani Amewaumba watu wote kutokana na kitu kile kile, na kuinua hadhi yao juu ya viumbe Wake wengine. Kufanikiwa au kushindwa, kupata au kukosa, havina budi basi kutegemea juhudi za mtu mwenyewe. Kadri anavyojibidiisha mwenyewe ndivyo kwa kiasi hicho yatakavyo kuwa makubwa maendeleo yake."**[19]

Mnaweza kukariri aya ya hapo juu kama bado hamjafanya hivyo.

## SEHEMU YA 9

Kuweza kupata furaha kutoka kwenye huduma, tunapaswa kulea mielekeo fulani ndani mwetu. Kwa mfano, lazima tuwe wenye shukrani kwa ajili ya fadhila ya huduma ambayo Mungu ametujalia juu yetu; kamwe haiwezi kudhaniwa kuwa tunamfanyia Mungu fadhila pale tunapotumikia Hoja Yake. Lazima pia tujifunze kuepukana na ukataji tamaa na kuyaendea maisha kwa mtazamo wenye matumaini ya ulimwengu. Vikwazo katika njia ya huduma vinaweza kugeuzwa kuwa mawe ya kuvukia kwa ajili ya maendeleo zaidi. Hata katikati ya matatizo, tunatazama mbele kwa macho yenye imani. Maneno yafuatayo ya 'Abdu'l-Bahá huonesha matumaini na matarajio chanya ambayo yanapaswa kuainisha juhudi zetu:

> **"Mwanzoni, ni kiasi gani mbegu ilivyo ndogo, walakini mwishowe ni mti wenye uwezo. Msiitazame mbegu, tazameni mti, na maua yake, na majani yake na matunda yake."[20]**

> **"Juwa kwa hiyo umuhimu mkubwa wa mbegu hii ndogo ambayo Mkulima wa kweli kwa mikono ya rehema Yake, amepanda kwenye mashamba yaliyolimwa ya Bwana, na kumwagiliwa na mvua ya majaliwa na fadhila na sasa inalelewa katika joto na mwangaza wa Nyota ya Mchana ya Ukweli."[21]**

> **"Pale unapouona mti ukikua na kuendelea, uwe mwenye matumaini kwa matokeo yake. Hatimaye utachanua maua na kuzaa matunda. Utakapoona kuni kavu au miti mikongwe, hakuna matumaini yoyote ya kupata matunda."[22]**

> **"Kwa hiyo lazima wapendwa wa Mungu, kwa juhudi kubwa, pamoja na maji ya jitahada zao, wanalinda na kulisha na kulea mti huu wa matumaini."[23]**

> **"Kama moyo hugeukia mbali kutoka baraka ambazo Mungu anatujaalia utategemeaje kuwa na matumaini ya kupata furaha? Kama hauweki matumaini yake na imani katika Rehema za Mungu, utaweza kupata pumziko wapi?"[24]**

Kutafakari juu ya aya za hapo juu, kamilisheni sentensi zifuatazo:

1. Mwanzoni, ni kiasi gani mbegu ilivyo ndogo, lakini mwishowe __________________ ________________________________________ .

2. Hatupaswi kutazama udogo wa mbegu lakini __________________________________ ____________________________________ .

3. Tunapaswa kutambua, basi, umuhimu wa mbegu ndogo ambayo Mungu kwa mikono ya rehema Yake, ame, ______________________________________________________ ________________________________________________________________________ ________________________________________________________________________ ________________________________________________________________________ .

4. Pale tunapouona mti ukikua na kuendelea, tunapaswa kuwa ____________________ ____________________ .

5. Pale tunapouona mti ukikua na kuendelea, tunapaswa kuwa wenye matumaini kuwa uta ____________________________________________________ .

6. Pamoja na maji ya jitahada yetu, tunapaswa ___________________________________ ________________________________________ .

7. Kama moyo hugeukia mbali kutoka baraka ambazo Mungu hujaalia ________________________________________________________________ ?

8. Kama moyo hauweki matumaini yake na imani katika Rehema ya Mungu, _____________________________________ ?

Sasa, tafakarini kwa muda kidogo: je, mnakubali kuwa roho zetu zenye furaha na matumaini zikiunganishwa na mwelekeo wa shukrani ya unyenyekevu ni chanzo cha furaha kwa wengine? Na, hebu kila mara tuweke akilini kwamba, katika kuinuka kuihudumia Hoja, tunabeba habari zenye furaha za mapambazuko ya Siku mpya, Siku ya mkusanyiko wa binadamu. Maneno ya Bahá'u'lláh hebu yadunde kwenye mioyo yetu:

> **"Ni wenye furaha wanaotenda; ni wenye furaha wanaoelewa; ni mwenye furaha mtu ambaye ameshikilia kwenye ukweli, amejitenga kutoka vyote vilivyomo mbinguni na vyote vilivyomo duniani."[25]**

## MAREJEO


1. *Makusanyo kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'i, 1983, 2017 kuchapa), CLIII, aya. 5, uk. 369.

2. Kama hapo juu., CXXXII, aya. 3, uk. 326.

3. Bahá'u'lláh, *Maneno Yaliyofichwa* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'i, 2003, 2012 kuchapisha), Kiarabu na. 2, uk. 3.

4. *Makusanyo kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh*, CVI, aya. 1, uk. 241.

5. Kama hapo juu., CIX, aya. 2, uk. 243.

6. Bahá'u'lláh, katika *Wanawake: Makusanyo kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh, 'Abdu'l-Bahá, Shoghi Effendi na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu*, yalikusanywa na Ifara ya Utafiti ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, Kuchapishwa 1986, 1997), na. 53, uk. 26.

7. *Maneno Yaliyofichwa*, Kiarabu, na. 11, uk. 6.

8. *Makusanyo kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh*, CLIII, aya. 5, uk. 370.

9. Kama hapo juu., CXXIX, aya. 1, uk. 316.

10. Kama hapo juu., XLIII, aya. 9, uk. 109.

11. Kutoka hotuba iliyotolewa mnamo tarehe 19 Novemba 1911, iliyochapishwa katika *Mazungumzo ya Paris: Yaliyowasilishwa na 'Abdu'l-Bahá 1911* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2006, 2016 kuchapisha), na. 32.2, uk. 121.

12. *Maneno Yaliyofichwa*, Kiajemi na. 12, uk. 26.

13. Kama hapo juu., Kiajemi na. 14, uk. 26.

14. Kama hapo juu., Kiarabu na. 15, uk. 7.

15. Kama hapo juu., Kiajemi na. 32, uk. 33.

16. Bahá'u'lláh, katika *Ulimwengu wa Kibahá'í: V. 1, 1925–1926* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í,kuchapishwa 1926, 1980 ), uk. 42.

17. *Mwito wa Wapendwa wa Watakatifu: Kazi zilizochaguliwa za Mafumbo ya Bahá'u'lláh* (Haifa: Makao Makuu ya Ulimwengu ya Kibahá'í, 2018), na. 2.12, uk. 17.

18. *Nyaraka za Mpango Mtakatifu: Zilizofunuliwa na 'Abdu'l-Bahá kwa ajili ya Wabahá'í wa Amerika ya Kaskazini* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1993, 2006 kuchapishwa), na. 13.6, ku. 95–96.

19. *Makusanyo kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh*, XXXIV, aya. 8, uk. 91.

20. *Makusanyo kutoka Maandiko ya 'Abdu'l-Bahá* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2010, 2015 kuchapishwa), na. 40.3, ku. 118–19.

21. Kama hapo juu., na. 40.3, uk. 119.

22. Kutoka mazungumzo yaliyotolewa 11 Mei 1912, yaliyochapishwa katika *Uenezaji wa Amani ya Ulimwengu: Mazungumzo Yaliyowasilishwa na 'Abdu'l-Bahá wakati wa ziara Zake Marekani na Canada mnamo 1912* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2012), aya. 2, uk. 153.

23. *Makusanyo kutoka Maandiko ya 'Abdu'l-Bahá*, na. 206.13, ku. 356–57.

24. Kutoka hotuba iliyotolewa na 'Abdu'l-Bahá mnamo 21 Novemba 1911, iliyochapishwa katika *Mazungumzo ya Paris*, na. 34.8, uk. 133.

25. Bahá'u'lláh, *Waraka kwa Mwana wa Mbwa Mwitu* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, kuchapishwa 1988, 2016), uk. 139.



# Mazungumzo Yainuayo

## Kusudi

Kupata uwezo wa kutambulisha
kanuni za kiroho kwenye mazungumzo

## SEHEMU YA 1

Katika kitengo cha kwanza cha kitabu hiki, tuliongelea furaha isiyopimika ambayo tunapata kutoka katika kitendo cha kushirikiana Neno la Mungu na wengine. Kadri tunavyotembea kwenye njia ya huduma, fursa lukuki hutujia za kujadiliana pamoja na marafiki na jamaa umaizi tunaopata kutoka Ufunuo wa Bahá'u'lláh. Miongoni mwa uwezo muhimu kabisa ambao sote tunahitaji kuukuza, kwa hiyo, upo ule ambao unatuwezesha kuchangia kwenye mazungumzo ya maana na yainuayo. Kusudi la kitengo hiki na kinachofuata ni kuwasaidia kuhusu suala hili. Hapa mtahusika na jinsi ya kuinua kiwango cha mazungumzo kwa kurejea kwenye kanuni za kiroho, kadri fursa inavyojitokeza. Katika kitengo kinachofuata, mtafikiria juu ya jinsi ya kuanzisha na kudumisha mfululizo wa mazungumzo juu ya dhima fulani kama sehemu ya juhudi zenye mpangilio kujenga jumuiya hai katika kijiji chenu au ujirani.

Tutakachokifanya katika sehemu zinazofuata ni kuchunguza idadi fulani ya kauli juu ya mada tofauti ambazo, ingawa siyo mateuzi kamili, zote zimeegemezwa juu ya misingi ya mazungumzo na Nyaraka za 'Abdu'l-Bahá na hujumuisha vifungu vingi vya maneno Aliyotumia. Mnapaswa kusoma kila kauli mara kadhaa, kubaini mlolongo wa mawazo, na kwa zamu pamoja na wajumbe wengine wa kikundi chenu kuzisema kwa sauti hadi muweze kuzielezea kiasilia. Zoezi hili litawasaidia kuwaandaa kuongea kwa urahisi mtakapoona inafaa kuchota kwenye mafundisho ya Imani ili kuendeleza mjadala.

Mtaendelea katika kitengo hiki, bila shaka, kukariri vifungu kutoka Maandiko, kwa kuwa vina nguvu maalum ambayo hupenyeza kwenye moyo na nafsi ya binadamu, vikifumwa kwenye mazungumzo yenu, huwa na athari ya kina kwa msikilizaji. Walakini kunukuu kutoka kwenye Maandiko katika mazungumzo huhitaji hekima. Cha muhimu ni ukadirifu, mizania kati ya kunukuu moja kwa moja kutoka Maandiko na kutumia maneno yenu wenyewe kuelezea mafundisho ya Imani. Kufikia mizania hii, mtahitaji kuweka wakfu kiwango kikubwa cha muda na nguvu katika kusoma Maandiko na kuyaruhusu kubumba fikra zenu na hisia.

## SEHEMU YA 2

Kauli ya kwanza mnayoombwa kujifunza inahusu hitaji la Mwelimishaji wa binadamu.

> Tunapoufikiria uwepo, tunaona kuwa milki za madini, mimea, wanyama na wanadamu kila moja na zote, zinahitaji Mwelimishaji. Bustani inahitaji mtunza bustani. Ili kupata mavuno mengi, ardhi inahitaji mkulima. Kama mtu akiachwa peke yake mwituni, atachukua tabia za wanyama. Akielimishwa, anaweza kufikia vilele vya juu vya mafanikio. Kama wasingekuwepo waelimishaji, kusingekuwa na ustaarabu.
>
> Elimu ni ya aina tatu: ya kimwili, ya kibinadamu, na ya kiroho. Elimu ya kimwili inahusu maendeleo ya kimwili. Elimu ya kibinadamu inahusu ustaarabu na maendeleo. Inahusika na utawala, utaratibu wa kijamii, ustawi wa jamii ya binadamu, biashara na viwanda, sanaa na sayansi, vumbuzi muhimu, na shughuli kubwa. Elimu

ya kiroho inajumuisha upatikanaji wa ukamilifu mtakatifu. Hii ndiyo elimu ya kweli, kwa msaada wake, asili ya kiroho, asili ya juu zaidi, ya jamii ya binadamu inakuzwa.

Ili kuendelea, jamii ya binadamu inahitaji Mwelimishaji mwenye mamlaka dhahiri kama mwelimishaji wa kimwili, kibinadamu na kiroho. Kama yeyote angesema, "nimejaliwa na akili nyingi, na sihitaji Mwelimishaji kama huyo," atakuwa anakanusha kitu kilichowazi. Ni kama mtoto anaposema, "sihitaji elimu; nitafanya kulingana na fikra na akili yangu mwenyewe na nitafikia ubora kwa uwezo wangu mwenyewe."

Jamii ya binadamu kila mara imekuwa katika uhitaji wa huyu mwelimishaji mkamilifu, ambaye anaweza kuisaidia kupangilia masuala yanayohusu lishe na afya ya mwili, anayeweza kuihamasisha kujiendeleza katika ujuzi, uvumbuzi na ugunduzi, na, muhimu kabisa, anayeweza kuipulizia ndani yake maisha ya roho. Hakuna binadamu wa kawaida anayeweza kufanikisha kazi hizi ngumu sana. Ni Wadhihirishaji wa Mungu pekee wenye uwezo wa kuzikamilisha. Hizi ni Nafsi teule Ambazo zinatumwa na Mungu kipindi hadi kipindi kuwa Waelimishaji wa jamii ya binadamu ya ulimwengu.

1. Someni kauli mara kadhaa katika kikundi chenu na saidianeni mmoja kwa mwingine kujifunza maudhui yake vizuri. Mnapaswa kuulizana maswali kuhusiana na mawazo yaliyowasilishwa na kufanya mazoezi ya kuyaelezea kihalisia na kwa urahisi.

2. Halafu, jadilianeni katika kikundi chenu jinsi gani mawazo mliyojifunza kuyaelezea hapa yangeweza kuingizwa kwenye mazungumzo. Ni dhahiri kuwa hamtakurupuka ghafla na kuwaambia rafiki zenu kuwa elimu ni ya aina tatu. Kwahiyo, inastahili kufikiria aina ya maingiliano ambayo kwayo mawazo ya hapo juu yangethibitisha kuwa yakufaa. Pengine suala linalojadiliwa linahusu mmomonyoko wa maadili kwenye jamii au jinsi ya kufanya kazi kwa ajili ya uboreshaji wa ulimwengu. Tafakarini juu ya mazungumzo anuai ambamo kwayo mnajihusisha na marafiki, wajumbe wa familia, na jamaa. Miongoni mwa masuala yaliyomo akilini mwao, je, kuna yoyote ambayo yangewapeleka kwenye majadiliano kuzunguukia kwenye mawazo ya kauli hii?

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

3. Maswali aghalabu huibuka kwenye mazungumzo juu ya mada kama ile ambayo tumejifunza hivi punde. Ninyi mngejibu nini ikiwa mtu angewauliza: "Ni Akina Nani hawa baadhi ya Waelimishaji mnaowaongelea?"

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

4. Hapo chini yapo mateuzi machache kutoka Maandiko ya Bahá’u’lláh yanayohusu mahitaji ya jamii ya binadamu kwa ajili ya Mwelimishaji. Yatafakarini na kukariri angalau moja. Kwa njia hii, mnaweza kufuma vifungu kutoka Maandiko kwenye mazungumzo yenu pale inapofaa.

> **“Watu wote wameumbwa kuendeleza mbele ustaarabu uendeleao daima.”[1]**
>
> **“Kusudi la yule Mungu mmoja wa kweli, utukuzwe utukufu Wake, kwa kujifunua Yeye mwenyewe kwa watu ni kuweka wazi vile vito ambavyo vimefichika ndani ya chimbo la nafsi zao halisi na za ndani kabisa.”[2]**
>
> **“Kusudi la Mungu katika kutuma Mitume Wake kwa watu lina pande mbili. La kwanza ni kuwaondoa watoto wa watu kutoka katika giza la ujinga, na kuwaongoza kwenye mwangaza wa uelewa wa kweli. La pili ni kuhakikisha amani na utulivu wa jamii ya watu, na kuwapatia wote njia ambayo kwayo vinaweza kustawishwa.”[3]**
>
> **“Watu wakati wote wapo katika uhitaji wa Yule wa kuwausia, kuwaongoza na kuwaelekeza na kuwafunza.”[4]**

## SEHEMU YA 3

Aya zifuatazo zinaelezea jinsi Mungu anavyoweza kujulikana kupitia Wadhihirishaji Wake pekee na zitakuwa za msaada kwenu mnapozungumza na marafiki:

> Fikiria ulimwengu usiokuwa na mwisho. Je, ingewezekana kuwa ungeumbwa bila Muumbaji? Au kwamba uhalisia wa Muumba ungeweza kufahamika daima na wale ambao Yeye aliwaumba? Kama tukiutazama muumbo mzima, tutaona kuwa chochote ambacho kipo chini zaidi, hakina uwezo wa kufahamu uwezo wa kile ambacho kipo juu zaidi. Hivyo jiwe na mti, hata viendelee namna gani, kamwe haviwezi kutambua uwezo wa uoni na usikivu. Mnyama kamwe hawezi kufahamu uhalisia wa binadamu na kutambua uwezo wa roho ya binadamu. Kwa hiyo tutawezaje, sisi tulioumbwa kuelewa uhalisia wa Muumba wetu?
>
> Ingawa uelewa wetu kamwe hauwezi kumfikia Mungu, hatujanyimwa kumjua Yeye. Kutoka kipindi hadi kipindi Kiumbe maalum hujitokeza duniani ambaye ni Mdhihirishaji wa Mungu. Ukamilifu wote, fadhila, na uangavu ambavyo ni vya Mungu vinaonekana kwa hawa Wadhihirishaji Watakatifu, kama mionzi ya jua inayoonekana katika kioo kisafi, na kilichong’arishwa. Kusema kuwa kioo kinaakisi jua haina maana ya kusema kuwa jua limeshuka kutoka vilele vyake na kujumuika katika kioo. Vilevile, Mungu hateremki kutoka mbingu ya utakatifu kuja kwenye sura hii ya uwepo. Kinachomaanishwa ni hiki: vyote ambavyo jamii ya binadamu hujua, hujifunza, na, huelewa juu ya majina na sifa na ukamilifu wa Mungu hurejea kwa Wadhihirishaji Wake Watakatifu.

1. Baada ya kusoma kauli hii mara kadhaa katika kikundi chenu na kujibu maswali mtakayoulizana juu ya maudhui yake, mnapaswa kufanya mazoezi ya kutamka mawazo kwa kiwango cha urahisi.

2. Sasa jadilini kwenye kikundi chenu namna ambavyo mngepaswa kuingiza kwenye mazungumzo kiasilia mawazo mliyojifunza hapa. Hili lingetekelezwa kirahisi, kwa mfano, katika mjadala juu ya uwepo wa Mungu au kusudi la maisha. Ni zipi baadhi ya mada nyingine na maswali yanayoibuliwa kwenye mazungumzo miongoni mwa familia yako na marafiki zako ambazo zingewapa uwezekano wa kushirikiana mawazo haya?

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

3. Hebu tuchukulie kuwa, kwenye mazungumzo na rafiki zenu, mnapata fursa ya kutambulisha mawazo ambayo mmejifunza hivi punde. Mngejibu namna gani kama mmoja wao angewauliza swali lifuatalo: "Ni yapi baadhi ya mambo mnayoyajua kuhusu Mungu kupitia Wadhihirishaji Wake?"

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

4. Mngependa kukariri moja au zaidi ya vifungu vifuatavyo kutoka kwenye Maandiko ya Bahá'u'lláh ili muweza kuvinukuu wakati mnazungumza na marafiki juu ya mada hii:

**"Elimu ya Yeye, Ambaye ni Asili ya vitu vyote, na kumfikia Yeye, haviwezekani isipokuwa kwa elimu ya, na kuzifikia, Nafsi hizi angavu zitokazo kwenye Jua la Ukweli."**[5]

**"Nafsi ya Mdhihirishaji daima imekuwa mwakilishi na msemaji wa Mungu. Yeye, kwa kweli, ni Mapambazuko ya Majina bora kabisa ya Mungu, na Mahali pa Mapambazuko ya Sifa Zake zilizo tukuka."**[6]

**"Muwe mliyohakikishiwa, tena kwamba kazi na vitendo vya yeyote na kila mmoja wa hawa Wadhihirishaji wa Mungu, hivyo chochote kuhusianacho nao, na yoyote ambayo wangeweza kuyadhihirisha katika siku zijazo, yote yameamriwa na Mungu na ni uakisi wa Mapenzi na Kusudi Lake."**[7]

## SEHEMU YA 4

Umoja wa dini ni mada inayowavutia wengi, na mawazo yafuatayo yatawasaidia katika matukio mbalimbali:

> Lazima tuwe wapenzi wa mwangaza haijalishi umeonekana kutoka taa gani. Lazima tuwe wapenzi wa waridi haijalishi linachanua kutoka bustani gani. Lazima tuwe

watafutaji wa ukweli haijalishi unatoka kwenye chanzo gani. Ung'ang'anivu kwa taa moja unaweza kutuzuia kuthamini mwangaza pale unapong'aa katika taa nyingine. Katika kutafuta ukweli, lazima tuondokane na dhana tulizozijenga tangu awali na kuachana na chuki zetu. Kama kikombe chetu kimejaa ubinafsi, hakuna nafasi ndani yake kwa ajili ya maji ya uzima.

Dini ni mwangaza wa ulimwengu. Inaongoza hatua zetu na kutufungulia milango ya furaha isiyo na kikomo. Tunapochunguza mafundisho ya dini zote kuu, huru kutokana na vizuizi vya mafundisho ya kiitikadi na uigaji kwa upofu, tunakuja kutambua kuwa zimeegemezwa juu ya msingi ule ule. Zote hufunua elimu ya Mungu. Zinatafuta maendeleo ya ulimwengu wa jamii ya binadamu.

Bila shaka, zipo tofauti miongoni mwa sheria za kijamii na kanuni zinazofundishwa na kila dini kulingana na mahitaji ya wakati na mahali. Lakini katika kiini chao dini zote ni moja. Zinalea imani, elimu, yakini, haki, ucha Mungu, wenye nia ya juu, usadikifu, upendo wa Mungu, na hisani. Zina fundisha utakaso, kujitenga, unyenyekevu, ustahimilivu, subira, na uthabiti. Njema hizi za kibinadamu huhuishwa katika kila Maongozi.

Inasikitisha kuwa, kwa sababu ya chuki na kuiga kwa upofu, wengi hawawezi kuona msingi wa umoja wa dini. Mwongozo wa Mungu kwa jamii ya binadamu ni ukweli, na ukweli haugawanyiki; Ni mmoja. Kama tukiuchunguza ukweli kwa uhuru, tukiweka kando dhana zetu tulizoamini tangu awali, utafutaji wetu utatuongoza kwenye umoja. Dini inapaswa kutuunganisha; lazima iimarishe mafundo ya upendo miongoni mwa watu. Kama itakuwa chanzo cha uadui na ugomvi, kutokuwepo kwake ni bora zaidi.

1. Kama ilivyo katika sehemu iliyotangulia, mnapaswa kusoma kauli hii mara kadhaa katika kikundi chenu, ulizaneni maswali kuhusiana na mawazo, na mfanye mazoezi ya kuyaelezea vizuri.

2. Fikirieni katika kikundi chenu namna mtakavyoweza kuuendea ufumaji wa mawazo mliojifunza kwenye mazungumzo, tuseme, kuhusu ugomvi wa kidini, ambao aghalabu umo akilini mwa watu. Lakini pia mngeweza kujikuta mwenyewe miongoni mwa marafiki kadhaa wakijadiliana juu ya umuhimu wa utafutaji ukweli na wasio shawishiwa kwa propaganda. Rudieni kufikiria tena mazungumzo yenu ya hivi karibuni pamoja na marafiki na majirani, wafanyakazi wenza na jamaa. Ni yapi baadhi ya masuala akilini mwao ambayo yangenufaisha mjadala kuzunguukia mawazo haya?

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

3. Mngejibu jinsi gani ikiwa, baada ya kushirikiana mawazo yaliyopo hapo juu kwenye mazungumzo, kama mtu angewauliza, “Ni zipi baadhi ya kweli zilizomo katika dini zote?”

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

4. Inapendekezwa kwamba mkariri kimoja au viwili kati ya vifungu vifuatavyo kutoka Maandiko ya Bahá’u’lláh:

**“Hakuna shaka yoyote kwamba watu wa ulimwengu, wa usuli wowote au dini, hupata upuuzio wao kutoka Chanzo kimoja cha mbinguni, na ni raia wa Mungu mmoja.”**[8]

**“Andamaneni na wafuasi wa dini zote katika moyo wa urafiki na upatano.”**[9]

**“Kusudi la kimsingi linalohuisha Imani ya Mungu na Dini Yake ni kulinda maslahi na kuleta umoja wa mbari ya wanadamu . . .”**[10]

**“Dini ya Mungu ni kwa ajili ya upendo na umoja; msiifanye kuwa chanzo cha uadui au mafarakano.”**[11]

## SEHEMU YA 5

Uhusiano kati ya sayansi na dini ni mada inayofuata ambayo mnaombwa kujifunza.

Dini lazima ikubaliane na sayansi. Mungu ametujalia uwezo wa kufikiri kimantiki ili tuweze kutambua kile ambacho ni kweli. Sayansi na dini vyote vinatarajiwa kukidhi viwango vya kufikiri kimantiki. Kwa hiyo, zinapaswa kuwa na makubaliano moja kwa nyingine. Sayansi na dini ni mabawa mawili ambayo juu yake akili ya binadamu inaweza kuruka na kufikia vilele virefu, mabawa mawili ambayo kwayo jamii ya binadamu inaweza kuruka. Bawa moja halitoshi.

Sayansi ni majaaliwa ya Mungu. Hugundua sheria za ulimwengu wa kimwili na kutuwezesha kushinda vizuizi ambavyo asili imeweka juu yetu. Kwa msaada wa vifaa vya kisayansi, tunaona vitu visivyoonekana kwa macho ya kawaida na kuwasiliana hadi masafa marefu katika sekunde chache. Sayansi huunganisha wakati wa sasa na uliopita na hupenyeza katika siri za siku zijazo. Maendeleo ya watu yanategemea juu ya mafanikio ya kisayansi.

Dini ya Mungu ni mwendelezaji wa ukweli, mhimili wa ujuzi, na mstaarabishaji wa mbari ya watu. Bila dini, sayansi inakuwa chombo cha kuendeleza tabia ya kuchukulia kuwa umiliki wa vitu vya kimwili na anasa za dunia kuwa muhimu zaidi kuliko tunu za kiroho, hatimaye hupelekea kwenye ukataji tamaa. Pale dini inapokuwa kinyume na sayansi, inakuwa ushirikina mtupu. Kama dini na sayansi

vikitembea pamoja kwa upatano, sehemu kubwa ya chuki na uchungu ambavyo kwa sasa vinaleta taabu kwa jamii ya binadamu vitafikia mwisho.

1. Kama kawaida, someni kauli hiyo mara kadhaa katika kikundi chenu, aya hadi aya, na ulizaneni kati yenu maswali mpaka mmejifunza maudhui vizuri kiasi kwamba mnaweza kuyaelezea kiasilia.

2. Mngemjibu namna gani mtu aliyesema yafuatayo: "Dini ni kitu kiilichopitwa na wakati; sayansi itatatua matatizo yote ya jamii ya binadamu." Je, itakuwa ya msaada kwenu kufafanua kwamba dini siyo sawa na ushirikina, lakini inakuwa hivyo bila sayansi, na kwamba sayansi bila dini hupelekea kwenye ukataji tamaa unaotokana na tabia ya kuchukulia kuwa umiliki wa vitu vya kimwili na anasa za dunia kuwa muhimu zaidi kuliko tunu za kiroho? Je, mngeweza kutoa mifano ya jinsi hali hii hutokea?

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

3. Inapendekezwa kuwa mkariri moja au zaidi ya vifungu vifuatavyo kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh:

**"Ya kwanza na ya muhimu kabisa miongoni mwa fadhila hizi, ambazo Mwenyezi amejalia juu ya mwanadamu, ni zawadi ya kuelewa. . . . Zawadi hii inampa mtu uwezo wa kubaini ukweli katika vitu vyote, humwongoza kwa kile ambacho ni sahihi, na humsaidia kugundua siri za muumbo."**[12]

**"Tazama ulimwengu na uufikirie kwa muda kidogo. Hufunua kitabu chake chenyewe mbele ya macho yako na kudhihirisha kile ambacho Kalamu ya Bwana wako, Mfanyiza, Mjuwa yote, imeandika humo."**[13]

**"Elimu ni kama mabawa katika maisha ya mtu, na ngazi yake ya kupandia. Upatikanaji wake ni wajibu wa kila mmoja."**[14]

## SEHEMU YA 6

Umoja wa wanadamu ni mada inayodunda katika mioyo ya watu kila mahali leo, na wengi watatoa fursa ya kujadiliana na ninyi mawazo yaliyowasilishwa hapo chini.

Bustani ambamo maua ya rangi mbalimbali na manukato hukua upande huu na ule huvutia machoni. Na ingawa ni tofauti, kila ua linastawishwa na mvua ile ile na hupokea joto la jua moja. Hili pia ni kweli kwa jamii ya binadamu. Imeundwa na mbari nyingi na rangi. Lakini wote hutoka kwa Mungu yule yule, na wote wana chimbuko lile lile. Utofauti katika familia ya binadamu unapaswa kuwa chanzo cha

upatano, kama ilivyo katika muziki ambapo nota tofauti zinaunganika pamoja kufanya muziki kamili.

Umoja ni muhimu kwa uwepo. Upendo ni chanzo hasa cha uhai. Katika ulimwengu wa kimwili, vipengele vya vitu vyote vinashikiliwa pamoja kwa sheria ya mvutano. Sheria ya mvutano huvileta pamoja baadhi ya vipengele katika umbo la ua zuri. Lakini pale ambapo mvutano unapoondolewa, ua huoza na hukoma kuwepo. Ndivyo ilivyo kwa jamii ya binadmu. Mvuto, upatano, na umoja ni nguvu zinazoshikilia pamoja jamii ya binadamu.

Bahá'u'lláh amechora mchoro kwa ajili ya kuunganisha watu wote wa ulimwengu. Tunapaswa kufanya kila juhudi kuwavutia kwenye duara hili la umoja. Tunapokutana na watu wa mbari, mataifa, dini, na maoni tofauti kuliko yetu wenyewe, hatupaswi kuruhusu tofauti hizi kuwa vizuizi kati yetu. Tunapaswa tuwafikirie kama mawaridi yenye rangi tofauti yanayostawi katika bustani nzuri ya jamii ya binadamu na kufurahia kuwa miongoni mwao.

1. Baada ya kujifunza kauli iliyopo hapo juu kama mlivyofanya sehemu zilizopita, fikirieni mazungumzo mengi yanayoendelea kukunjuka kuwazunguukia. Ni yapi baadhi ya masuala katika akili za watu ambayo yangeleta uwezekano kwa ajili yenu kushirikiana nao mawazo haya?

____________________

____________________

____________________

____________________

2. Mazungumzo juu ya umoja wa wanadamu yanaweza kupelekea kwenye majadiliano kuhusu umuhimu wa umoja katika jumuiya yenu wenyewe. Mnaweza kusema maneno machache kuhusu jinsi gani kila mmoja wetu angeweza kuchangia kwenye hili?

____________________

____________________

____________________

3. Pengine mngependa kukariri moja au zaidi ya mateuzi yafuatayo ili muweze kurejea kwayo mtakapokuwa mnaongelea mada hii na marafiki zenu:

**"Hema la umoja limeinuliwa; msiangaliane kama wageni. Ninyi ni matunda ya mti mmoja, na majani ya tawi moja."[15]**

**"Ni wenye nguvu mno mwanga wa umoja kwamba unaweza kuangazia dunia nzima."[16]**

**"Elekezeni nyuso zenu kwenye umoja, na acheni wangavu wa mwangaza wake ung'ae juu yenu. Kusanyikeni pamoja, na kwa ajili ya Mungu suluhisheni kuondoa chochote kile ambacho ni chanzo cha ugomvi miongoni mwenu."[17]**

**"Imempasa mtu kushikilia imara kwenye kile ambacho kitaendeleza upatano, wema na umoja."[18]**

## SEHEMU YA7

Kauli ifuatayo itawasaidia kuchangia kwenye majadiliano juu ya mada ya haki, suala lenye umuhimu mkubwa kwa watu wengi zaidi:

> Utofauti wa uwezo kati ya watu binafsi ni wa msingi kwa uwepo wa binadamu. Kwa hiyo, haiwezekani kwa watu wote kuwa sawa katika kila hali. Walakini masuala ya kibinadamu, katika ujumla wake, yanapaswa kuongozwa na kanuni ya haki. Haki lazima iwe takatifu, na haki za kila mtu lazima zilindwe.
>
> Haki haina mipaka; ni sifa ya ulimwengu. Lazima ifanye kazi katika idara zote za maisha ya binadamu. Kila mmoja na wajumbe wote wa jamii wanapaswa kufurahia manufaa ya ustaarabu, kwa sababu sote ni sehemu ya chombo cha jamii ya binadamu. Kama mjumbe moja wa chombo hiki yupo katika uchungu au mfadhaiko, wajumbe wengine wote hawanabudi kuteseka. Inawezekanaje mmoja kuteseka na wengine wakakaa kwa starehe? Jamii ya leo inakosa usaidizi wa pamoja na msaada unaohitajika na ulinganifu; haijapangiliwa vizuri. Sheria na kanuni zinahitajika zitakazo hakikisha ustawi na furaha ya familia nzima ya binadamu.
>
> Haki imeegemezwa juu ya nguzo za thawabu na adhabu. Serikali zinazotawaliwa na wale wasiyokuwa na imani, wasiyo na hofu ya adhabu ya Mungu, zitatumia sheria zisizo na haki. Matumaini kwa ajili ya thawabu na hofu ya adhabu vyote vinahitajika kama dhuluma inatakiwa kuzuiliwa. Watunga sheria na watawala wa sheria lazima watambue matokeo ya kiroho ya maamuzi yao. Watawala wanaoamini kwamba athari za matendo yao zitawafuata zaidi ya maisha ya ulimwengu huu na wanaojua kwamba maamuzi yao yatapimwa katika mizania ya haki Takatifu kwa hakika watajiepusha na udhalimu na dhuluma.

1. Mara mtakapojifunza kuelezea mawazo ya hapo juu kiasilia, fikirieni mada zipi za mazungumzo zingeweza kunufaika kutoka kwenye umaizi utolewao na kauli hizi.

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

2. Mtamjibuje mtu ambaye anaamini kuwa utovu wa haki hautaisha kamwe?

________________________________________

________________________________________

________________________________________

3. Hapo chini ni mateuzi kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh yanayohusu haki ambayo mnahimizwa kuyakariri.

> **"Mwangaza wa watu ni Haki. Usiuzime kwa pepo tofauti za ukandamizaji na udhalimu. Kusudi la haki ni utokeaji wa umoja miongoni mwa watu."**[19]

> **"Hakuna nuru inayoweza kulinganishwa na ile ya haki. Utaratibu wa ulimwengu na utulivu wa mwanadamu hutegemea juu yake."**[20]

> **"Kile ambacho hufunza ulimwengu ni Haki, kwa kuwa imeshikiliwa na nguzo mbili, thawabu na adhabu. Nguzo hizi mbili ni vyanzo vya uhai kwa ulimwengu."**[21]

## SEHEMU YA 8

Pengo kati ya matajiri na maskini linazidi kupanuka kila kukicha, na kauli iliyopo hapo chini itawasaidia kwenye kuzungumza na marafiki juu ya hili na mada zinazohusiana.

> Leo, kwa sababu ya ukosefu wa usaidizi wa mmoja kwa mwingine na mahusiano yenye upatano, baadhi ya wajumbe wa jamii wanaridhika, wanaishi katika starehe kubwa na anasa, wakati wengine wanahitaji chakula na malazi. Baadhi ni matajiri kupindukia, na wengine wanaishi katika umaskini wa kutisha kabisa.
>
> Sheria za jamii lazima zitungwe na kufuatwa kwa namna ambayo haitawaruhusu wachache kulimbikiza utajiri wa kupindukia na wengine kubaki katika umaskini kabisa. Hii haina maana ya kusema kuwa lazima sote tuwe sawa, kwa kuwa tofauti katika kiwango na uwezo ni jambo la kiasili katika muumbo. Lakini wingi wa mali uliopindukia vyakusikitisha ulioambatana na umaskini uliokithiri vinaweza kutokomezwa. Ikiwa ni sahihi kwa bepari kumiliki hazina kubwa, vilevile ni sawa kwa mfanyakazi kuwa na nyenzo za kutosha kwa ajili ya kuishi. Pale tunapouona umaskini uliokithiri, basi mahali fulani lazima tutakuta dhuluma.
>
> Kiini cha suala hili ni kwamba haki Takatifu lazima idhihirike katika hali za kibinadamu. Misingi ya mfumo nzima wa kiuchumi ni mitakatifu kiasili na inahusiano na ulimwengu wa moyo na roho. Matajiri lazima watoe kutoka utajiri wao; lazima walainishe mioyo yao na kukuza akili yenye huruma. Mioyo lazima iwe imeunganishwa pamoja zaidi, upendo lazima utawale kwa kiasi kikubwa kiasi kwamba matajiri kwa hiari kabisa watachukua hatua ya kustawisha marekebisho ya kudumu ya kiuchumi. Wenyewe lazima watambue kuwa siyo haki wala halali kuwa wao waweze kumiliki utajiri mkubwa ambapo upo umaskini wa kukithiri katika jumuiya. Kwa njia hii, watatoa utajiri wao kwa hiari, na kubakiza kiasi cha kutosha cha kuwawezesha kuishi kwa raha.

1. Someni tena kauli na mjifunze kwenye kikundi chenu kama ilivyozoeleka. Yapo masuala mengi katika akili za watu yanayohusu utajiri na umaskini — ajira, ujira, makazi kutaja tu machache. Je, mnaweza kufikiria mada zingine za mjadala ambao kwayo ungenufaika kutoka mawazo ya kwenye kauli hii?

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

2. Mngejibu nini kama mtu aliyekusikia ukitaja mawazo yaliyopo hapo juu akikuuliza yafuatayo: "Mnasema kuwa matajiri watakuja kuelewa na kuunga mkono sheria za kodi zinazowabana, na kwa hiari watalipa kile wanachopaswa? Nini kinachowafanya mfikiri kuwa hili linawezekana?"

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

3. Inapendekezwa kuwa mkariri moja au mawili kati ya mateuzi haya kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh:

> **". . . lazima mzae matunda mema na ya ajabu, ili ninyi wenyewe na wengine mpate kunufaika nayo. Hivyo inampasa kila mmoja kujishughulisha katika ufundi na kazi mbalimbali, kwani ndimo ilimo siri ya mali, Enyi watu wa ufahamu!"[22]**

> **"Ikiwa macho yako yataelekezwa kuelekea huruma, achilia mbali vitu vinavyo kunufaisha na ushikilie kile kitakachonufaisha jamii ya binadamu. Na ikiwa macho yako yatageuziwa kwenye haki mchagulie jirani yako kile ambacho hujichagulia mwenyewe."[23]**

> **"Amebarikiwa yule ampendeleaye nduguye kabla yake mwenyewe."[24]**

> **"Hakuna kitendo kizuri ambacho kimewahi au ambacho daima kitapotea, kwa kuwa vitendo vizuri ni hazina zilizohifadhiwa na Mungu kwa manufaa ya wale wanao tenda."[25]**

> **". . . jihadharini msije kupita mipaka ya kiasi, na kuhesabiwa miongoni mwa wabadhirifu."[26]**

## SEHEMU YA 9

Hapo chini yapo baadhi ya mawazo ambayo yatawasaidia kushiriki kwenye mjadala kuhusu mada ya ubaguzi.

> Ubaguzi katika kila hali zake zote — kidini, kimbari, kijinsi, kikabila, kiuchumi — huharibu mfumo wa jamii ya binadamu na ni kinyume cha amri za Mungu. Kwa maelfu ya miaka, jamii ya binadamu imeteseka kutokana na vita na umwagaji wa damu ambavyo vimesukumwa na moja au nyingine ya ubaguzi huu. Kadri vitakavyoendelea, ndivyo jamii ya binadamu haitaweza kupumzika.

Mungu ametuma Mitume Wake kwa ajili ya kusudi moja tu la kujenga upendo na umoja. Vitabu vyote vya mbinguni ni neno lililoandikwa la upendo. Kama wakithibitisha kuwa chanzo cha utengano, wanakuwa wasio zaa matunda. Kwa hiyo, ubaguzi wa kidini, haswa unapingana na mapenzi na amri ya Mungu.

Ubaguzi wa utaifa, hauhalalishwi kwa vyovyote vile. Dunia ni ardhi moja, nchi moja. Mistari na mipaka inayotenganisha mataifa ni ya kufikirika; haikuumbwa na Mungu. Watu ndio hutangaza mto kuwa alama ya mpaka kati ya nchi mbili, na wakiupa kila upande jina lake, ambapo mto uliumbwa kwa ajili ya pande zote mbili na ni njia ya asili kwa pande zote. Je, sio udhanifu na ujinga wao ambavyo vimewalazimisha watu kugeuza fadhila za maisha kuwa sababu ya vita na maangamizi?

Ubaguzi wa kimbari si kingine bali ushirikina. Rangi ya ngozi ya mtu ni matokeo tu ya jinsi mababu zake walivyoweza kukabiliana na hali ya hewa na mazingira kadri wakati ulivyopita. Tabia ndiyo kigezo cha kweli cha jamii ya binadamu. Ubora hautegemei juu ya mbari na rangi. Imani, usafi wa moyo, matendo mema na kauli inayostahili sifa ndivyo vinavyokubalika kwenye kizingiti cha Mungu.

Kwa muda mrefu sana, wanawake wamechukuliwa kuwa ni duni kuliko wanaume na kudhulumiwa. Utofauti kati ya mwanaume na mwanamke ni hitaji la ulimwengu wa kimwili; katika ulimwengu wa kiroho, wako sawa. Katika makadirio ya Mungu, hakuna tofauti kati ya wanaume na wanawake. Jamii nzima ya binadamu imejaliwa na Yeye akili na uelewa. Wote wanao uwezo wa kukuza njema. Hakuna mazingira yoyote wakati wa sasa ambamo jinsia ya mtu hutoa misingi ya kufanya ubaguzi.

Kufuatana na maneno ya Agano la Kale, Mungu amesema, "Na tumfanye mtu kwa mfano na sura yetu." Kiudhahili hili huwahusu wanawake vile vile. Mwanadamu ameumbwa katika sura ya Mungu; hii ndiyo kusema, njema takatifu zinaakisiwa na kufunuliwa katika uhalisia wa binadamu. Huu ni ukweli kuhusu jamii nzima ya binadamu. Inawezekanaje kudai hata kidogo kuwa wale wenye rangi moja tu, kabila au utaifa ndiyo wameumbwa katika mfano wa Mungu. Ni upuuzi ulioje kusema kuwa matajiri peke yao ndiyo wameumbwa katika mfano Wake au kufikiria kuwa kigezo kwa ajili ya ukaribu na Mungu ni kuwa na daraja la juu katika jamii. Jamii ya binadamu haiwezi kufikia uangazio isipokuwa kupitia kuachana na ubaguzi na kupata maadili ya Ufalme.

1. Jifunze kauli hii kama ulivyofanya kwa zile zilizotangulia, halafu fikiria baadhi ya changamoto ambazo marafiki zako na majirani wameziibua katika mazungumzo yanayoongelea utokomezaji wa ubaguzi.

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

2. Wewe ungejibuje kama mtu aliyekusikia ukiongelea mawazo yaliyopo hapo juu angekuuliza: "Je, sisi tunaweza kuwa wenye ubaguzi na tusijue kuwa tunao?"

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

3. Pengine utapata fursa ya kujumuisha katika majadiliano yako juu ya mawazo haya, moja au nyingine ya mateuzi yafuatayo kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh:

**"Dunia ni nchi moja, na binadamu ni raia wake."[27]**

**"Miche yote ya ulimwengu imetokea kutoka Mti moja, na matone yote kutoka Bahari kuu moja, na viumbe vyote wanategemea uwepo wao kutoka kwa Uwepo Mmoja."[28]**

**"Kwamba ni mtu yule, kwa siku ya leo, amejifunga kuihudumia mbari ya binadamu."[29]**

**"Mwanga wa tabia njema hupita mwanga wa jua na nuru iliyomo ndani yake."[30]**

**"Utofauti wa mtu haumo katika mapambo au utajiri, lakini katika tabia njema na uelewa wa kweli."[31]**

**"Mungu akujalie kuwa uweze kusaidiwa kwa neema katika hali zote kuvunja masanamu ya ushirikina na kupasulia mbali tando za dhana za watu."[32]**

**"Mzembe kabisa kati ya watu wote ni Yule ambaye hubishana bure na kutafuta kujikweza mbele ya ndugu yake."[33]**

## SEHEMU YA 10

Wakati ukizungumza pamoja na marafiki, aghalabu utakuwa na uwezo wa kuchota mawazo yaliyomo katika kauli ifuatayo kuhusu usawa wa wanaume na wanawake:

> Jua la kimwili, kupitia mwangaza wake na joto, hufunua uhalisia wa vitu vyote juu ya dunia. Tunda lililojificha katika mti huonekana juu ya matawi yake katika kuitikia nguvu ya jua. Vilevile, Jua la Ukweli, liking'aa katika uzuri wake wote katika anga la kiroho, huleta katika mwangaza uhalisia ambao haukua dhahiri zamani. Ndiyo maana, katika zama hizi, kanuni ya usawa wa wanaume na wanawake imetambuliwa kikamilifu na sasa imestawishwa.
>
> Bahá'u'lláh amesema katika istilahi za uwazi kabisa kuwa katika uoni wa Mungu hakuna tofauti kati ya wanaume na wanawake. Hali ya ukosefu wa usawa ambayo imekuwepo kupitia zama nyingi siyo matokeo ya ubora wa wanaume; ni kwamba wanawake hawajapewa fursa zilezile za kukuza uwezo wao. Licha ya ubaguzi dhidi yao, hata hivyo, historia imeweka kumbukumbu ya maisha ya wanawake lukuki ambao wamefanikiwa kufanya mambo makubwa.

Mojawapo wa wanawake kama hao alikuwa Mshairi wa Kiajemi, Ṭáhirih. Yeye alizaliwa katika miaka ya mwanzo ya 1800 katika nchi ambamo wanawake walikuwa wametawaliwa kabisa na wanaume. Alikuwa mwanamke wa kwanza kukubali ukweli wa Ufunuo mpya wa Mungu. Kadri alivyoshuhudia alfajiri ya Siku mpya, aliendelea kupata uhakika kuwa wakati ulikuwa umewadia kwa ajili ya uhalisia wa usawa wa wanaume na wanawake kutambulika. Alitumia nguvu zake kutangaza ukweli huu. Ujuzi wake na ufasaha viliwakanganya wanaume wengi wasomi wa wakati wake. Ingawa majeshi yote ya mfalme dhalimu na makuhani wajinga na wenye kiburi waliinuka dhidi yake, hata kwa nukta moja hakusita kusema ukweli. Na mwishowe, alitoa maisha yake kwa ajili ya Hoja ambayo alikuwa ameikumbatia kwa uthabiti kabisa.

Kuamini katika kile ambacho Mungu hakukusudia ni ujinga na ushirikina. Leo wanawake sharti wapewe kila fursa ya kupata elimu na kushika daraja la usawa pamoja na wanaume katika nyanja zote za jitihada za binadamu. Maendeleo ya kweli ya jamii ya binadamu hayatawezekana, hadi usawa wa wanaume na wanawake utakapokuwa halisi katika ulimwengu huu, kama ulivyo katika milki za kiroho,

1. Kama siku zote mnapaswa kusoma kauli hii katika kikundi chenu na fanyeni mazoezi ya kusema mawazo haya. Je, yapo mazungumzo yoyote ambayo wewe na marafiki zako hivi karibuni mmenufaika kutoka umaizi uliyomo humo? Masuala yapi yaliongelewa katika majadiliano?

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

2. Ni zipi baadhi ya itikadi na mielekeo inayoshamiri katika jamii ya leo ambayo itapaswa kubadiliishwa kama wanawake wanatakiwa kuchukua nafasi sawa na wanaume katika nyanja zote za jitihada?

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

3. Hapa chini yapo mateuzi machache kutoka katika Maandiko ya Bahá'u'lláh ambayo pengine ungependa kukariri:

**"Wanawake na wanaume wamekuwa na wataendelea kuwa sawa katika macho ya Mungu."**[34]

**"Hamjui kwa nini tuliwaumba ninyi nyote kutokana na mavumbi yale yale? Ili asiwepo yeyote wa kujitukuza juu ya mwingine."**[35]

**"Katika Siku hii Mkono wa neema tukufu umeondoa tofauti zote. Watumishi wa Mungu na vijakazi Wake wanahesabika kuwa katika kiwango kimoja."**[36]

## SEHEMU YA 11

Kauli ya mwisho unayoombwa kujifunza ipo kwenye somo la elimu kwa wote:

Uendelezaji wa elimu ni hitaji la haraka kabisa la wakati wetu. Hakuna taifa ambalo linaweza kufanikisha ustawi isipokuwa kama litaifanya elimu kuwa moja ya jambo lake la msingi. Sababu ya msingi ya mmomonyoko wa watu ni ukosefu wa kupata ujuzi.

Elimu lazima ianze utotoni. Ni jukumu la baba na mama kufanya kila wanaloweza kuwaelimisha watoto wao, kuboresha tabia zao kufuatana na sheria za kiroho na za kimaadili, na kuhakikisha kuwa wao wamefunzwa katika mafunzo ya sanaa na sayansi. Akina mama ni waelimishaji wa kwanza wa jamii ya binadamu; huwalea watoto wao kwenye kifua cha ujuzi. Kila mtoto lazima aelimishwe; hili siyo jambo linaloweza kupuuziwa. Kama wazazi wanaweza kukabiliana na gharama za lazima zinazohitajika, wao lazima wafanye hivyo. La sivyo jumuiya lazima itoe njia kwa ajili ya elimu ya mtoto.

Elimu sharti ikuze katika kila mwanadamu shauku ya kufanikisha ubora. Tunapaswa kuupenda ukamilifu wa kibinadamu na kuufuata kwa hamu. Tunatakiwa kutamani kuwa na utofauti wa kiroho, kujulikana kwa ajili ya sifa za ulimwengu wa kibinadamu — kwa ukweli, utiifu, huduma kwa jamii ya wanadamu, upendo na haki. Tutafute kujulikana kwa juhudi zetu za kuendeleza amani na umoja na kulea ujifunzaji. Kuwaongoza watu katika njia kama hii ni kazi halisi ya elimu.

1. Baada ya kusoma kauli hii katika kikundi chako, jaribu kubaini baadhi ya fikra walizonazo marafiki zako juu ya elimu. Mawazo yaliyopo hapo juu yanashughulikiaje fikra zao?

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

2. Inapendekezwa kwamba ukariri moja au zaidi ya mateuzi yafuatayo kutoka katika Maandiko ya Bahá’u’lláh:

**“Haifai kwamba mtu aachwe bila elimu au ustadi, kwani yeye basi amekuwa mti tasa tu.”**[37]

**“Elekezeni akili zenu na nia kwenye uelimishaji wa watu na jamaa wa dunia . . .”**[38]

**“Sanaa, kazi za ufundi na sayansi huinua ulimwengu wa uhai, na huelekea kuleta adhama yake.”**[39]

**“Kwa kweli, elimu ni hazina ya kweli kwa mtu, na chanzo cha utukufu, cha baraka, cha furaha, cha adhama, cha uchangamfu na shangwe kwake.”**[40]

## SEHEMU YA 12

Amani ni moja ya masuala yaliyomo katika akili ya kila mtu. Ustawishaji wake unatakiwa kwa haraka sana na ni muhimu. Sasa kwa kuwa umefikiria kidogo juu ya kanuni hii iliyoandikwa katika kauli zilizotangulia, utaona kuwa itakusaidia kutafakari juu suala la amani ya ulimwengu.

Mengi yanategemea, bila shaka, juu ya serikali kuchukua hatua zinazofaa kutokomeza vita. Makubaliano ya kisiasa kwa ajili ya kumaliza mafarakano na kupunguza silaha ni lazima katika kutafuta amani, kama ilivyo miundo lukuki ya ushirikiano wa kimataifa miongoni mwa mataifa. Bado, haidhuru zina umuhimu kiasi gani mbinu hizi, zenyewe hazitaweza kupelekea kwenye amani ya kudumu ikiwa kanuni zilizoongelewa hapo awali hazitastawishwa kila mahali ulimwenguni. Sharti tujiulize wenyewe, je, watu wasipojifunza kuchunguza uhalisia na kutambua kuwa ukweli ni mmoja, uadui wa tangu zamani hautaendelea kudumu? Sote tunatoka kwenye chimbuko moja. Mungu anatuangalia na hutufunza sote kupitia Wadhihirishaji Wake. Mafundisho Yao yamewekwa juu ya msingi uleule wa upendo na udugu. Ni pale tu ambapo umoja wa dini utakapothaminiwa, ndipo ugomvi wa kidini utakapokwisha na mwangaza wa dini utaangaza njia kuelekea amani. Sharti tuendelee kujiuliza, kwani siyo lazima kwa sayansi na dini kufanya kazi kwa upatano, kuondoa mawingu ya ujinga na kuonesha uwongo wa kila aina ya ubaguzi, ambayo kila moja ni kikwazo kikubwa kwa amani? Je, ulimwengu wenye amani unaweza kujengwa, ni walakini swali lingine la kujiuliza, kama hali iliyopo sasa ya utofauti mkubwa kati ya tajiri na maskini isiposhughulikiwa katika kila pembe ya sayari? Na, siyo hadi wanawake watakapo ruhusiwa kufanya kazi katika nyanja zote za jitihada za wanadamu kwa usawa pamoja na wanaume, ndipo mapigano ambayo yamekuwa tabia ya sehemu kubwa sana ya historia yatatoa nafasi kwa amani na ustawi wa kweli. Vizazi vipya lazima vielimishwe kiujumla kufuatana na kanuni kama hizo, la sivyo kila tumaini kwa ajili ya amani litavunjika kabisa. Pengine ungependa kukariri maneno yafuatayo ya Bahá’u’lláh ili uweze kushiriki pamoja na wengine wanaojali kuhusu mustakabali wa jamii ya wanadamu:

> **“Ustawi wa binadamu, amani na usalama wake, haviwezi kufikiwa isipokuwa na mpaka umoja wake umewekwa imara.”[41]**

# MAREJEO


1. *Makusanyo kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1983, 2017 kuchapisha), CIX, aya. 2, uk. 243.

2. Kama hapo juu., CXXXII, aya. 1, uk. 325.

3. Kama hapo juu., XXXIV, aya. 5, uk. 89.

4. *Nyaraka za Bahá'u'lláh Zilizofunuliwa baada ya Kitáb-i-Aqdas* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1988, 2005 kuchapisha), na. 11.1, uk. 161.

5. Bahá'u'lláh, *Kitáb-i-Íqán: Kitabu cha Yakini* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2003, 2018 kuchapisha), aya. 151, uk. 131.

6. *Makusanyo kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh*, XXVIII, aya. 2, uk. 77.

7. Kama hapo juu., XXIV, aya. 1, uk. 66.

8. Kama hapo juu., CXI, aya. 1, uk. 246.

9. Kama hapo juu., XLIII, aya. 6, uk. 106.

10. Kama hapo juu., CX, aya. 1, uk. 244.

11. *Nyaraka za Bahá'u'lláh Zilizofunuliwa baada ya Kitáb-i-Aqdas*, na. 15.4, uk. 220.

12. *Makusanyo kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh*, XCV, aya. 1, ku. 219–20.

13. *Nyaraka za Bahá'u'lláh Zilizofuuliwa baada ya Kitáb-i-Aqdas*, na. 9.13, uk. 141.

14. Kama hapo juu., na. 5.13, uk. 51.

15. *Makusanyo kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh*, CXII, aya. 1, kur. 247–48.

16. Kama hapo juu., CXXXII, aya. 3, uk. 326.

17. Kama hapo juu., CXI, aya. 1, uk. 246.

18. *Nyaraka za Bahá'u'lláh Zilizofunuliwa baada ya Kitáb-i-Aqdas*, na. 7.20, uk. 90.

19. Kama hapo juu., na. 6.25, ku. 66–67.

20. Bahá'u'lláh, ilivyonukuliwa na Shoghi Effendi, *Majirio ya Haki Takatifu* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2006, 2018 kuchapishwa), aya. 42, p. 41.

21. *Nyaraka za Bahá'u'lláh Zilizofunuliwa baada ya Kitáb-i-Aqdas*, na. 3.23, uk. 27.

22. Bahá'u'lláh, *Maneno Yaliyofichwa* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2003, 2012 kuchapishwa), Kiajemi na. 80, uk. 51.

23. *Nyaraka za Bahá'u'lláh Zilizofunuliwa baada ya Kitáb-i-Aqdas*, na. 6.19, uk. 64.

24. Kama hapo juu., na. 6.37, uk. 71.

25. Bahá'u'lláh, katika *Ḥuqúqu'lláh — Haki ya Mungu: Mkusanyo wa dondoo kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh and 'Abdu'l-Bahá na kutoka Barua zilizoandikwa kwa Niaba ya Shoghi Effendi na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu*, uliyokusanywa na Idara ya Utafiti ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2007), na. 16, uk. 16.

26. *Makusanyo kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh*, CXVIII, aya. 2, uk. 283.

27. Kama hapo juu., CXVII, aya. 1, uk. 282.

28. Bahá'u'lláh, Ilivyonukuliwa na Shoghi Effendi, *Siku Iliyoahidiwa Inakuja* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1996, 2018 kuchapishwa), aya. 279, uk. 187.

29. *Makusanyo kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh*, CXVII, aya. 1, uk. 282.

30. *Nyaraka za Bahá'u'lláh Zilizofunuliwa baada ya Kitáb-i-Aqdas*, na. 4.11, uk. 36.

31. Kama hapo juu., na. 6.3, uk. 57.

32. Kama hapo juu., na. 6.3, uk. 58.

33. *Maneno Yaliyofichwa*, Kiajemi na. 5, ku. 23–24.

34. Bahá'u'lláh, katika *Wanawake: Dondoo kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh, 'Abdu'l-Bahá, Shoghi Effendi na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu*, uliyokusanywa na Idara ya Utafiti ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1986, 1997 kuchapishwa), na. 54, uk. 26.

35. *Maneno Yaliyofichwa*, Kiarabu na. 68, uk. 20.

36. Bahá'u'lláh, katika mkusanyo *Wanawake*, na. 3, uk. 3.

37. Bahá'u'lláh, katika *Ubora katka Vitu Vyote: Mkusanyo wa Dondoo kutoka Maandiko ya Kibahá'í*, uliyokusanywa na Idara ya Utafiti ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu (London: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1981, 1989 kuchapishwa), na. 5, uk. 2.

38. *Makusanyo kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh*, CLVI, aya. 1, uk. 378.

39. Bahá'u'lláh, *Waraka kwa Mwana wa Mbwa mwitu* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1988, 2016 kuchapishwa), uk. 26.

40. *Nyaraka za Bahá'u'lláh Zilizofunuliwa baada ya Kitáb-i-Aqdas*, na. 5.13, uk. 52.

41. *Makusanyo kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh*, CXXXI, aya. 2, uk. 324.



# Dhima za Kujiongezea Elimu Zaidi

## Kusudi

Kukuza tabia ya kutembelea marafiki na majirani kuzungumza juu ya dhima muhimu za kiroho

## SEHEMU YA 1

Kitengo hiki cha tatu, kama kile kilichotangulia, kinahusu uwezo ambao hutuwezesha kuingia kwenye mazungumzo ya maana na yainuayo. Shabaha yetu katika kitengo cha pili ilikuwa juu ya fursa lukuki zinazojitokeza zenyewe kuinua kiwango cha mazungumzo kwa kurejea kwenye kanuni za kiroho. Hapa shabaha inahamia kwenye ziara tunazozifanya kwenye nyumba za marafiki na majirani kwa ajili ya kuchunguza pamoja nao dhima kuu za maisha ya jumuiya.

Katika vijiji na ujirani kila mahali ulimwenguni pote, vikundi vya marafiki vinajihusisha kwa nguvu nyingi katika seti za shughuli zinazohusiana ambazo zinajumuisha mikutano ya ibada ya kila mara, madarasa kwa ajili ya elimu ya kiroho ya watoto, mikutano ya vijana chipukizi, vikundi vya mafunzo, na makambi ya vijana na aina mbali mbali za kampeni. Kadri mtindo huu wa shughuli unavyojikita katika sehemu moja na idadi inayoendelea kuongezeka ya wanaojitolea wenyewe katika vitendo vya huduma, kiini cha marafiki kinaendelea kukua kiidadi na kiuwezo. Programu ya ziara zenye mpangilio kwenye nyumba zaidi na zaidi katika kijiji au ujirani ni kipengele muhimu cha mchakato wa ujenzi wa jumuiya ambao sasa unaongeza mwendo. Dhima anuai huwasilishwa wakati wa matembezi kama hayo. Mwalimu wa Madarasa ya Kibahá'í ya watoto, kwa mfano, lazima awatembelee mara kwa mara wazazi wa watoto ili kujadili dhima zinazohusiana na elimu. Ziara kama hizo zinahitaji kufanywa kwenye nyumba za vijana chipukizi na vijana na wale wanaohudumia kama wahuishaji na wakufunzi ili kujadili mada zinazohusu changamoto na fursa zinazohusiana na hii miaka ya matumaini katika maisha ya binadamu. Mazungumzo yanayofanyika pamoja na wajumbe wa kaya juu ya dhima zinazoimarisha kina cha ujuzi wao wa Imani vile vile huthibitisha kuwa ya muhimu. Kwa vyovyote vile athari za ziara kama hizo kwenye utamaduni wa udugu unaoibuka kwenye jumuiya haziwezi kukadiriwa.

## SEHEMU YA 2

Kwa ajili ya kusudi la kitengo hiki, tutaangalia ujirani wa kufikirika ambamo mchakato ulioelezwa hapo juu unaendelea, na tutautumia kama muktadha kwa ajili ya kuchunguza aina ya mazungumzo yanayoweza kukunjuka wakati wa ziara kwenye nyumba fulani.

Alejandra ni kijana wa kike anayesoma katika chuo kikuu mwaka wa tatu. Yeye na mmoja wa kaka zake, ambaye pia ni mwanafunzi, wanaishi pamoja na wazazi wao katika ujirani tunaoufikiria, katika nyumba walimozaliwa na kukulia. Hao wanne pamoja na wanandoa walioona hivi karibuni ambao wamehamia hivi karibuni katika ujirani huo hukutana kila juma kwa ajili ya kusali na kushauriana juu ya maendeleo ya shughuli zinazoendelea kustawishwa kwenye eneo hilo lenye idadi ya watu takribani 8,000. Wengine watatu wanashiriki wakati hadi wakati katika mikutano hii ya kila juma na wanaanza kufikiria kimpangilio siyo tu juu ya vitendo vyao vya huduma, lakini pia mchakato mzima wa ujenzi wa jumuiya: mwalimu mmoja wa darasa la watoto ambalo lilianza miezi sita iliyopita na vijana wawili wenye umri wa miaka kumi na saba ambao wanaongoza jitihada za kikundi cha vijana chipukizi kwa msaada kutoka kaka mkubwa wa Alejandra, ambaye aliwahi kuwa mhuishaji wa kikundi chao walipokuwa wangali wadogo zaidi na ambaye huwatembelea wazazi wake mara kwa mara.

Seti ya kwanza ya mazungumzo ambayo tutachunguza ni kati ya Alejandra na akina Sanchez, familia maarufu na inayoheshimika katika ujirani. Mume na mke wana umri wa miaka kama sitini hivi na, baada ya kuwalea watoto wao wa kiume na wa kike, wao wanaishi peke yao nyumba chache mbali kutoka kwa makazi ya Alejandra. Bw. na Bi. Sanchez wanajua kusoma na kuandika lakini hawakupata elimu kubwa rasmi ya juu. Heshima kubwa sana wanayopewa ni kutokana na hekima walioipata kupitia uzoefu wao katika maisha yenye ukarimu na vitendo vilivyotakasika. Wao wanatambua mafundisho ya Kibahá'í kwa muda sasa, lakini ni hivi karibuni tu kwamba wao wameamua kuyachunguza kwa dhati. Juma moja lililopita, waliwasiliana na wazazi wa Alejandra kuhusu shauku yao ya kujiunga na jumuiya. Mkusanyiko kwa ajili ya kuwakaribisha ulikuwa tayari umeshapangwa, na zaidi ya hapo, walikubaliana kuwa Alejandra angewatembelea kila mara kwa kipindi cha majuma kadhaa kwa ajili ya kushirikiana nao mlolongo wa dhima zitakazo wasaidia kuongeza kina cha ujuzi wao wa Imani. Kwa kufuatilia kisa cha ziara hizi, mtaweza kuchunguza dhima hizi na kwa wakati huo huo kutafakari juu ya mwenendo wa mazungumzo katika matukio kama hayo.

## SEHEMU YA 3

Alejandra anapanga kuegemeza mazungumzo yake ya kwanza na Bw. na Bi. Sanchez kwenye maelezo mafupi ya dhima hapo chini, Agano la Mungu la milele.

> Muumba wa vitu vyote ni Mungu, Mmoja, Asiyekifani, Aliyepo Mwenyewe. Bahá'u'lláh hutufundisha kwamba asili ya Mungu haiwezi kueleweka na akili ya binadamu, kwa sababu kile ambacho kina mipaka hakiwezi kuelewa kile kisichokuwa na mipaka. Mifano ambayo watu wanaitengeneza juu Yake ni matunda ya fikra zao wenyewe. Mungu siyo mtu, na Yeye siyo nguvu fulani tu iliosambaa katika ulimwengu wote. Maneno ambayo hatunabudi kutumia kurejea kwenye Chanzo cha uwepo wetu, kama vile Baba wa Mbinguni, Uwezo wa Mbinguni, Roho Kuu, yanaelezea majina Yake na sifa katika ulimi wa kibinadamu na hayatoshi hata kidogo kumuelezea Yeye.
>
> Katika Maneno Yaliyofichwa, tunasoma:
>
> **"Ewe Mwana wa Mtu! Nilipendezwa na kuumbwa kwako, ndipo Nikakuumba. Kwa hiyo, nipende, ili niweze kulitaja jina lako na kuijaza roho yako kwa pumzi ya uzima."**[1]
>
> Katika kifungu hiki, Bahá'u'lláh hutuambia kuwa Upendo wa Mungu kwetu ni sababu yenyewe ya uwepo wetu. Lazima daima tutambue upendo huu ambao, hutulinda, hutudumisha, na hutujaza kwa pumzi ya uzima. Katika nyakati za shida au raha, huzuni au furaha, lazima tukumbuke kuwa upendo Wake daima hutukumbatia.
>
> Kutoka mafundisho ya Kibahá'í, tunajifunza kwamba, baada ya kutuumba kutokana na upendo Wake, Mungu ameingia katika Agano pamoja nasi. Neno "agano" linamaanisha mkataba au ahadi kati ya watu wawili au zaidi. Kulingana na Agano la Milele, Muumba Mjaalia Kabisa kamwe hatatutelekeza na, mara kwa mara, anatufahamisha Amri Yake na Kusudi Lake kupitia mmoja wa Wadhihirishaji Wake.

Kitenzi "Kudhihirisha" kinamaanisha kufunua, kuonesha kitu ambacho kilikuwa hakijulikani hapo awali. Wadhihirishaji wa Mungu ni zile Nafsi maalum Ambazo hutufunulia Neno la Mungu. Wao ni Waelimishaji wa ulimwengu ambao hutufundisha jinsi ya kuishi kufuatana na Amri ya Mungu na jinsi ya kufanikisha furaha ya kweli. Miongoni mwa Wadhihirishaji hawa ni Abraham, Krishna, Musa, Zoroasta, Buddha, Kristo, Muḥammad na, bila shaka, Báb na Bahá'u'lláh, Wadhihirishaji Pacha wa Mungu kwa ajili ya zama hizi katika historia ya wanadamu.

Hivyo, katika Agano la Mungu la milele, sehemu Yake daima imekuwa ikitimizwa. Swali la msingi ambalo lazima tujiulize wenyewe ni, "Nawezaje kutimiza sehemu yangu ya Agano?" Jibu tunalopata katika maandiko ya dini zote ni: kwa kumtambua Mdhihirishaji wa Mungu na kutii Mafundisho Yake. Jibu hili linaashiria kwenye kusudi lenyewe la maisha yetu, ambalo ni kumjua na kumwabudu Mungu. Katika Sala Fupi ya Faradhi, tunatamka:

**"Nashuhudia, Ee Mungu wangu, kwamba Wewe umeniumba mimi kukujua Wewe na kukuabudu Wewe. Nahakikisha, katika wakati huu, juu ya unyonge wangu na uwezo Wako, juu ya umaskini wangu na utajiri Wako.**

**"Hakuna Mungu mwingine ila Wewe, Msaada Mashakani, Aliyepo Mwenyewe."**[2]

Kwa kuwa haiwezekani kwetu kumjua Mungu isipokuwa kupitia Wadhihirishaji Wake, njia pekee ya kufanikisha kusudi la maisha yetu ni kwa kuwatambua Wao na kufuata Mafundisho Yao. Leo, mioyo yetu inabubujika kwa shukrani kwa ajili ya fadhila ya kuishi katika wakati ambamo ahadi iliyotolewa katika Vitabu vyote Vitakatifu, kwamba amani na haki vingestawishwa duniani, sasa inaendelea kutimizwa. Bahá'u'lláh hutangaza:

**"Hii ndiyo Siku ambamo fadhila bora kabisa za Mungu zimemiminwa juu ya watu, Siku ambamo neema Yake yenye nguvu kabisa imeingizwa ndani ya viumbe vyote. Imewapasa watu wote wa ulimwengu kusuluhisha tofauti zao, na, kwa umoja kamili na amani, waishi chini ya kivuli cha Mti wa uangalizi Wake na wema Wake wa upendo."**[3]

Kabla ya kuendelea na hadithi yetu, mnapaswa kusoma maelezo yaliyopo hapo juu na kutafakari juu yake aya kwa aya pamoja na washiriki wa kikundi chenu. Mnaweza kuulizana maswali kati yenu na kuyajibu pamoja, hadi kila mmoja wenu atakapoweza kuyaelezea mawazo kiasilia na kwa urahisi. Kujifunza mateuzi vizuri ni muhimu haswa, kwa kuwa kushirikiana vifungu kutoka Maandiko kwenye mijadala ya aina hii hakuepukiki. Mazoezi yafuatayo yatawasaidia kufikiria juu ya mawazo yaliyowasilishwa katika sehemu hii na juu ya maana ya vifungu vilivyonukuliwa:

1. Mngewezaje kumuelezea mtu kwamba Mungu ni asili isiyojulikana? Aya ya kwanza iliyopo hapo juu itaweza kuwasaidia kuhusu suala hili.

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

2. Kwa nini Mungu ametuumba? ____________________________________________

________________________________________________________________________

3. Nini maana ya neno “agano”? ____________________________________________

________________________________________________________________________

4. Mungu ameahidi nini kwa jamii ya binadamu kuhusu Agano Lake la milele?

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

5. Ni lipi kusudi la maisha yetu? ____________________________________________

________________________________________________________________________

6. Kama kamwe hatuwezi kujua asili ya Mungu, inamaanisha nini kwamba kusudi la maisha yetu ni kumjua Mungu? ____________________________________________

________________________________________________________________________

7. Nini maana ya neno “dhihirisha”? ____________________________________________

________________________________________________________________________

8. Taja baadhi ya Wadhihirishaji wa Mungu: ____________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

9. Nini kinahitajika kwetu ili tukamilishe sehemu yetu katika Agano? ______________

________________________________________________________________________

10. Kamilisha sentensi zifuatazo:

a. Katika Siku hii, ________________________________ za Mungu zimemiminwa juu ya jamii ya binadamu.

b. Katika Siku hii, __________________________________ ya Mungu imeingizwa katika vitu vyote vilivyoumbwa.

c. Katika Siku hii, tunapaswa ku ___________________ tofauti zetu, na, kwa umoja kamili na amani, ________________________________________________________

________________________________________________________________ .

11. Bahá’u’lláh anawaambia watu wa ulimwengu wafanye nini? ____________________

________________________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

## SEHEMU YA 4

Maudhui ya dhima ambayo Alejandra anapanga kushirikiana na Bw. na Bi. Sanchez sio jambo pekee alilokuwa nalo akilini mwake. Anatumaini kujenga mafundo imara ya urafiki na wana ndoa hawa. Kutoka uzoefu wa moja kwa moja, anajua athari mbaya kwa vyote ubaguzi na mwelekeo wa kujikweza. Mielekeo hii kiasilia ataepukana nayo, elimu yake ya juu haijamuondolea sifa ya unyenyekevu. Hana chochote moyoni mwake isipokuwa upendo wa kweli na heshima kwa ajili ya akina Sanchez. Wakati anafikiria jinsi atakavyoeleza dhima ya kwanza, anajikumbusha kuwa haya mazungumzo ni mwanzo tu wa mwendelezo wa mazungumzo ambayo yatakunjuka katika majuma mengi yanayofuata. Anatambua kwamba ingawa ni muhimu kuwasilisha mlolongo wa mawazo kwa uwazi, inambidi aweke vituo vya kusikiliza majibu ya wanandoa. “Sipaswi kuwa na wasiwasi,” anajisemea mwenyewe, “kwa sababu nikiendelea kuongea wakati wote bila kusimama, haitatokea nafasi kwa ajili ya mazungumzo kupata mwelekeo.” Alejandra anaendelea kufikiria juu ya ziara yake kwa muda fulani kwa kufuata mawazo haya. Kama mngekuwa kwenye nafasi yake, ni yapi kati ya yafuatayo mngeyazingatia kama  mawazo yanayofaa kuyaingiza akilini mwenu?

_____ Ni kazi yangu kuwaelekeza akina Sanchez katika Imani na kuhakikisha kuwa wanajifunza kila kitu nitakacho wafundisha.

_____ Ni upendeleo ulioje kuweza kutumia muda fulani na wanandoa hawa wa kuvutia na kushirikiana nao vifungu kutoka Maandiko.

_____ Ninajua kuwa ziara hii ni muhimu. Hata hivyo, nina tumaini kuwa haitachukua muda mrefu kwa sababu nina vitu vingine vya kufanya.

_____ Mateuzi yatakuwa magumu sana kwao. Ni bora niwatajie baadhi ya mawazo mepesi. Cha muhimu ni kuwaonesha upendo.

_____ Kwa umri wao, akina Sanchez hawawezi kujifunza mengi.

_____ Ninatazamia kwa hamu kwenye ziara hii na kusikiliza umaizi wao, kadri tutakavyojadiliana dhima na kutafakari juu ya mateuzi.

_____ Wanaweza kusoma. Nitatambulisha mada tu na kuwaachia mateuzi wajifunze wenyewe.

_____ Wakati wa kutambulisha mawazo nitakuwa nikisita mara kadhaa ili tuweze tujifunza mateuzi pamoja na, kushauriana juu yake.

_____ Ninatumaini naweza kuwasilisha mada nzima bila kukatishwa na kuwauliza kama wanamaswali yoyote, mwishoni.

Je, mnaweza kufikiria mawazo mengine ambayo mngependa au msingependa kuwa nayo wakati wa kujiandaa kwa ajili ya ziara kama hiyo?

## SEHEMU YA 5

Ziara ya kwanza ya Alejandra nyumbani kwa familia ya Sanchez inaenda vizuri. Wana ndoa hawa wanatambua kuwa alikuwa na wasiwasi na wanamtuliza kwa fukuto lao la wema. Wanasikiliza kwa umakini na wanashiriki kikamilifu kwenye majadiliano, wakimakinikia zaidi kwenye mateuzi. Ugumu unakuja mwishoni tu pale Bi. Sanchez alipomshtukiza Alejandra kwa swali: “Je, ninamsahau Kristo kwa kujiunga na jumuiya ya Kibahá’í?” Alejandra anajua jibu, lakini inamchukua muda kubuni namna ya kulitoa. Bw. Sanchez anatabasamu na anamsaidia: “Ninafikiri upendo wangu kwa Kristo haswa umeongezeka tangu tulipoanza kujifunza juu ya Mafundisho ya Kibahá’í.” “Na ndivyo ilivyo kwa wengi sana kila mahali ulimwenguni,” Alejandra anaongeza, ambaye amefanikiwa kukusanya mawazo yake pamoja. “Upendo wao kwa Musa, Kristo, Krishna, Buddha, Zoroasta, na Muḥammad unaimarika kwa sababu ya kile Bahá’u’lláh anachofundisha kuhusu umoja wa Mungu, umoja wa dini, na umoja wa wanadamu.”

Ingekuwa yenye msaada kwenu kuchukua muda kidogo kwenye kikundi chenu kujadili baadhi ya sifa na mielekeo ambayo haikuwa na budi kuwepo wakati wa ziara ya Alejandra, kuifanya iwe yenye matunda namna hiyo. Kubwa miongoni mwa sifa ambazo mnahitaji kufikiria ni unyenyekevu. Msingi wa unyenyekevu wote ni unyenyekevu mbele za Mungu. Kutoka kwake huchipuka unyenyekevu mbele ya viumbe Wake. Hakuna wakati wowote ambapo unyenyekevu ni muhimu zaidi kuliko pale mtu amuongeleapo Mungu na Wadhihirishaji Wake. Mnapaswa kutafakari juu ya maneno yafuatayo ya Bahá’u’lláh na mfanye kila jitihada kuyakariri:

> **“Wao ambao ni wapendwa wa Mungu, katika sehemu yoyote ile wakutanapo na yeyote yule wawezaye kukutana naye, sharti wadhihirishe, katika mwelekeo wao kwa Mungu, na katika jinsi ya utukuzaji wa sifa Yake na utukufu, unyenyekevu ule na upole kwamba kila chembe ya vumbi chini ya miguu yao itaweza kushuhudia kina cha moyo wao wa ibada. Mazungumzo yafanywayo na roho hizi takatifu sharti yajazwe na nguvu ile kwamba chembe hizi hizi za vumbi zitasisimuliwa na mvuto wake. Sharti wajiweke wenyewe katika jinsi ambayo kwamba dunia ambayo juu yake wakanyaga isiweze kuruhusiwa kamwe kuwaambia maneno kama haya: ‘Mimi nimependelewa juu yenu. Shuhudieni, jinsi nilivyo na subira katika kuubeba mzigo ambao mkulima ameuweka juu yangu. Mimi ni ile nyenzo ambayo daima hutoa kwa viumbe baraka ambazo Yeye Ambaye Ndiye Chanzo cha neema yote amenikabidhi. Japokuwa nimejaliwa heshima kama hiyo, na ushuhuda usiohesabika wa utajiri wangu — utajiri ambao hutoa mahitaji ya muumbo mzima — tazama kiasi cha unyenyekevu wangu, shuhudia kwa utii kamili ulioje najiruhusu mwenyewe kukanyagwa chini ya miguu ya watu. . . .’”[4]**

Kama ilivyotajwa hapo juu, unyenyekevu mbele ya binadamu wenzetu huibuka kutoka unyenyekevu mbele za Mungu. Ni kwa unyenyekevu huo huo kwamba tunakuwa na mwelekeo wa kiibada tunapokuwa tunatembelea nyumba ya rafiki mmoja au jirani ili kuongeza uelewa wetu wa kina juu ya dhima fulani pamoja. Wakati wa mazungumzo, mara kwa mara tunaelekeza fikra zetu kwa Mungu, tukimuomba Yeye kuangazia akili na mioyo yetu na ile ya kila mtu aliyepo. Kuna vifungu vingi vya maneno na sentensi kutoka sala ambazo tunaweza kukariri pamoja na kusudi hili akilini. Hivi ni vichache tu:

> **“Angazia mioyo yetu, utujalie macho yaonayo na masikio sikivu.”[5]**

**"Ee Bwana! Utujalie baraka Zako zisizo na kikomo, na acha mwanga wa uongozi Wako uwake."[6]**

**"Fungulia milango ya ufahamivu wa kweli na acha mwanga wa imani uwake kwa uangavu."[7]**

**"Ee Bwana! Angazia macho yetu ili kwamba tuweze kuona mwangaza Wako."[8]**

**"Ninageukia Kwako kabisa, nikikusihi Wewe kwa dhati, kwa moyo wangu wote, akili yangu na ulimi wangu, kunikinga kutoka yale yote yanayoenda kinyume na amri Yako katika hili, duru la umoja Wako mtakatifu . . ."[9]**

## SEHEMU YA 6

Moyo wa Alejandra umejaa furaha baada ya ziara yake kwenye nyumba ya akina Sanchez na mazungumzo yake pamoja nao juu ya dhima ya Agano la milele. "Ziara ifuatayo," anafikiria, "ingekuwa fursa nzuri kwao kuongeza kina cha ujuzi wao wa maisha ya Bahá'u'lláh." Ufuatao ni uwasilishaji ambamo atachota:

> Bahá'u'lláh alizaliwa mnamo tarehe 12 Novemba 1817 huko Ṭihrán, mji mkuu wa Uajemi. Kutoka utoto Wake Alionesha sifa zisizokuwa za kawaida, na wazazi Wake walikuwa wenye uhakika kuwa Alikuwa amekusudiwa kwa ajii ya ukuu. Baba Yake Bahá'u'lláh, waziri maarufu katika baraza la mfalme, alikuwa na upendo mwingi mno kwa Mwanaye wa Kiume. Usiku mmoja aliota ndoto kwamba Bahá'u'lláh alikuwa anaogelea katika bahari isiokuwa na mipaka, mwili Wake ukimeremeta na kuangaza bahari hiyo pana. Kuzungukia kichwa Chake nywele Zake ndefu na nyeusi zikielea pande zote. Kundi la samaki lilikusanyika Kumzunguka, kila samaki mmoja akishikilia ncha ya unywele mmoja. Ingawa idadi ya samaki ilikuwa kubwa, hata unywele mmoja haukung'oka kutoka kichwa cha Bahá'u'lláh. Yeye aliogelea kwa uhuru na bila kuzuiliwa, na samaki wote Walimfuata. Baba Yake Bahá'u'lláh alimwuliza mtu mmoja aliyekuwa mashuhuri kutokana na busara zake ili aweze kuelezea ndoto hiyo. Aliambiwa kuwa bahari isio na mipaka ulikuwa ulimwengu wa uwepo. Peke Yake Yeye mwenyewe, Bahá'u'lláh angekuwa na mamlaka juu ulimwengu huo. Kundi la samaki liliwakilisha ghasia ambazo Ataziamsha miongoni mwa watu wa ulimwengu. Atakuwa na ulinzi usioshindwa wa Mwenyezi; ghasia hizi Hazitomdhuru.
>
> Bahá'u'lláh alipofikisha umri wa miaka kumi na tatu au kumi na nne, alikuwa maarufu katika baraza la mfalme kwa ajili ya hekima Yake na ujuzi Wake. Alikuwa ana umri wa miaka ishirini na mbili baba Yake alipofariki, na serikali ilimpatia Bahá'u'lláh wadhifa wa baba yake. Lakini Hakuwa na nia ya kutumia muda Wake kusimamia masuala ya kiulimwengu. Aliacha nyuma baraza na mawaziri wake ili kufuata njia iliyoandaliwa na Mungu kwa ajili Yake. Alitoa muda Wake ili kuwasaidia wadhulumiwa, wagonjwa na maskini, na punde tu akawa maarufu kama chanzo na mtetezi wa haki.
>
> Katika umri wa miaka ishirini na saba, Bahá'u'lláh alipokea kupitia tarishi maalum, baadhi ya Maandiko ya Báb, Ambaye alikuwa Anatangaza mapambazuko ya Siku

mpya, Siku ambamo Mdhihirishaji mpya wa Mungu angeleta amani, umoja na haki kwa ulimwengu ambavyo vimesubiriwa kwa muda mrefu na jamii ya binadamu. Bahá'u'lláh papo hapo alikubali Ujumbe wa Báb na akawa mmoja wa wafuasi Wake wenye shauku kubwa. Lakini ole wao, wale waliowatawala watu Uajemi, wakipofushwa na tamaa zao za kibinafsi, walianza kuwatesa wafuasi wa Báb kwa ukatili mkubwa. Bahá'u'lláh, ingawa alikuwa anajulikana kwa ajili ya uungwana Wake, Alijumuishwa katika mateso hayo. Zaidi kidogo ya miaka minane baada ya kujitangaza kwa Báb, na miaka miwili baada ya Báb Mwenyewe kuwa ameuawa, Alifungwa katika gereza lenye giza chini ya ardhi liitwalo Shimo Jeusi. Minyororo aliowekewa kuzunguka shingo Lake ilikuwa mizito mno kiasi kwamba hakuweza kuinua kichwa Chake. Hapa Bahá'u'lláh alikaa kwa kipindi cha miezi minne mibaya sana katika hali ngumu kabisa. Walakini ilikuwa katika gereza hili hili kwamba roho wa Mungu alijaza roho Yake na kumfunulia kwamba Yeye ndiye alikuwa Yule Mwahidiwa wa zama zote. Kutoka gereza hili lenye giza, Jua la Bahá'u'lláh lilichomoza likiuangazia muumbo mzima.

Baada ya miezi minne katika Shimo Jeusi, Bahá'u'lláh alinyang'anywa mali Zake zote, na Yeye pamoja na familia Yake walipelekwa uhamishoni. Katikati ya msimu wa baridi kali, walisafiri kufuata milima ya magharibi ya Uajemi kuelekea Baghdád, wakati huo jiji katika Ufalme wa Uturuki, na leo ndio mji mkuu wa Iráq. Hakuna maneno yanayoweza kuelezea mateso yao kadri walivyotembea mamia ya kilometa juu ya theluji na ardhi iliyofunikwa kwa barafu, wakiwa njiani kuelekea kwenye mji ule wenye hatma nzito.

Umaarufu wa Bahá'u'lláh punde tu ulisambaa kila mahali Baghdád na miji mingine ya jimbo hilo, na watu zaidi na zaidi walikuja mlangoni kwa Mfungwa huyu aliye uhamishoni ili kupokea baraka Zake. Lakini walikuwepo wachache walio kuwa na husuda juu ya umaarufu Wake. Miongoni mwao alikuwemo mdogo wa kambo wa Bahá'u'lláh Mwenyewe, Mírzá Yaḥyá, ambaye alikuwa anaishi chini ya uangalizi Wake wa upendo. Njama alizokuwa akipanga Mírzá Yaḥyá zilisababisha utengano miongoni mwa wafuasi wa Báb na kumletea huzuni kubwa Bahá'u'lláh. Usiku mmoja, bila kumwambia mtu yeyote, Bahá'u'lláh aliondoka nyumbani Kwake na kwenda kwenye milima ya Kurdistán. Huko Yeye aliishi maisha ya utawa akijishughulisha katika sala na tafakari. Aliishi katika pango dogo na kutumia vyakula vya kawaida kabisa. Hakuna mtu yeyote katika eneo hilo ambaye alifahamu alikotoka, na hakuna mtu yeyote aliyejua jina Lake. Lakini, halafu, polepole watu wa jimbo hilo walianza kuongea juu ya "Yule Asiyekuwa na Jina", Mtakatifu mkuu ambaye alikuwa mwenye ujuzi aliopewa na Mungu. Taarifa za Mtakatifu huyu zilipomfikia 'Abdu'l-Bahá Mwanaye wa kiume wa kwanza wa Bahá'u'lláh, Yeye mara moja alitambua alama za Baba Yake mpendwa. Barua zilipelekwa na tarishi maalum zikimsihi Bahá'u'lláh arejee Baghdád. Hili Alilikubali, na hivyo akamaliza kipindi cha utengano wenye maumivu ambacho kilikuwa kimedumu miaka miwili.

Katika kipindi ambamo Bahá'u'lláh hakuwepo, hali ya jumuiya ya Wabábí ilikuwa imemomonyoka kwa haraka sana. Ndani ya miaka saba ambamo Yeye aliishi Baghdád baada ya kurudi kwake kutoka milimani, Bahá'u'lláh aliingiza roho mpya katika wafuasi wa Báb walioteswa na kuchanganyikiwa. Ingawa Yeye alikuwa bado hajalitangaza daraja Lake Kuu, uwezo wa maneno na hekima Yake vilianza kuvutia utiifu wa idadi iliyokuwa inaongezeka ya Wabábí na upendo wa watu wa kila tabaka la maisha. Lakini makuhani wa Kiislamu wenye msimamo mkali wasingeweza

kuvumilia kuona ushawishi mkubwa aliokuwa nao Bahá'u'lláh juu ya idadi kubwa ya roho kama hizo. Wao walilalamika na kulalamika kwa mamlaka hadi serikali ya Uajemi iliungana pamoja na baadhi ya maafisa wa Ufalme wa Uturuki kumuondoa Bahá'u'lláh na kumpeleka mbali zaidi kutoka nchi Yake ya kuzaliwa, safari hii kuelekea mji wa Constantinople.

Aprili ya mwaka 1863 ulikuwa mwezi wa masikitiko makubwa kwa watu wa Baghdád. Yule Ambaye wao walikuwa wamezoea kumpenda alikuwa anauacha mji wao, akielekea kule wasikokujua. Mara kabla ya kuondoka, Bahá'u'lláh alihamia kwenye bustani moja nje ya mji, aliweka hema Lake pale kwa muda wa siku kumi na mbili na kupokea msururu wa wageni waliokuja Kumuaga. Wafuasi wa Báb walikuja kwenye bustani wakiwa na mioyo mizito, baadhi yao wangemsindikiza Bahá'u'lláh katika hatua iliyofuata ya uhamisho Wake, ingawa wengi ingewalazimu kubaki nyuma na kunyimwa ushirikiano wa karibu pamoja Naye. Lakini Mungu hakupanga kuwa tukio hili liwe lenye huzuni. Milango ya fadhila Zake zisizokuwa na kikomo ilifunguliwa wazi, na Bahá'u'lláh aliwatangazia wote waliomzunguka kwamba Yeye Alikuwa Yule aliyetabiriwa na Báb — Yule Ambaye Mungu angemdhihirisha. Huzuni ikaondoka na kuacha nafasi kwa furaha isiyokuwa na mipaka; mioyo iliinuliwa na roho ziliwaka kwa moto wa upendo Wake. Kipindi cha Siku hizi kumi na mbili katika mwezi Aprili zinasherehekewa kila mahali kama Sikukuu za Riḍván, maadhimisho ya kujitangaza kwa Bahá'u'lláh kuhusu Ujumbe Wake unaokumbatia ulimwengu.


Constantinople ulikuwa mji mkuu wa Ufalme wa Uturuki. Hapa tena, baada ya miezi minne, hekima kubwa na haiba ya kuvutia ya Bahá'u'lláh viliwavutia idadi kubwa ya watu. "Yeye hapaswi kuendelea kuishi hapa Constantinople," walinong'ona makasisi Waislamu wenye msimamo mkali, ambao waliishawishi mamlaka kumhamisha tena kumpeleka katika mji wa Adrianople. Huko Adrianople, ambako alibaki kwa kipindi cha miaka minne na nusu, Bahá'u'lláh aliandika Nyaraka kwa wafalme na watawala wa ulimwengu akiwaita kuacha njia zao za udhalimu na kujidhatiti kujitolea kwa ustawi wa watu wao. Halafu maadui Wake walibuni adhabu nyingine mbaya kabisa. Yeye na familia Yake wangehamishiwa 'Akká, ambako wakati huo palikuwa mahali pa mahabusu mbaya kuliko zote katika ufalme mzima. "Bila shaka Yeye atakufa katika mazingira magumu ya mji-gereza huo," waliwaza watu wenye akili dhaifu ambao walidhani kuwa wao wangeweza kuzuia mipango ya Mungu ambayo Yeye Mwenyewe alikuwa ameanzisha.

Shida alizopata Bahá'u'lláh katika mji wa 'Akká ni nyingi mno kuweza kusimulia. Alinyimwa kila aina ya starehe na alizungukwa na maadui mchana na usiku. Lakini hali ya kifungo polepole ilibadilika. Wakazi wa 'Akká na serikali yake walihakikishiwa juu ya kutokuwa na hatia kwa kundi dogo la Wabahá'í ambao walikuwa wamehamishiwa kwenye mji wao. Kwa mara nyingine tena, watu walivutiwa na hekima na upendo wa Mtu huyu Ambaye hakuwa wa kawaida, japokuwa sehemu kubwa ya watu hawakuelewa daraja Lake la juu. Baada ya kama miaka tisa hivi, milango ya mji-gereza ilifunguliwa kwa Bahá'u'lláh na wafuasi Wake. 'Abdu'l-Bahá Mwanaye mpendwa wa kiume aliweza kumpatia mahali penye heshima kwa ajili ya Baba Yake kuishi nje kidogo ya kuta za mji, na mwishowe 'Abdu'l-Bahá aliweza kupanga nyumba katika maeneo ya shamba ambako Bahá'u'lláh aliweza kuishi miaka kumi na tatu ya mwisho ya maisha Yake, kwa amani na utulivu. Kwa sasa tunitambua nyumba hii kama Jumba la Bahjí, na hapo

ndipo Alipofariki dunia mnamo mwezi Mei 1892 kwenye kilele cha ufahari na utukufu Wake.

Bahá'u'lláh aliinua bendera ya amani ya ulimwengu na udugu na alifunua Neno la Mungu. Ingawa maadui Wake waliunganisha majeshi yao dhidi Yake, Yeye alikuwa mshindi juu yao kama Mungu alivyomwahidi pale alipokuwa katika minyororo katika gereza lenye giza huko Ṭehrán. Wakati wa uhai Wake, Ujumbe Wake ulifufua mioyo ya maelfu ya watu. Na leo, Mafundisho Yake yanaendelea kusambaa kila mahali ulimwenguni. Hakuna kinachoweza kumzuia kutimiza lengo Lake la mwisho, ambalo ni la kuunganisha jamii ya binadamu katika Hoja moja ya ulimwengu, katika Imani moja ya pamoja.

Kisa kilichopo hapo juu cha maisha ya Bahá'u'lláh ni kirefu kiasi. Kabla ya kusonga mbele kwenye mazoezi yaliyopo hapo chini, mnapaswa kusoma kisa chote, aya kwa aya katika kundi chenu na ulizaneni maswali mmoja kwa mwingine hadi mmejifunza maudhui yake vizuri na mnaweza kukiwasilisha kwa ufasaha na urahisi. Ramani ifuatayo itawasaidia katika kukumbusha njia za uhamisho wa Bahá'u'lláh na matukio yaliyotokea njiani.




1. Itakusaidia kuandika katika nafasi iliyopo hapo chini, juu ya msingi wa kisa kilichopo hapo juu, mlolongo wa matukio makubwa yanayohusu maisha ya Bahá'u'lláh.

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

2. Katika mjadala unaozungukia dhima ya maisha ya Bahá'u'lláh, zipo idadi fulani ya dhana ambazo zinatakiwa kutiliwa mkazo, mbali na mlolongo wa matukio. Zenye umuhimu maalum ni tafakari juu ya mateso aliyoyastahimili kutokana na upendo kwa ajili ya jamii ya binadamu, pia ushindi wa ajabu alioupata kupitia Imani Yake mbele ya upinzani. Hebu yaache maneno haya yachongwe katika akili na mioyo yetu:

**"Uzuri wa Kale amekubali kufungwa kwa minyororo ili kwamba binadamu waweze kufunguliwa kutoka kwenye utumwa wao, na amekubali kufanywa mfungwa ndani ya Ngome hii kuu kabisa kwamba dunia yote iweze kufikia kwenye uhuru wa kweli. Amekunywa mashinda ya kikombe cha huzuni, ili watu wote wa dunia waweze kupata shangwe ya kudumu, na kujazwa na furaha. Hii ni kwa huruma ya Bwana wenu, Mwenye huruma, Mwenye rehema Kabisa. Tumekubali kudhalilishwa, Ee waumini katika Umoja wa Mungu, ili muweze kutukuzwa, na tumepatwa na mateso ya namna nyingi, ili muweze kufanikiwa na kusitawi. Yeye Ambaye amekuja kujenga upya ulimwengu wote, tazama, jinsi wao ambao wamefanyiza Mungu washiriki wamemlazimisha Yeye kukaa ndani ya miji ya majangwa kabisa!"**[10]

3. Pale tunapoongelea juu ya mateso ya Bahá'u'lláh, sharti tuwe waangalifu tusimfanye aonekane kama Mtu dhaifu, kama muhanga wa maadui Wake. Yeye amekubali kwa hiari kufungwa katika minyororo ili kuikomboa jamii ya binadamu. Hadithi ya maisha Yake, ingawa imejaa masimulizi ya mateso makubwa, kiasili inaonesha ushindi Wake. Kwa msaada wa Mkufunzi wa kikundi chenu, je, mnaweza kuandaa mazungumzo mafupi juu ya mateso na ushindi wa Bahá'u'lláh kutokana na uelewa mlionao sasa wa maisha Yake? Pengine maswali yaliyopo hapo chini yanaweza kuwa yenye msaada kwenu.

a. Kwa nini Bahá’u’lláh alikubali kufungwa kwa minyororo? __________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

b. Kwa nini Bahá’u’lláh alikubali kuwa mfungwa? __________________________

________________________________________________________________

c. Kwa nini Bahá’u’lláh alikunywa kutoka kikombe cha huzuni? _______________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

d. Kwa nini Bahá’u’lláh alikubali kudhalilishwa? ___________________________

________________________________________________________________

e. Kwa nini Bahá’u’lláh alipata mateso mengi? ______________________________

________________________________________________________________

f. Je, Bahá’u’lláh alikubali kuteswa kwa sababu Yeye alikuwa hana uwezo wa kufanya vinginevyo? ________________________________________________

________________________________________________________________

g. Kama Bahá’u’lláh hakuwa mnyonge mbele ya maadui Wake, basi kwa nini alikubali kuteseka? __________________________________________________

________________________________________________________________

## SEHEMU YA 7

Ziara ya pili ya Alejandra nyumbani kwa akina Sanchez ilikuwa yenye furaha kama ile ya kwanza. Bw. na Bi. Sanchez tayari wamekwisha kuwa na ufahamu juu ya hadithi ya maisha ya Bahá’u’lláh, lakini wanafurahi kujifunza zaidi kutoka kwa uwasilishaji wa Alejandra na wanaonekana kuguswa kwa uwazi na kisa cha mateso Yake. “Inaonekana kuwa,” wakati fulani anasema kwa kutafakari Bi. Sanchez, “Wadhihirishaji wa Mungu daima wanateseka kwenye mikono ya wale ambao wana kiu ya uongozi na uwezo wa kiulimwengu.” Alejandra anaamua kuwa ni sawa kushirikiana nao teuzi ambalo amelikariri — ambalo ninyi pia, mnalifahamu kutoka usomaji wenu wa sehemu iliopita — ambamo Bahá’u’lláh anaongea kuhusu mateso ambayo Ameyastahimili kwa ajili ya jamii ya binadamu, ili kwamba tuweze kuachiliwa huru kutoka ukadamizwaji na kufikia furaha ya milele. Marafiki wote watatu walipata nguvu mpya kutokana na majadiliano ya siku hiyo.

Katika kufikiria ziara yake ya safari inayofuata, Alejandra anaamua haraka kuwa daraja la ‘Abdu’l-Bahá ingekuwa mada inayofaa kwa ajili ya majadiliano yao. Hivi ndivyo vipengele ambavyo atahakikisha anaviongelea:

> Mwana mkubwa wa kiume wa Bahá’u’lláh, ‘Abdu’l-Bahá ni mtu wa kipekee kabisa katika historia ya wanadamu, na hatuwezi kumpata mtu kama Yeye katika dini

yoyote iliyotangulia. Alilitambua daraja takatifu la Baba Yake tangu akiwa mtoto na alishiriki katika uhamisho na mateso Yake. Baada ya kufariki Kwake, Bahá'u'lláh aliiacha Jumuiya ya Kibahá'í chini ya uangalizi na ulinzi wa 'Abdu'l-Bahá. Hatuwezi kamwe kutambua kikamilifu ile fadhila kuu mno ambayo Bahá'u'lláh aliwajalia jamii ya binadamu kwa kutupatia siyo tu Ufunuo Wake bora kabisa lakini pia Mwanae wa Kiume, Ambaye kupitia ujuzi Wake na busara, Yeye alisema kuwa, ulimwengu ungeongozwa na kuangaziwa.

Tunapojifunza maisha na maandiko ya 'Abdu'l-Bahá, tunapata umaizi katika daraja la kipekee Alilinalo katika Maongozi haya. Sura tatu za daraja hili ni za muhimu kwetu kuziweka akilini.

Kwanza, 'Abdu'l-Bahá ni Kiini cha Agano la Bahá'u'lláh. Bahá'u'lláh alifanya agano na wafuasi Wake akiwaita kuelekeza mioyo yao kuelekea kiini hicho na kuwa watiifu kabisa kwake. Katika Wosia Wake na Agano, 'Abdu'l-Bahá alimtaja Shoghi Effendi, Mlinzi wa Imani, kuwa kiini ambacho wote wanapaswa kugeukia baada ya kufariki Kwake. Leo, kiini hiki ni Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, ambayo imeanzishwa kufuatana na amri dhahiri ya Bahá'u'lláh na maagizo wazi yaliyotolewa na 'Abdu'l-Bahá na Mlinzi. Nguvu ya Agano huishikilia Jumuiya ya Kibahá'í pamoja na huilinda kutokana na mgawanyiko na kusambaratika.

Pili, 'Abdu'l-Bahá ni Mfasiri Asiyekosea wa maneno ya Bahá'u'lláh. Ufunuo wa Bahá'u'lláh ni mpana mno, na maana zilizomo katika maandiko Yake ni za kina sana, kiasi kwamba Yeye aliona kuwa lilikuwa jambo muhimu kumwacha Mfasiri, Yule Ambaye Yeye Mwenyewe angempa uvuvio. Hivyo, kwa ajili ya vizazi vijavyo, jamii ya binadamu ingeweza kuelewa mafundisho ya Bahá'u'lláh kwa kujifunza fasiri za 'Abdu'l-Bahá katika Nyaraka Zake nyingi na katika nakala zilizothibitishwa za mazungumzo Yake. Mlinzi alikuwa Mfasiri wa mafundisho ya Bahá'u'lláh baada ya 'Abdu'l-Bahá; Kazi ya ufasiri ilihitimishwa naye, na hakuna aliye na mamlaka kufasiri maneno ya Bahá'u'lláh kwa muda wote uliobaki wa Maongozi Yake.

Katika nyakati zilizopita, kila dini imeathiriwa na mgawanyiko kutokana na fasiri tofauti za vifungu kutoka Maandiko yake Matakatifu. Lakini katika Maongozi haya, pale ambapo hakuna uhakika kuhusu maana ya kauli ya Bahá'u'lláh, kila mmoja hugeukia kwenye fasiri za 'Abdu'l-Bahá na Mlinzi. Mashaka yakibaki, mtu anaweza kuigeukia Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa ajili ya ufafanuzi. Hivyo, hakuna nafasi inayobaki, kwa ajili ya mafarakano juu ya maana ya mafundisho, na umoja wa Imani unalindwa.

Tatu, 'Abdu'l-Bahá ni Mfano kamili wa mafundisho ya Baba Yake. Ingawa kamwe hatuwezi kutumaini kufika kwenye kiwango hicho cha ukamilifu, tunapaswa kumweka Yeye mbele ya macho yetu na kujitahidi kufuata mfano Wake. Pale tunaposoma katika Maandiko juu ya upendo, tunaweza kumgeukia 'Abdu'l-Bahá na tutaona asili yenyewe ya upendo na wema. Tunaposoma kuhusu utakaso, haki, unyoofu, shangwe na ukarimu, tunaweza kumgeukia Yeye na kufikiria maisha Yake, na tutaona jinsi Yeye alivyodhihirisha sifa hizi kwa ukamilifu kabisa.

Alama ya maisha ya 'Abdu'l-Bahá, bila shaka, ilikuwa utumishi Wake. Jina 'Abdu'l-Bahá maana yake ni "mtumishi wa Bahá", na huu ulikuwa wadhifa Wake ambao

Aliupendelea juu ya mwingine wote aliyopewa. Maneno yafuatayo ya ‘Abdu’l-Bahá ni udhihirisho wa shauku Yake kubwa ya kutoa huduma:

**“Jina Langu ni ‘Abdu’l-Bahá. Sifa Yangu ni ‘Abdu’l-Bahá. Uhalisia Wangu ni ‘Abdu’l-Bahá. Utukuzo Wangu ni ‘Abdu’l-Bahá. Utumwa kwa Ukamilifu Uliobarikiwa ni taji langu tukufu na ling’aalo, na utumwa kwa jamii nzima ya binadamu dini yangu ya daima . . . Hakuna jina, hakuna wadhifa, hakuna mtajo, hakuna sifa ambayo Mimi ninayo, wala daima nitakuwa nayo, isipokuwa ‘Abdu’l-Bahá. Hii ndiyo hamu yangu. Hii ndiyo tamaa yangu kuu kabisa. Huu ndiyo uzima wangu wa milele. Huu ndiyo utukufu wangu wa milele.”**[11]

Ni wazi kuwa kile ambacho Alejandra anapanga kushirikina na akina Sanchez katika ziara yake inayofuata siyo zaidi ya kumtambulisha mtu wa kipekee kabisa, Utambuzi wao wa daraja lake ‘Abdu’l-Bahá katika Maongozi haya utaendelea kukua katika miaka ijayo. Katika maisha yenu wenyewe, kadri mtembeavyo kwenye njia ya huduma, mtakuwa na fursa nyingi za kukumbuka mifano Yake na kutafakari juu ya maneno Yake. Tayari, katika kitengo kilichopita mmejifahamisha na baadhi ya maandiko Yake, na mlitiwa moyo kujifunza kuyaelezea mawazo yaliyotolewa katika nyaraka na hotuba Zake kwa namna alivyofanya Yeye. Kwa sasa, ili muweze kuimarisha uelewa wenu wa sasa wa daraja Lake, mnapaswa kushauriana juu ya hoja muhimu zilizotajwa hapo juu na kufanyia mazoezi kuzisema vizuri. Tafakari juu ya kifungu kilichonukuliwa kitawahamasisha katika juhudi zenu za kuendelea kwenye njia ya huduma.

## SEHEMU YA 8

Swali ambalo Alejandra amekuwa nalo akilini mwake tangu alipoanza ziara zake kwa Bw. na Bi. Sanchez limekuwa, ni dhima zipi za majadiliano zingewasaidia zaidi kuweza kupata uthibitisho na kuwa washiriki hai katika mchakato wa ujenzi wa jumuiya katika ujirani. Kwa upande mmoja zipo dhima kama sala, umilele wa roho, uthabiti katika upendo wa Mungu, ambazo anatumaini kujadiliana nao, kwa kuwa msingi wa maisha yao ya kiroho lazima uendelee kuimarishwa. Na kwa upande wa pili, itakuwa muhimu kwao kupata muono juu ya aina ya jumuiya ambayo hatua kwa hatua inaendelezwa na kujua kuwa wanaweza kutoa mchango wenye thamani kwa ajili ya mafanikio yake. Wakati wa mazungumzo yake na Bw. na Bi. Sanchez kuhusu daraja la ‘Abdu’l-Bahá, Alejandra polepole anakuja kutambua kile kitakachokuwa dhima ya ziara yake itakayofuata. “Walipata uelewa mzuri kuhusu kusudi la Imani ambalo ni kuunganisha watu,” anafikiria. “Kwa hiyo, dhima ambayo pengine tunapaswa kuichunguza sasa ni namna ya kujenga na kudumisha jumuiya yenye umoja.”

Alejandra anaanza ziara yake ya nne kwa kuelezea shughuli ambazo kwa sasa zinafanywa na kundi dogo la marafiki katika ujirani. “Kadri idadi yetu inavyoongozeka,” anaeleza, “jukumu lenye changamoto kubwa tulilo nalo ambalo tunapaswa kulibeba ni kuwa wenye umoja zaidi na zaidi katika maneno yetu, katika fikra zetu, na katika vitendo vyetu. Kama mnakubali, basi leo tunaweza kuchunguza mada ya umoja pamoja.”

“Ninaweza kuona jinsi umoja ulivyo muhimu kwa maendeleo ya jumuiya yetu,” anajibu Bi. Sanchez.

"Na baada ya yote, ulikuwa ujumbe wa Bahá'u'lláh juu ya umoja ambao kwanza ulivutia mioyo yetu kwenye Mafundisho Yake," Bw. Sanchez anasema.

"Nimechagua mawazo machache na nimepata teuzi moja kwa kila wazo," Alejandra anasema. "Kama hamtajali", tunaweza kupitia moja baada ya lingine na kuyajadili."

Hapo chini ni orodha ya mawazo ya Alejandra:

- Ili jumuiya yetu iweze kuunganika kwa dhati, lazima kila mmoja wetu aepukane na ugomvi na kushindana. Bahá'u'lláh husema:

**"Hakuna chochote, katika Siku hii, kinachoweza kutia madhara makuu kwenye Hoja hii kuliko mafarakano na ugomvi, kushindana, kutengana na utepetevu, kati ya wapendwa wa Mungu. Vikimbieni, kupitia uwezo wa Mungu na msaada mkuu wa enzi Yake, na jitahidini kufuma pamoja mioyo ya watu, katika Jina Lake, Muunganishaji, Mjua yote, Mwenye Hekima zote."[12]**

- Tunapaswa kuwa na upendo kwa kila mmoja kwenye jumuiya, upendo ambao ni uakisi upendo wetu kwa Mungu. 'Abdu'l-Bahá husema:

**"Muwe katika umoja kamili. Kamwe msikasirikiane mmoja kwa mwingine. . . . Pendeni viumbe kwa ajili ya Mungu na siyo kwa ajili yao wenyewe. Kamwe hamtakasirika au kukosa subira kama mnawapenda kwa ajili ya Mungu. Jamii ya wanadamu siyo kamili. Kuna kasoro katika kila mwanadamu, na daima utakuwa huna furaha kama ukiwaangalia watu wenyewe. Lakini kama ukimwelekea Mungu utawapenda na kuwa mwema kwao, kwa kuwa ulimwengu wa Mungu ni ulimwengu wa ukamilifu na rehema kamili."[13]**

- Pamoja na upendo wote ambao tunahisi mmoja kwa mwingine, kama mivutano itaibuka miongoni mwetu, tunapaswa papo hapo tukumbuke ushauri huu wa 'Abdu'l-Bahá:

**"Ninawaasa kila mmoja kukazia mawazo yenu yote ya moyo wenu juu ya upendo na umoja. Wakati wazo la vita likija, lipinge kwa wazo la nguvu zaidi la amani. Wazo la chuki lazima liangamizwe na wazo la nguvu zaidi la upendo. Mawazo ya vita huleta uharibifu kwa upatano wote, ustawi, utulivu na ridhaa.**

**"Mawazo ya upendo yanajenga udugu, amani, urafiki, na furaha."[14]**

- Na kama, baada ya kufanya juhudi zote kuzidhibiti, tunaona kuwa tamaa zetu zinatushinda na wenyewe tunajikuta katika mafarakano pamoja na wengine, tunapaswa kujikumbusha wenyewe maneno ya Bahá'u'lláh:

**"Kama tofauti zozote zikiibuka miongoni mwenu, nitazameni Mimi nikisimama mbele ya uso wenu, na puuzieni makosa mmoja kwa mwingine kwa ajili ya jina Langu na kama alama ya upendo kwa ajili ya Hoja Yangu dhahiri na angavu."[15]**

- Nidhamu ya kiroho ya kupuuzia makosa ya wengine, kwa kulenga juu ya sifa zao stahiki na kujizuia kabisa kusengenya ni mbinu inayofaa kabisa dhidi ya utengano.

Kuushinda mwelekeo wa kusengenya ni rahisi zaidi pale tunapopendana kati yetu. Lazima tukumbuke kuwa tunatabia ya kutokuona makosa ya wale tunaowapenda na hatuna ugumu kuwatazama kwa jicho linalofunika dhambi. 'Abdu'l-Bahá husema:

**"Jicho lenye kasoro huona mapungufu. Jicho linalofunika makosa linatazama kuelekea kwa Muumba wa roho. Yeye aliwaumba, huwafunza, na huwapatia riziki, huwajalia uwezo na uhai, uoni na usikivu; kwa hiyo, wao ni alama za ukuu Wake. Lazima uwapende na uwe mwema kwa wote, uwajali masikini, uwalinde wadhaifu, uwaponye wagonjwa, uwafundishe na kuwaelimisha wajinga."[16]**

Bahá'u'lláh hutushauri:

**"Ewe Mwenzi wa Kiti Changu cha Ufalme! Usisikie uovu, na usiuone uovu, usijishushe, wala kuhema kwa mashaka na kulia. Usiseme uovu, ili usiweze kuusikia unasemwa kwako, na usiyakuze makosa ya wengine ili makosa yako mwenyewe yasije yakaonekana makubwa; na usimtakie fedheha yeyote, ili fedheha yako mwenyewe isije kufichuliwa. Ishi basi siku za uhai wako ambazo ni chache kuliko muda mfupi upitao, ukiwa na akili yako isiyo na mawaa, moyo wako usiyo na uchafu, mawazo yako safi, na asili yako iliyotakasika, ili kwamba ukiwa huru na aliyeridhika, uweze kuliweka mbali umbo hili la mauti, na kwenda kwenye paradiso isioelezeka na kuishi katika ufalme wa milele hata milele."[17]**

Na hutuambia:

**"Enyi Wahamiaji! Ulimi nimeukusudia kwa kumbukumbu Yangu, msiunajisi kwa kuukashifu. Kama moto wa nafsi ukiwashinda, kumbukeni makosa yenu wenyewe na siyo makosa ya viumbe Wangu, kwa kuwa kila mmoja wenu anaijua nafsi yake mwenyewe zaidi kuliko anavyowajua wengine."[18]**

- Umoja siyo tu ukosefu wa ugomvi na mafarakano, na upendo siyo wa kuoneshwa kwa maneno peke yake. Tunaweza tu kudai kwamba umoja wa kweli upo miongoni mwetu kama upendo wetu wa mmoja kwa mwingine umetafsiriwa katika huduma kwa jumuiya na kama shughuli zetu zinaongozwa kwa roho ya ushirikiano na msaada wa pamoja. 'Abdu'l-Bahá hutuambia:

**"Msipumzike, hata kwa sekunde moja, na msitafute raha, hata kwa muda mfupi; bali mjitahidi kwa moyo na roho ili muweze kutoa huduma ya dhati kwa angalau mmoja miongoni mwa marafiki na kuleta furaha na shangwe angalau kwa moyo mmoja mwangavu. Hii ni fadhila ya kweli, na kupitia kwayo paji la 'Abdu'l-Bahá limeangaziwa. Muwe wenzi Wangu na washiriki humo."[19]**

Na husema:

**"Hitaji kuu la jamii ya wanadamu ni ushirikiano na kusaidiana. Kadiri mafundo ya urafiki na mshikamano yanavyo kuwa yenye nguvu zaidi miongoni mwa watu, ndivyo zitakavyo kuwa kubwa nguvu za ujengaji na kufanikiwa katika ngazi zote za shughuli ya binadamu."[20]**

- Ufunguo wa muhimu kabisa kwa utendaji wa jumuiya yenye mafanikio ni ushauriano wazi na wenye upendo katika mambo yote. Njia mbalimbali ambazo kila mmoja wetu hulitazama jambo huletwa pamoja, kupitia ushauriano, na tunagundua uelekeo gani tunapaswa kuufuata katika utendaji wetu wa pamoja. Kupitia ushauriano, tunafikia umoja wa fikra; na tukiwa na fikra zetu na maoni yaliyounganishwa, tunafanya mipango yenye ufanisi kwa ajili ya ukuaji wa jumuiya zetu. 'Abdu'l-Baha anasema hivi juu ya wale wanaoshauriana:

**"Kigezo kikubwa kwa ajili yao wanaoshauriana pamoja ni usafi wa nia, uangavu wa roho, kujitenga kutoka vyote isipokuwa Mungu, mvuto kwa Manukato Yake Matakatifu, unyenyekevu na udhilifu miongoni mwa wapendwa, subira na ustahimilivu katika matatizo na huduma kwa Kizingiti Chake kilichotukuka. Kama wakiwa wamesaidiwa kwa neema kupata sifa hizi, ushindi kutoka Ufalme usioonekana wa Bahá utakuwa wao."**[21]

- Umoja wa fikra haujakamilika kama haujatafsiriwa katika utendaji wa pamoja. Kutenda katika umoja haimaanishi kwamba wote tunafanya jambo lile lile. Kinyume chake, katika kitendo cha pamoja vipaji mbali mbali vya wajumbe wa jumuiya vinatumika kikamilifu. Nguvu zetu huzidishwa, na hata pale ambapo idadi yetu bado ni ndogo, tunaweza kutimiza kile ambacho mashirika makubwa makubwa zaidi na yenye nguvu ulimwenguni hayawezi kutimiza. 'Abdu'l-Bahá husema:

**"Wakati wowote roho takatifu, zikichota kwenye nguvu za mbinguni zitainuka pamoja na sifa kama hizo za kiroho, na kutembea kwa pamoja, safu kwa safu, kila moja ya roho hizo itakuwa kama elfu moja, na mawimbi yasukasukayo ya ile bahari yenye uwezo yatakuwa vikosi vya Umati wa juu."**[22]

Baada ya kusoma yaliyopo hapo juu kwa uangalifu, na kujadiliana maudhui dondoo kwa dondoo na washiriki katika kikundi chenu, mtapenda kusaidiana kufanya mazoezi ya kuwasilisha mada kama mlivyofanya katika zile tatu zilizotangulia. Mtakuta mazoezi yaliyopo hapo chini ni yenye msaada kwenye juhudi zenu.

1. Kamilisheni sentensi zifuatazo:

   a. Hakuna chochote, katika Siku hii, kinachoweza kutia madhara makuu zaidi kwenye Hoja hii kuliko ____________________ na ugomvi, kushindana, kutengana na utepetevu, kati ya wapendwa wa Mungu.

   b. Hakuna chochote, katika Siku hii, kinachoweza kutia madhara makuu zaidi kwenye Hoja hii kuliko mafarakano na _______________ , kushindana, kutengana na utepetevu, kati ya wapendwa wa Mungu.

   c. ________________ chochote kinachoweza, katika Siku hii, kutia madhara makuu zaidi kwenye Hoja hii kuliko mafarakano na ugomvi, kushindana, kutengana na utepetevu, kati ya wapendwa wa Mungu.

d. Hakuna chochote kinachoweza, katika Siku hii, kutia madhara makuu zaidi kwenye Hoja hii kuliko mafarakano na ugomvi, kushindana, kutengana ____________________ , kati ya wapendwa wa Mungu.

e. Hakuna chochote, katika Siku hii, kinachoweza kutia madhara makuu zaidi kwenye Hoja hii kuliko mafarakano na ugomvi, ___________________ , kutengana na utepetevu, kati ya wapendwa wa Mungu.

f. Hakuna chochote, katika Siku hii kinachoweza kutia madhara makuu zaidi kwenye Hoja hii kuliko mafarakano na ugomvi, kushindana, _________________ na utepetevu, kati ya wapendwa wa Mungu.

g. Hakuna chochote, katika Siku hii, kinachoweza kutia madhara makuu zaidi kwenye_____________ hii kuliko mafarakano na ugomvi, kushindana, kutengana na utepetevu, kati ya wapendwa wa Mungu.

2. Katika teuzi la pili, 'Abdu'l-Bahá hutuambia:

a. Lazima tuishi katika __________________ kamili.

b. Kamwe tusi ______________ kwa ________________________ .

c. Lazima tuwapende watu wote kwa ajili ya _______________________________ na siyo kwa ajili yao wenyewe.

d. Kamwe hatuwezi ____________________ au ____________________ kama tunawapenda watu kwa ajili ya ________________ .

e. Jamii ya wanadamu siyo _______________ .

f. Daima tutaweza __________________________ kama tukitazama kuelekea ___________________________ .

g. Kama tukitazama kuelekea ______________ , tuta ________________ watu na kuwa ________________ kwao.

3. Katika teuzi la tatu, 'Abdu'l-Bahá hutuambia:

a. Kila mmoja wetu lazima amakinikie mawazo yote ya mioyo yetu juu ya _______________ na ________________ .

b. Wakati wazo la vita likija, sharti tulipinge kwa _______________________ ___________________________ .

c. Wazo la chuki linaweza kuharibiwa ______________________________

____________________ .

d. Mawazo ya vita huleta madhara kwa ______________ , ______________ ,

__________________ na ______________ .

e. Mawazo ya upendo yanajenga __________________ , ______________ ,

___________________ , na ___________________ .

4. Mnapaswa kufanya nini unapoona tofauti zinaibuka kati yako mwenyewe na wengine katika jumuiya? ______________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

5. Eleza nidhamu ya kiroho ambayo hukusaidia kuchangia kuleta umoja katika jumuiya yako: ______________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

6. Ni zipi miongoni mwa zifuatazo zinachangia katika umoja?

_____ Kuangalia mapungufu ya wengine

_____ Kupuuzia makosa ya wengine

_____ Kutoa maoni juu ya mapungufu ya mtu mwingine kwa rafiki mmoja

_____ Kukuza au kubadilisha hadithi ili kumfanya mtu aonekane mbaya.

_____ Kufikiria makosa ya wengine

7. Kwa nini tunawakosoa baadhi ya watu pale wanapofanya makosa, na siyo wengine, wanapofanya kosa hilo hilo? ______________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

8. Je, inawezekana kuwa na umoja katika hali ambamo watu wanasengenyana? Kwa nini haiwezekani? ____________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

9. Kusema uongo juu ya mtu fulani ni wazi kuwa ni kosa. Lakini je, ni sawa kutoa maoni yenye kukosoa kuhusu mtu mmoja kwa wengine juu ya kitu ambacho kweli amekifanya?

10. Ni ipi tofauti kati ya umbea, usengenyaji, na kuwakosoa wengine?

11. Umbea, usengenyaji, na ukosoaji wa mara kwa mara vina athari gani kwenye jumuiya?

12. Tunawezaje kutokomeza tabia hizi katika maisha yetu?

13. Ni nini kingetokea kama tu tungewaongelea watu kana kwamba wapo mbele yetu?

14. Kama tukisengenya mbele ya watoto, itakuwa na athari gani juu yao?

15. Desturi ya umbea na kujihusisha katika usengenyaji inatoka wapi?

16. Bahá'u'lláh anatuonya: "Kama moto wa nafsi ukiwashinda, ____________________ ____________________ na siyo ________________________________ , kwa kuwa kila mmoja wenu anaijua __________________________________ kuliko ana ________________________ ."

17. Upendo hauelezwi tu kwa maneno. Kitu gani kingine kinahitajika? _____________ ____________________________________________________________________

18. Kuhusu umoja na upendo, 'Abdu'l-Bahá hutuambia: "_________________ hata kwa sekunde moja, na ________________________ , hata kwa muda mfupi; bali _____________________ kwa ____________________________ ili muweze kutoa __________________________ kwa angalau mmoja miongoni mwa marafiki na _______________________________ angalau kwa moyo mmoja mwangavu".

19. Na Yeye anaendelea kusema: "Hitaji kuu la jamii ya wanadamu ni ________________________ na ______________________ . Kadiri mafundo _________________ na __________________ yanavyo kuwa yenye nguvu zaidi miongoni mwa watu, ndivyo zitakavyo kuwa kubwa nguvu za ________________ na ____________________ katika ngazi zote za shughuli ya wanadamu."

20. Ni upi ufunguo muhimu kabisa kwa mafanikio ya utendaji wa jumuiya? _________ ____________________________________________________________________

21. 'Abdu'l-Bahá anasema kwa wale wanaoshauriana: "Kigezo kikubwa kwa ajili yao wanaoshauriana pamoja _____________________________ , __________________ ________________ , ________________________________________________ __________ , _______________________________________________________ , __________________________________________ miongoni mwa wapendwa Wake, _____________________________________ katika matatizo na ________________ kwenye Kizingiti Chake kilichotukuka. Kama wao wakiwa wamesaidiwa kwa neema kupata sifa hizi _______________ kutoka Ufalme usioonekana wa Bahá utakuwa wao."

22. Kuhusu nguvu ya kufanya kazi kwa umoja,'Abdu'l-Bahá anatuambia: "Wakati wowote roho takatifu, zikichota ________________________________________ , zitainuka pamoja na ______________________________________ , na kutembea _______________ , safu kwa safu, ________________ ya roho hizo zitakuwa _______________________ , na mawimbi yasukasukayo ya bahari hiyo kuu yatakuwa kama _________________ vya ____________________________ ."

## SEHEMU YA 9

Katika ziara yake ya nne kwa Bw. na Bi. Sanchez, Alejandra anapata furaha ya kukutana na Beatrice, mjukuu wa kike ambaye amekuja kuishi nao huku akiendelea na masomo yake ya sekondari kwenye shule iliyopo jirani. Beatrice ni mdadisi sana juu ya dhima ya umoja na anashiriki kwa shauku kubwa katika majadiliano. Kadri mazungumzo yanavyokaribia mwisho, Bi. Sanchez huleta kahawa na keki kwa ajili ya kila mmoja. Hii inampa Alejandra fursa ya kumjua Beatrice vizuri zaidi, na anapanga kukutana naye siku inayofuata kwa ajili ya kuongea juu ya juhudi za ujenzi wa jumuiya katika ujirani. "Yeye pengine angependa kusoma mlolongo mkuu wa kozi," Alejandra anafikiria mwenyewe. "Ningeweza kumsaidia kupitia vitabu vichache vya mwanzo kwa kasi ya kawaida. Pengine baadaye angetaka kuanza darasa la watoto au kusaidia kikundi cha vijana chipukizi kilichoundwa katika ujirani. Kwa hali hiyo, polepole angebeba majukumu mengi zaidi kwa ajili ya kikundi kadri atakavyoendelea hadi Kitabu cha 5, ambacho kingemwandaa kutoa huduma kama mhuishaji." Alejandra amehudhuria mikusanyiko kadhaa ya vijana ambayo ililenga mada fulani za majadiliano, ambayo imepelekea kwenye ushiriki wa wengi kwenye mchakato wa taasisi. Anaamua kuwa atafuata mlolongo uleule wa mawazo katika mazungumzo yake na Beatrice siku inayofuata. Hivi ndivyo mazungumzo yanavyoanza:

> Sisi sote tunataka kuona ulimwengu uwe mahali pazuri zaidi. Tunatazamia kuwa na mustakabali ambapo amani ya ulimwengu imestawishwa na familia ya wanadamu huishi kwa upatano. Mustakabali kama huo siyo ndoto na unaweza kujengwa kadri wengi zaidi na zaidi kati yetu tunavyofanya jitihada za kuchangia kwenye uboreshaji wa ulimwengu. Ndani kabisa ya mioyo yetu kila mmoja wetu anashauku ya kutumikia jumuiya yetu. Kile ambacho tunahitaji ni kukuza uwezo wetu wa kufanya vitendo vya huduma bila ubinafsi kwa ajili ya ustawi wa wote.
>
> Tunaweza kufikiri kuhusu huduma yetu kwa jamii ya wanadamu kwa kufikiria njia ya huduma ambayo kwayo tunatembea pamoja. Njia hii iko wazi kwa wote. Kila mmoja wetu anaweza kufanya uchaguzi wa kuingia humo, na kuendelea juu yake kwa hatua zetu wenyewe. Hatutembei njia hii peke yetu; tunahudumia sambamba na marafiki zetu, kujifunza pamoja na kuambatana mmoja kwa mwingine. Kila hatua tunayo chukua huzaa furaha na uhakika, na kila jitihada tunayofanya huleta uthibitisho mtakatifu.

Beatrice anapenda kile anachosikia, na mazungumzo yenye uchangamfu yanafuata baada ya uwasilishaji huu mfupi. Kabla ya kwenda mbele zaidi, hebu tusite kidogo hapa na kutafakari juu asili ya mwingiliano wa utendaji kati ya marafiki wapya wawili. Alejandra ameamua kujiusisha kwenye mazungumzo ya maana ili kumwalika Beatrice kushiriki katika mchakato wa taasisi. Kwa nini isingetosha tu kumwambia Beatrice kuna mlolongo wa kozi zinatolewa na taasisi na kumkaribisha kujiunga nazo?

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

## SEHEMU YA 10

Mazungumzo kati ya Alejandra na Beatrice yanaendelea kwa takribani masaa mawili. Hapa chini yapo mawazo mengine kadhaa ya ziada ambayo Alejandra anashirikiana na rafiki yake mpya. Bila shaka, tunaelewa kuwa yeye hawezi kufanya uwasilishaji mrefu bila kuukatisha. Sehemu kubwa ya masaa mawili inatumika kujadili pamoja juu ya mawazo yaliyoelezwa katika aya hizi:

> Sisi ni vijana, tuna nguvu, na tuna shauku kubwa. Watu wanadhani kuwa hatujali. Lakini ni kinyume chake, tunajali mustakabali wa jamii ya wanadamu na tungependa kuona mabadiliko ya kweli yakiletwa katika jamii. Na lazima pia tufikiri juu ya maisha yetu wenyewe — elimu, kazi, marafiki, familia. Kila mwaka kadiri tunavyokuwa wakubwa, tunajikuta tunabeba majukumu mengi zaidi wenyewe; wazazi wetu wanategemea mengi kutoka kwetu. Wakati mwingine, ninapofikiria majukumu yangu yote, ninajihisi kuzidiwa. Halafu nakumbuka teuzi nililolikariri kutoka kwenye maandiko ya Kibahá'í: "Maisha ya mwanadamu yana msimu wake wa mchipuo na yamejaliwa utukufu wa ajabu. Kipindi cha ujana kina ainishwa na nguvu na uwezo ambavyo vinajitokeza wakati bora kabisa katika maisha ya mwanadamu."
>
> Kile ambacho ningependa kushiriki na wewe ni kwamba vijana wengi kote ulimwenguni katika jumuiya kama zetu wanaendelea kutambua kuwa nguvu zetu zinaweza kuelekezwa kwa kusudi lenye pande mbili: kuchukua wajibu wa ukuaji wao wenyewe wa kiakili na wa kiroho na kuchangia katika mabadiliko ya jamii. Sura hizi mbili za kusudi letu zimeunganika. Kadri tunavyokuza uwezo wetu wenyewe, tunaweza kuwahudumia wengine vizuri zaidi, na katika kusaidiana wenyewe, kama watu binafsi tunakua na kuimarisha tunu tulizonazo.
>
> Hapa ndipo wazo la njia ya huduma nililotaja linapo kuja. Kutembea humo siyo kitu ambacho tunaongeza tu katika maisha yetu; huleta maana kwa kila kitu tunachofanya. Huduma kwa jumuiya hutusaidia kuelewa vizuri zaidi kusudi la elimu yetu, kuweka wazi fikra zetu kuhusu siku zijazo, kukuza sifa tunazozihitaji kwa ajili ya kuchangia kwa ustawi wa familia zetu. Huimarisha urafiki wetu. Hutufanya tusipoteze nguvu zetu juu ya mambo ya kipuuzi.
>
> Katika kufikiria juu ya ukuaji wetu wa kiroho na kiakili, lazima tutambue kuwa zipo nguvu nyingi zinazotushawishi. Baadhi yao, ni kama vile nguvu ya ujuzi, ya haki, na ya upendo, ambazo hutupeleka katika mwelekeo sahihi, na lazima tujifunze kujiweka wenyewe sambamba nazo. Zingine, ni kama vile nguvu za ubinafsi na tabia ya kuchukulia kuwa umiliki wa vitu vya kimwili na anasa za dunia kuwa muhimu zaidi kuliko tunu za kiroho, zinafanya kinyume chake, na tunapaswa kuzipinga. Lazima tujitahidi kufikia ubora na kuwa na imani kwamba juhudi zetu zitabarikiwa kwa uthibitisho mtakatifu.

Na katika kufikiria juu ya michango yetu kwenye mbadiliko wa jamii — kuubadilisha ulimwengu wenye vurugu, umaskini, na mateso kuwa ulimwengu wenye amani, ustawi, na upatano — lazima tufikirie vyote viwili maendeleo ya kimwili na ya kiroho. Maendeleo ya kimwili kwa ajili ya watu wote hayatafikiwa ikiwa hatujengi maendeleo ya kiroho pia. Ni pale tu vitu hivi viwili vikienda bega kwa bega ndipo uboreshaji wa ulimwengu utakapotimizwa. Lipo teuzi lingine ambalo nimelikariri: "Ustaarabu wa kimwili ni kama taa, ambapo ustaarabu wa kiroho ni mwangaza ndani ya taa hiyo. Kama ustaarabu wa kimwili na wa kiroho unaunganika, ndipo tutakuwa na mwangaza na taa pamoja, na matokeo yake yatakuwa kamili."

Kadri tutembeavyo kwenye njia ya huduma, tunajifunza kufanya kazi na vikundi vya watu binafsi, hususani watoto na vijana chipukizi, tukiwasaidia kupata ujuzi, stadi, na sifa za kiroho. Pia tunajifunza kuwa makini zaidi kwenye umoja wa jumuiya zetu. Watu binafsi, familia, na mashirika ambayo yanapenda kuchangia kwenye maendeleo ya jumuiya lazima washirikiane. Lazima wajenge muono wa pamoja na kusudi na kuacha nyuma njia zenye migogoro.

Ni muhimu basi, kwamba sisi kama vijana tukuze tabia za mwingiliano wenye upatano na wengine. Tunahitaji kuwa marafiki: kuambatana mmoja kwa mwingine katika kazi tunayoifanya, kila mmoja akikubali michango ya mwenzake, tukihamasishana na kusaidiana, tukitambua nguvu ya kila mmoja wetu, kutafuta na kupeana ushauri unaosaidia, na kufurahia mafanikio ya kila mmoja. Katika kukanyaga njia ya huduma, lazima tutende, tutafakari juu ya vitendo vyetu, tushauriane na tujifunze pamoja.

Katika miongo michache iliyopita, jumuiya ya Kibahá'í imefanikiwa kuanzisha asasi maalum kabisa ya ujifunzaji katika takribani kila nchi ya ulimwengu. Asasi hizi ndizo tunazoziita, taasisi, ambazo hutoa kozi zinazoimarisha uwezo wetu wa kuhudumia jumuiya. Kwa kujifunza kozi hizi, tunapata umaizi wa kiroho na stadi za kufanyia kazi zihitajikazo kwa ajili ya kusonga mbele kwenye njia ya huduma pamoja. Kadri tunavyoendelea kuzipitia, ndivyo uwezo wetu wa kufanya vitendo vya huduma vyenye utata uongezekao hukua. Wakati wote, tunasindikizwa na wale ambao wana uzoefu zaidi kuliko sisi, na kadri muda unavyopita tunaambatana kiasilia na marafiki wenye uzeofu mdogo. Tangu mwanzo, sote ni washiriki wakuu wa mabadiliko ya mtu binafsi na ya jamii, tukibeba majukumu kwa shauku kubwa kwa ajili ya ujifunzaji wetu wenyewe na kwa ajili ya kuhudumia jumuiya.

"Kuwa mshiriki mkuu" maana yake ni kuwa mwenye nia ya kutenda kwa kutafakari, kustahimili katika jitihada zetu, na kupata na kutumia ujuzi kwenye kila hatua. Mshiriki mkuu siyo tu mpokeaji mtepetevu wa manufaa, bali ni mchangiaji hai katika maendeleo. Ili kuwa mshiriki mkuu mtu lazima ajifunze kufanya jitihada za kiubunifu na zenye nidhamu. Kozi za taasisi zinatusaidia kuongeza uwezo wetu wa kuwa washiriki wakuu wa mchakato wa ujenzi wa jumuiya.

Tunapaswa tuchukue muda kidogo wa kutafakari juu ya mawazo yaliyopo katika aya za hapo juu. Kama ilivyotajwa katika mwanzo wa sehemu hii, Alejandra asingeweza kuwasilisha tu mawazo yake moja baada ya lingine, bali angehakikisha kuwa Beatrice amepata fursa ya kutosha kufikiria juu yake na kuchangia kwenye majadiliano. Kile ambacho pengine mngependa kufikiria — baada ya ninyi kupata nafasi ya kujadili kila aya katika kikundi chenu na mmekwisha jifunza kuyaeleza mawazo kwa ufasaha ninyi wenyewe — ni

kama mazungumzo yameshafikia mahala ambapo Alejandra angeweza kujihisi mwenye ujasiri katika kushiriki maneno machache kuhusu baadhi ya kozi za taasisi na katika kumualika Beatrice kujiunga na mafunzo ya Kitabu cha 1. Je, mnaweza kuandika katika nafasi iliyopo hapo chini kile ambacho mngesema kama ninyi mngekuwa yeye? Mngevielezeaje Vitabu vya 1 na 2 na vitendo vya huduma vinavyohamasishwa humo? Maelezo mafupi juu ya vitendo vya huduma vinavyofanywa katika vitabu vinavyofuata — hususani katika kufundisha madarasa ya elimu ya kiroho ya watoto na kuongoza kikundi cha vijana chipukizi kama mhuishaji wake — bila shaka yangemsaidia Beatrice kupata mtazamo wa huduma ipi angeweza kutoa katika siku za mbele. Mkufunzi wa kikundi chenu anaweza kuwasaidia katika kuandika sentensi chache juu ya vitendo hivi viwili vya huduma, sawa na vile ambavyo Alejandra angeongeza katika kumualika Beatrice kujifunza Kitabu cha 1.

## SEHEMU YA 11

Majuma mawili yanapita kabla Alejandra hajafanya ziara nyingine nyumbani kwa Sanchez. Katika kipindi hicho, Beatrice aliweza kushiriki katika kampeni za taasisi na kukamilisha vitengo viwili vya kwanza vya Kitabu cha 1. Kwa sasa anapitia kitengo cha tatu pamoja na kikundi cha marafiki watano kinachokutana mara mbili kwa wiki katika ujirani. Alejandra anafikiria kuwa ni muda muafaka wa kuzungumza na familia ya Sanchez juu ya dhima ya sala na anamuliza Beatrice kama angependa kumsaidia. Ninyi wenyewe mmesoma kitengo cha pili cha Kitabu cha 1, kwa hiyo hakuna ulazima wa kufanya muhtasari kwa ajili yenu hapa juu ya maudhui yaliyoongelewa na Alejandra na Beatrice wakati wa ziara. Baada ya kupitia tena kitengo hicho, mnapaswa kuwa na uwezo wa kubainisha hoja muhimu ambazo mngeweza kuzielezea katika mjadala kuhusiana na dhima hii. Hapo chini ipo nafasi kwa ajili yenu kuandika mawazo yenu.

## SEHEMU YA 12

Ziara za Alejandra kwa Familia ya Sanchez zinaendelea kwa majuma kadhaa yajayo, na wanapata fursa ya kujadili dhima kadhaa ambazo hutiririka kiasilia kutoka kwenye

mazungumzo yao juu ya umuhimu wa sala — maisha ya roho, maendeleo ya sifa za kiroho, utii kwa sheria na kanuni za Mungu na uthabiti katika upendo Wake. Wakati mmoja, walizungumzia pia kidogo kuhusu asasi za Utaratibu wa Kiutawala, hususani kuhusu Mabaraza ya Kiroho ya Mahali na ya Kitaifa. Hatuhitaji kufikiria maudhui waliyoongelea katika kila ziara iliyofuata. Hata hivyo, yapo maswali mawili ambayo aghalabu huibuka miongoni mwa washiriki katika mlolongo wa mazungumzo kama haya tunayoyatazamia. La kwanza linahusu asili ya mikutano inayoitishwa na jumuiya na la pili linahusu rasilimali fedha. Tutaongelea suala la mikutano hasa Karamu ya Siku Kumi na Tisa, katika sehemu hii na kuangalia suala linalohusu fedha katika sehemu inayofuata.

Hoja zifuatazo zinaweza kuunda msingi wa mazungumzo juu ya dhima ya Karamu ya Siku Kumi na Tisa:

- Katika jumuiya ya Kibahá'í, mikutano inafanywa kwa makusudi mbalimbali — kufanya ibada, kujifunza, kusherehekea matukio maalum, kushauriana juu ya masuala ya jumuiya na huduma kwa jamii, kujadiliana mipango ya utekelezaji. Bahá'u'lláh anatupa ahadi ifuatayo:

  **"Kwa uhai Wangu na Hoja Yangu! Kuzungukia makazi yoyote ambamo marafiki wa Mungu wataingia, na ambamo kutoka humo sauti zao zitainuka watakapokuwa wanamsifu na kumtukuza Bwana, zitazungukia zile roho za waumini wa kweli na malaika wote waliopendelewa."[23]**

- Kusikiliza Neno la Mungu katika mikutano miongoni mwa marafiki huleta furaha kwenye mioyo na huimarisha mafundo ya umoja. Bahá'u'lláh hutusihi:

  **"Inawapasa marafiki katika nchi yoyote waishimo, kukusanyika pamoja katika mikutano, na humo kuongea kwa busara na kwa ufasaha, na kusoma aya za Mungu; kwa kuwa ni Maneno ya Mungu yanayowasha moto wa upendo na kuufanya uwake."[24]**

  'Abdu'l-Bahá huandika:

  **"Fanyeni mikutano na someni na mghani Mafundisho ya mbinguni, ili pengine mji huo uweze kuangaziwa kwa mwangaza wa ukweli na kwamba nchi hiyo iweze, kupitia uthibitisho wa Roho Mtakatifu, kuwa kama paradiso yenye kufurahisha, kwa kuwa zama hizi ni karne ya Bwana Mtukufu Kabisa, na lahani ya umoja wa jamii ya binadamu ya ulimwengu inafika kwenye masikio kila mahali Mashariki na Magharibi."[25]**

- Kati ya mikutano yote ya Kibahá'í, Karamu ya Siku Kumi na Tisa hustahili mtajo maalum. Kalenda ya Kibahá'í ina miezi kumi na tisa yenye siku kumi na tisa kila mmoja, na, katika kila mahali, Wabahá'í hukusanyika pamoja mara moja kwa mwezi kwa kuwa mkutano huu umeamriwa na Bahá'u'lláh Mwenyewe:

  **"Hakika imeamrishwa juu yenu kufanya karamu, mara moja kila mwezi, hata kama ni kwa maji tu; kwa maana Mungu amekusudia kuunganisha mioyo pamoja, japo kupitia namna zote mbili za kidunia na za mbinguni."[26]**

- Karamu ya Siku Kumi na Tisa ina sehemu tatu. Sehemu ya kwanza ni ya ibada, ambamo sala na vifungu kutoka Maandiko Matakatifu husomwa. Sehemu ya pili ni ya kiutawala, ambamo jumuiya hushauriana juu ya masuala yanayofanyika mahali hapo. Sehemu ya tatu ni ya kijamii.

- Tunapata kuona kidogo umuhimu wa sehemu ya ibada ya Karamu ya Siku Kumi na Tisa kutoka maneno yafuatayo ya 'Abdu'l-Bahá:

> **"Enyi watumishi watiifu wa Uzuri wa Kale! Katika kila duru na maongozi, karamu imependelewa na kupendwa, na kuandaa meza kwa ajili ya wapenzi wa Mungu imechukuliwa kuwa kitendo kinachostahili sifa. Hii ndiyo ilivyo hali hususani leo, katika maongozi haya yasiyo na kifani, zama hizi zenye ukarimu kuliko nyingine zote, pale inaposifika sana, kwa kuwa kiukweli miongoni mwa ile mikutano ambayo inafanywa kwa ajili ya kumwabudu na kumtukuza Mungu. Hapa aya takatifu, mashairi na sifa zinaimbwa na moyo unachapuzwa, na kuchukuliwa kutoka nafsi yake yenyewe**."[27]

- Wakati wa sehemu ya utawala ya Karamu, marafiki waliyokusanyika husikiliza taarifa za shughuli za jumuiya ya Kibahá'í za karibu na mbali, hushauriana juu ya masuala ya Imani katika jumuiya yao wenyewe na juu ya michango kwa ajili ya ustawi wa jamii, hujifahamisha na miongozo iliyopokelewa kutoka Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, hutafakari juu ya maendeleo ya mipango yao, na hutoa mapendekezo kwenye asasi za Imani. Ushauriano katika Karamu ya Siku Kumi na Tisa ni wa umuhimu kabisa, kwani, kupitia mbinu hii, kila mtu binafsi anaweza kushiriki katika masuala ya jumuiya ya Kibahá'í ulimweguni kote.

- Kuhusiana na sehemu ya kijamii ya Karamu, huu ni muda kwa ajili ya urafiki na ukarimu. Muziki unaweza kuchezwa, mazungumzo yainuayo yanaweza kutolewa, na uwasilishwaji kufanywa na watoto. Kwa kifupi, uchaguzi makini wa maonesho ya kitamaduni, ambayo yanaheshima na wakati huo huo yenye furaha, yanaweza kutumiwa ili kusheheneshsa sehemu hii ya Karamu.

- Karamu ya Siku Kumi na Tisa ni sura muhimu ya Utaratibu wa Utawala wa Imani. Huleta pamoja sura za kiibada, kiutawala, na kijamii za maisha ya jumuiya. Sura zote hizi lazima zitiliwe mkazo sawasawa, kwa kuwa mafanikio ya Karamu yanategemea juu ya mizania sahihi miongoni mwa sehemu hizi tatu. Katika ujumbe wake ulioandikwa mwezi Agosti 1989, Nyumba ya Haki ya Ulimwengu husema:

> **"Utaratibu wa Ulimwengu wa Bahá'u'lláh hukumbatia nyanja zote za jamii ya binadamu; huunganisha michakato ya kiroho, kiutawala na ya maisha ya kijamii; na huelekeza njia kwa ajili ya mtazamo wa kibinadamu katika miundo yake tofauti kuelekea ujenzi wa ustaarabu mpya. Karamu ya Siku Kumi na Tisa hukumbatia sura zote hizi kwenye msingi wenyewe wa jamii. Hufanywa katika kijiji, mji, jiji, ni asasi ambamo watu wote wa Bahá ni wajumbe wake. Imekusudiwa kuendeleza umoja, kuhakikisha maendeleo, na kulea furaha."[28]**

- Tukio muhimu kama Karamu ya Siku Kumi na Tisa haliwezi kufanywa kwa haraka. Kupitia sala na tafakari, kila mtu binafsi lazima ajiandae kiroho kwa ajili ya Karamu, na wakati wa tukio lenyewe, kila mmoja anapaswa kushiriki kwa moyo na akili, iwe kusoma wakati wa sehemu ya ibada au kusikiliza tu kwenye vifungu vinaposomwa;

iwe kutoa taarifa, kupokea mwongozo, au kutoa mapendekezo; iwe kuwa mkaribishaji au anashiriki kama mkaribishwa tu kwa ukarimu wake wa furaha na angavu. Katika barua hiyohiyo juu ya Karamu ya Siku Kumi na Tisa, Nyumba ya Haki ya Ulimwengu husema:

**"Sura Muhimu za maandalizi ya Karamu zinajumuisha uteuzi wa maandiko yanayofaa, upangaji wa wasomaji wazuri mapema, na hisia ya staha pote pawili katika uwasilishaji na katika upokeaji wa programu ya ibada. Umakini wa mazingira ambamo Karamu itafanyika, iwe ndani au nje, utakuwa wenye mvuto mkubwa. Usafi, mpangilio wa mandhari katika njia za vitendo na zinazopendeza—vyote vina nafasi muhimu. Kujali muda pia ni kipimo kizuri cha maandalizi.**

**"Kwa kiwango kikubwa sana mafanikio ya Karamu hutegemea juu ya ubora wa maandalizi na ushiriki wa mtu binafsi. Bwana Mpendwa anatoa ushauri ufuatao: 'Wekeni uzito mkubwa juu ya mikutano ya Siku Kumi na Tisa, ili katika tukio hili wapendwa wa Bwana na vijakazi wa Mwenye Rehema waweze kugeuza nyuso zao kuelekea Ufalme, kuimba sifa, kusihi msaada wa Mungu, kujawa na furaha mmoja kwa mwingine, na kukua katika utakaso na utakatifu, na katika kicho cha Mungu, na katika kujiepusha na tamaa mbaya na ubinafsi. Hivyo watajitenga wenyewe kutoka ulimwengu huu wa asili, na kujizamisha wenyewe katika shauku kali ya roho.'"[29]**

Kama kawaida, mnapaswa kusoma mawazo ya hapo juu mara kadhaa na muyajadili katika kikundi chenu ili kwamba mjifunze kuyasema kwa urahisi. Mazoezi yafuatayo yatawasaidia kupata umaizi zaidi katika umuhimu wa Karamu ya Siku Kumi na Tisa:

1. Bahá'u'lláh anatuhakikishia kitu gani kitakachobainisha kila makazi ambamo tunakusanyika pamoja kumsifu na kumtukuza Bwana? ________________________

   ________________________________________________________________________

2. Katika teuzi la pili lililopo hapo juu, Bahá'u'lláh anatuambia kuwa, pale tunapokuja pamoja katika mikutano, sharti tuongee __________________________ na kwa _________________ , na kusoma _____________________________ ; kwa kuwa ni Maneno ya Mungu ambayo__________________________________________________ __________________________________ na _________________________________ .

3. Katika teuzi la tatu lililopo hapo juu, 'Abdu'l-Bahá anatushauri kufanya mikutano na kusoma na kuimba Mafundisho ya mbinguni, kwamba

   – mji ambamo tunaishi uweze kuwa ________________________________________ ____________________ .

   – nchi ambamo tunaishi iweze kuwa ________________________________________ ______________________________________________________________________ .

4. Kalenda ya Kibahá'í ina miezi mingapi? ____________________

5. Kila mwezi una siku ngapi? ____________________

6. Mkutano gani maalum hufanyika mara moja kila mwezi miongoni mwa Wabahá'í?

____________________

7. Ni zipi sehemu tatu za Karamu ya Siku Kumi na Tisa? ____________________

____________________

____________________

8. Je, sehemu za Karamu ya Siku Kumi na Tisa zinafanyika kwa mpangilio maalum? _

____________________

9. Ni lipi kusudi la sehemu ya ibada ya Karamu? ____________________

____________________

____________________

____________________

____________________

10. Ni lipi kusudi la sehemu ya kiutawala ya Karamu? ____________________

____________________

____________________

____________________

____________________

11. Ni lipi kusudi la sehemu ya kijamii ya Karamu? ____________________

____________________

____________________

____________________

____________________

12. Mada zipi miongoni mwa zifuatazo zingefaa kujadiliwa wakati wa sehemu ya kiutawala ya Karamu?

_____ Mahitaji ya kifedha ya shughuli ambazo jumuiya inazifanya

_____ Magoli ya timu ya mpira ya taifa

_____ Jinsi ya kumaliza malumbano kati ya wajumbe wawili wa jumuiya

_____ Maendeleo ya madarasa ya watoto ya Kibahá'í katika jumuiya

_____ Maana ya kifungu kutoka Maandiko ambacho mmoja wa wajumbe wa jumuiya alikuwa anajifunza mwanzoni mwa juma

_____ Uhai wa programu ya vijana chipukizi katika jumuiya

_____ Fursa za kazi zilizopo kijijini kwa ajili ya vijana

_____ Msaada ambao jumuiya inaweza kuutoa kwa vikundi vya vijana chipukizi ambavyo miradi yao ya huduma imekuwa na utata

_____ Ziara kwa wazazi wa watoto na vijana chipukizi katika programu za kielimu zinazoendeshwa na taasisi

_____ Uimara wa tabia ya kiibada ya jumuiya

_____ Matukio ya maonesho yanayotolewa kwenye runinga

_____ Umaizi uliopatikana kuhusu kulea mandhari yenye furaha na nidhamu katika vikundi vya mafunzo

_____ Kusherehekea Sikukuu Takatifu ijayo

_____ Jitihada za shughuli ya kijamii inayoibuka kutokana na mchakato wa ujenzi wa jumuiya

13. Jadilini swali lifuatalo kwenye kikundi chenu: Kwa nini mizania miongoni mwa sehemu tatu za Karamu ni muhimu sana?

14. Sasa jadilini maswali mawili yaliyopo hapa chini.

    a. Ungejiandaaje kwa ajili ya Karamu unayoikaribisha?

    b. Ungejiandaa namna gani kwa ajili ya Karamu ambayo wewe ni mshiriki tu?

## SEHEMU YA 13

Swali la pili ambalo aghalabu huibuka katika mazungumzo juu ya Imani ni kwa namna gani jumuiya ya Kibahá'í inakidhi mahitaji yake ya kifedha. Hapa kuna hoja chache zitakazo wasaidia kujibu maswali kama hayo.

- Nyenzo ambayo jumuiya ya Kibahá'í inatumia kwa jili ya kushughulikia mahitaji yake ya kimwili ni Mfuko wa Hazina wa Kibahá'í. Ambayo husimamiwa na asasi za Imani kwenye ngazi tofauti tofauti: mahali, kitaifa, kibara, na kimataifa. Wabahá'í wanaamini kuwa wao wenyewe wanapaswa kubeba gharama za jitihada za kuendeleza Imani yao, na kwa hiyo Mfuko wa Hazina hupokea michango kutoka wajumbe wa jumuiya ya kibahai pekee.

- Uchangiaji kwa Mfuko wa Hazina ni tendo la hiari. Ni siri kwa kumaanisha kuwa ni jambo linalohusu mtu binafsi na asasi ya Imani; majina ya wachangiaji na kiasi wanachotoa havitangazwi. Hakuna shinikizo juu ya wajumbe wa jumuiya kuchangia. Asasi huitangazia jumuiya kwa pamoja, kuikumbusha umuhimu wa Mfuko wa Hazina, na kueleza mahitaji. Aghalabu jumuiya inaweza kuweka lengo la kiasi cha michango inayohitaji kwa ajili yake yenyewe. Lakini mtu haambiwi kiwango cha kutoa kamwe, na pesa haiombwi. Imeachwa kwa kila mtu binafsi kuamua kulingana na uelewa wake wa kanuni zinazohusika ni kiasi gani cha kuchangia.

- Ustaarabu ambao tunajaribu kuujenga utakuwa wenye ufanisi pote pawili wa kimwili na wa kiroho. Utajiri unakubalika pale tu kama vigezo fulani vinafuatwa. Sharti tuupate kupitia kazi halali. Tunapaswa kuutumia kwa ajili ya maslahi ya jamii ya binadamu. Na jumuiya nzima inapaswa kuinuliwa; haikubaliki kuwa wachache wawe matajiri wa kupindukia wakati sehemu kubwa ya watu wana shida ya kupata hata vitu vya msingi tu vya maisha. Bahá'u'lláh hutuambia:

**"Watu bora kabisa kuliko wote ni wale ambao hupata riziki kwa kazi zao na kutumia kwa ajili yao wenyewe na kwa ajili ya ndugu zao kwa upendo wa Mungu Bwana wa malimwengu yote."[30]**

**". . . ninyi lazima mzae matunda mema na ya ajabu, ili ninyi wenyewe na wengine mpate kunufaika nayo. Hivyo inampasa kila mmoja kujishughulisha katika ufundi na taaluma, kwa kuwa humo ndimo ilimo siri ya mali, Enyi watu wa ufahamu!"[31]**

Na 'Abdu'l-Bahá hueleza:

**"Utajiri ni wa kupongezwa sana, kwa sharti kwamba jamii nzima ni tajiri. Ikiwa hata hivyo, wachache wana utajiri wa kupindukia, wakati wengi wao wanaishi katika umaskini uliokithiri, na hakuna tunda au manufaa yatokanayo na utajiri huo, hivyo basi hapo ni hasara tu kwa mmiliki wake."[32]**

- Kujenga jamii ambayo ni huru kutokana na utovu wa haki na masaibu, lazima sote tuwe wakarimu na wanaotoa. Hata kama vyanzo vyetu vya kifedha ni vidogo, bado tunaweza kuchangia chochote kuelekea maendeleo ya jamii ya binadamu, kwa kuwa ustawi wa kweli unaweza kupatikana tu kupitia utoaji. Ukarimu ni sifa ya roho ya mtu; haina uhusiano na hali zetu za kiuchumi. Katika Maneno Yaliyofichwa, Bahá'u'lláh husema:

**"Kutoa na kuwa mkarimu ni sifa Zangu; heri ni yake yule ajipambaye kwa njema Zangu."[33]**

- Tunapaswa kukumbuka kwamba chanzo cha kweli cha utajiri wowote tunaoumiliki, ni Mungu, Mjaalia wa vyote. Yeye hutupatia njia zetu za kuishi; Yeye hufanya iwezekane kwa sisi kuendelea. Na pale tunapochangia kwenye Mfuko wa Hazina, tunatumia kwa ajili ya Hoja Yake sehemu ya kile alichotupatia. Hivyo basi, kwa Wabahá'í, kutoa kwenye Mfuko wa Hazina siyo tu suala la ukarimu; pia ni fadhila ya kiroho na jukumu kubwa la mtu binafsi. Mlinzi hutushauri:

**" Sisi lazima tuwe mithili ya kisima au chemchemi ambayo inaendelea kumwaga nje yote yaliyomo ndani mwake na inaendelea kujazwa tena kutoka chanzo kisichoonekana. Kuweza kutoa kwa uendelevu kwa ajili ya maslahi ya wenzetu bila kuzuiliwa na woga wa umaskini na kwa kutegemea fadhila isiyoshindwa ya Chanzo cha utajiri wote na wema wote — hii ndiyo siri ya kuishi kwa usahihi."[34]**

Mtapata fursa ya kufikiria baadhi ya mawazo hapa kwa kina zaidi katika kozi za baadaye katika mlolongo huu, ambayo inaongelea mada ya nyenzo za kimwili. Kwa sasa, mnatiwa moyo kama siku zote, kujadiliana maudhui yaliyopo hapo juu kipengele kwa kipengele na kufanya mazoezi yafuatayo ili muweze kujifunza kuyaelezea mawazo kwa kiasilia na kwa urahisi:

1. Kwa kuzingatia mateuzi, jaza nafasi wazi katika sentensi hapa chini.

   a. Bahá'u'lláh hutuambia kwamba lazima tupate __________________ kwa kazi yetu na tuitumie kwa ajili ya __________________________________________ .

   b. Sisi lazima tuzae matunda _______________ na _________________ ili sisi wenyewe na wengine _________________________________ .

   c. Kila mmoja wetu lazima _______________________ katika ___________ na ________________ , kwa kuwa humo ndimo ilimo ________________ ya ______________ .

   d. 'Abdu'l-Bahá hueleza kuwa utajiri ni wa _________________________ , kwa sharti kwamba ___________________________ ni tajiri.

   e. Kama ______________ wanao __________________________________ ambapo ______________________________________________ , na hakuna ___________ au _______________ inayopatikana kutoka _______________ , basi hapo ni ______________ tu kwa _____________________ .

   f. Bahá'u'lláh husema, "____________ na kuwa ______________ ni sifa Zangu; heri ni yake yule _______________ mwenyewe ____________ Zangu."

   g. Na Mlinzi anatuhamasisha kuwa mithili ya ______________ au ____________ ambayo daima ina __________________________ yote yaliyomo ndani mwake na inaendelea ____________________________________________________ .

   h. Kuendelea ___________________ kwa ajili ya ______________________ wenzetu _______________________ kwa ____________________________ na kutegemea _________________________________________________________ _________________________________ — hii ndiyo siri ya kuishi kwa usahihi.

2. Andikeni mlolongo wa mawazo yaliyofuatiliwa katika uwasilishaji uliyopo hapo juu:

____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________

## SEHEMU YA 14

Ili kupata umaizi katika aina za mazungumzo ambayo yanaweza kukunjuka katika kijiji au ujirani ambamo shughuli nyingi zinafanyika, tumezifuatilia juhudi za Alejandra, mwanafunzi kijana wa chuo kikuu. Katika mlolongo wa ziara, ambao ulichukua majuma kadhaa, amejadiliana na Bw. na Bi. Sanchez idadi fulani ya dhima ambazo, anatumaini, zitawasaidia kuongeza kina cha ufahamivu wao wa Imani na kuimarisha kujidhatiti kwao kwenye mafundisho ambayo wameyakumbatia. Hatimaye, kuwasili kwa Beatrice, mjukuu wa akina Sanchez, ulituwezesha kuchunguza aina nyingine ya mazungumzo, hii ilikuwa kati ya vijana wawili, ambao wote wana shauku ya kujifunza jinsi wanavyoweza kuhudumia jumuiya yao. Wakati wa kuendelea na kisa hiki na katika kufanya mazoezi, tumeona kuwa, zaidi ya kuongeza ujuzi wa mada zinazohusika, sifa kadhaa za kiroho, mielekeo na stadi zinahitajika ili kudumisha mazungumzo ambayo tunayafikiria hapa.

Katika sehemu hii na inayofuata ya kitengo hiki tutachunguza dhima za aina tofauti — yaani, zile ambazo kwa kawaida zinachukuliwa kwa ajili ya majadiliano wakati wa ziara kwa familia pamoja na vijana wanaoshiriki katika programu za kielimu zinazoanzishwa na taasisi. Kama ambavyo imekwisha dokezwa, ufundishaji wa madarasa kwa ajili ya watoto na

kuongoza kikundi cha vijana chipukizi kama mhuishaji ni vitendo vya huduma vinavyoongelewa katika kozi zinazofuata, katika Kitabu cha 3 na cha 5 mtawalia. Mnaweza kuwa mnazifahamu au hamzifahamu programu hizi mbili, kutegemeana na ikiwa ninyi wenyewe mlishiriki programu hizi katika umri mdogo.

Hebu tuangalie, kwanza, maudhui ambayo aghalabu yanaunda msingi kwa ajili ya mazungumzo endelevu na familia za vijana chipukizi. Tutadhani kwamba muda fulani umepita tangu tulipoacha hadithi yetu na kwamba Beatrice sasa anasoma Kitabu cha 2. Alejandra anamuuliza rafiki yake kama angependa kumsindikiza atakapo kwenda kuzitembelea familia za vijana chipukizi kadhaa kuanzisha kikundi kwa msaada wake. Anakubali kwa shauku.

Alejandra anamweleza Beatrice kile anachotazamia. "Tutaanza kila ziara," anamfahamisha, "kutambulisha kwa wazazi programu ambayo mtoto wao wa kiume au wa kike ameonesha shauku kujiunga nayo, na kwa kutaja kuwa hiyo ni sehemu ya mchakato wa ujenzi wa jumuiya unaoendelea kufanyika katika ujirani. Kisha tutachunguza pamoja nao baadhi ya dhana na mawazo makuu ya programu. Hii itakuwa ya kwanza kati ya mlolongo wa ziara zetu, na matumaini yetu ni kwamba, kadri mazungumzo yanavyoendelea, muda unavyopita, siyo tu familia hii itakisaidia kikundi kwa nguvu katika njia tofauti bali pia watakuwa waendelezaji wa uwezeshwaji wa kiroho wa vijana chipukizi katika jumuiya."

Alejandra na Beatrice wanaendelea kujadiliana baadhi ya hoja ambazo wamepanga kuongelea pamoja na kila familia. Wanaamua kuandika mawazo yote wanayofikiria ni muhimu, wakijua fika kuwa wataweza kuyazungumzia machache tu kati yao katika ziara yao ya kwanza na wataongelea mengine katika mazungumzo yatakayofuata. Hapa zipo hoja ambazo wanataja kuhusu uwezo uliomo ndani ya vijana chipukizi:

- Katika maisha ya mtu, miaka mitatu kati ya umri wa miaka 12 na 15 ni kipindi muhimu sana — hatua ya mpito kutoka utoto hadi ukomavu.

- Aghalabu sisi huwaita vijana katika rika hili kama "vijana chipukizi". Wao siyo watoto tena lakini bado hawajafikia ujana kamili.

- Kwa bahati mbaya, ipo taswira potofu walakini iliyoenea sana kuwa vijana chipukizi ni watundu, wakaidi, wanajipenda na walioko hatarini wakati wowote. Hata hivyo, tunawaona katika mwangaza tofauti. Ni kweli kuwa, mnamo kipindi hiki kifupi cha maisha, sote tunapitia mabadiliko ya haraka, kimwili, kimihemko, na kiakili. Na pia ni kweli kuwa, kama matokeo yake, tunaweza kuonesha ukaidi fulani. Lakini, kiuhalisia, huu ni umri wenye uwezo mkubwa usiodhihirika na wenye matumaini makubwa.

- Sisi wenyewe tulikuwa vijana chipukizi siyo muda mrefu uliyopita na tumbuke jinsi tulivyoathirika na mabadiliko haya. Wakati mwingine tulikuwa jasiri na wakati mwingine waoga. Wakati fulani tulipenda kuchangamana na wengine na wakati mwingine tulikuwa wenye aibu. Aghalabu tulionesha hamu ya kuachwa wenyewe huku tukitumaini kupokea umakinifu. Tulitaka kuelewa vitu gani tuliweza kufanya vizuri na vipaji na uwezo tuliokuwa nao. Na tulijali sana jinsi watu walivyotuangalia na waliyachukuliaje mawazo yetu.

- Jambo muhimu la kutambua ni kwamba tabia kama hii ni ya mpito tu. Katika maisha ya binadamu ni mnamo kipindi cha miaka hii ambamo nguvu fulani za kiakili hukua kwa haraka. Tunaanza kutafuta majibu kwa maswali ya kimsingi juu ya uwepo. Tunaanza kuchambua yote yanayotuzunguka na kuhoji takriban kila kitu tulichofundishwa. Na hatuko tayari kama tulivyokuwa wakati mmoja kufuata kila tunachoambiwa na watu wazima bila kuuliza, hususani pale tunapoona mkanganyiko kati ya maneno na vitendo vyao.

- Kama vijana wanatakiwa kusaidiwa kutumia ipasavyo nguvu zao zinazoanza kuibuka, ni lazima kuepuka kuwatendea kana kwamba wao ni watoto. Hivi ndivyo 'Abdu'l-Bahá anavyokieleza kipindi hiki:

> **"Baada ya muda anaingia katika kipindi cha ujana, ambamo hali yake na mahitaji ya zamani yanapitwa na mahitaji mapya yanayoweza kutumika katika kuendeleza daraja lake. Vipawa vyake vya kuchunguza vinapanuka na kujiimarisha; uwezo wake wa kiakili unafunzwa na kuamshwa; mapungufu na mazingira ya utoto havizuii tena nguvu zake na mafanikio yake."**[35]

- Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, chombo cha kiutawala cha Imani ya Kibahá'í, inasema hili kuhusu njia ambayo tumeifuata katika kufanya kazi pamoja na vijana chipukizi:

> **"Wakati mielekeo ya ulimwengu huonesha taswira ya kundi rika hili kama tatanishi, iliyopotea katika machungu ya mabadiliko yakimsukosuko yakimwili yakihisia, isiyoitika na iliyoteketezwa na nafsi, jumuiya ya Kibaha'i — katika lugha iitumiayo na njia iichukuayo — inasonga mbele kwa vyovyote vile katika upande mwingine, ikiona katika vijana chipukizi badala yake utu, hisia kali ya haki, hamu ya kujifunza juu ya ulimwengu na tamaa ya kuchangia kwa ujenzi wa ulimwengu bora zaidi."**[36]

Alejandra na Beatrice kisha wanageuzia umakinifu wao kwenye programu ya uwezeshwaji wa kiroho yenyewe na kujaribu kubaini baadhi ya sura zake:

- Wale wenye umri kati ya miaka 12 na 15 hutamani kuwa sehemu ya kikundi cha marafiki wanaoweza kushirikiana nao mawazo yao, kufanya miradi, kucheza michezo na kadhalika. Kwa sababu hii, programu imejengwa kuzungukia dhana ya "kikundi cha vijana chipukizi". Kila kikundi kinaongozwa na "mhuishaji", aghalabu kijana mkubwa zaidi ambaye, kama rafiki wa kweli kwa wajumbe, huwasaidia kuendeleza uwezo wao.

- Vikundi hukutana mara kwa mara. Katika mikutano yao, vijana chipukizi hujifunza kuchunguza dhana na kuelezea mawazo bila hofu ya kukosolewa au kuchekwa. Hutiwa moyo kusikiliza, kuongea, kutafakari, kuchambua, kufanya maamuzi, na kuyafanyia kazi.

- Tunaishi katika wakati ambamo nguvu nyingi hasi zinaathiri jinsi vijana chipukizi wanavyofikiri na wanavyoenenda. Wahuishaji huwasaidia kupambatana na nguvu hizi — siyo tu kuwalinda wenyewe kutoka mmomonyoko wa maadili wa jamii bali pia kwa ajili ya uboreshaji wa ulimwengu.

- Programu inatafuta kulea nguvu zilizomo kiasili katika roho ya binadamu, uwezo ambao mnamo miaka ya mwanzo wa ujana unaanza kujitokeza wenyewe kwa kiasi kikubwa zaidi na zaidi. Vyenye umuhimu wa kipekee ni uwezo wa fikra na kujieleza. Vijana lazima wakuze lugha inayohitajika pote pawili kuelezea mawazo ya kina juu ya ulimwengu na kusema jinsi wao wanavyotaka kuuona unavyobadilika.

- Vijana chipukizi wana shauku ya kutafakari juu ya maana ya dhana za kimsingi kwa ajili ya maisha yenye maana. Furaha, matumaini, na ubora ni mifano michache. Kwa masikitiko watu huelekea kuongea juu ya mawazo haya katika njia ya kijuujuu. Kupata uelewa wa kina wa dhana kama hizi, wakitambua jinsi wanavyoweza kujieleza katika maisha ya kila siku, kunaweza kusaidia akili za vijana katika kujenga muundo imara wa kimaadili na katika kuhimili nguvu hasi za jamii.

- Uelewa wa dhana ni wa lazima kwa maendeleo ya kiakili. Vijana chipukizi wakati mwingine wanaweza kukabiliana na ugumu shuleni kwa sababu wanategemewa kujifunza habari nyingi sana juu ya mada tofauti, bila kupata msaada wa kutosha kuelewa dhana kwenye msingi wake. Programu hii inawahamasisha kufikiri kwa kina juu ya mawazo — ya kimaadili, kihisabati, kisayansi, na kadhalika — na hii bila shaka huboresha utendaji wao shuleni.

- Vijana chipukizi wana shauku kubwa ya kufanya mambo yenye mantiki. Wanataka kuelewa sababu za kile kinachotokea kuwazunguka. Ili waweze kufanikiwa, wanapaswa kuwa na uwezo wa kuona siyo tu kwa macho yao ya kimwili bali pia kwa jicho la kiroho. Lengo muhimu la programu, kwa hiyo, ni uimarishaji wa utambuzi wa kiroho: uwezo wa kutambua nguvu za kiroho na kubaini kanuni za kiroho katika hali wanazokutana nazo.

- Programu hufanikisha malengo yake mbalimbali — kukuza maadili, utambuzi wa kiroho, na uwezo wa kujieleza — kwa msaada wa mlolongo wa vitabu. Vitabu vina hadithi rahisi juu ya maisha ya vijana katika sehemu mbalimbali za ulimwengu. Zaidi ya kusoma vitabu hivi pamoja, kujadili maudhui yake na kufanya mazoezi yanayohitajika, vijana chipukizi hushiriki katika michezo na kujifunza juu ya sanaa na ufundi.

- Kwa msaada wa mhuishaji, vikundi pia hubuni na hutekeleza mlolongo wa miradi ya huduma, ambacho ni kipengele kikubwa cha programu. Kupitia miradi hii, vijana chipukizi hujifunza kufikiri juu ya jumuiya na mahitaji yake, kushauriana, na kushirikiana kati yao wenyewe na pamoja na wengine katika jumuiya.

- Mada zilizomo katika vitabu ni tofauti; kila moja inalenga juu ya dhima ya lazima kwa uwezeshwaji wa kiroho wa vijana chipukizi. Kitabu cha kwanza, kwa mfano, kinaongelea dhima ya "uthibitisho" — kwamba Mungu huthibitisha juudi tuzifanyazo ili kufanikisha malengo bora. Kitabu kingine ni juu ya "matumaini" — Namna ambavyo tunalazimika kutazama wakati ujao kwa matumaini hata katika nyakati ngumu kabisa. Kingine kinachambua dhana ya "ubora". "Furaha" ni dhima ya hadithi moja, wakati "nguvu ya neno" ni mada ya tafakari katika kitabu kingine. Miongoni mwa vitabu vinavyoongelea dhana za kihisabati, kimoja huchunguza tabia za akili yenye mpangilio. Katika nyanja ya sayansi, kipo kitabu kinacholenga utunzaji wa afya ya mtu — kimwili, kiakili, na kiroho. Na kuna dazeni au zaidi ya vitabu ambavyo vijana chipukizi huvisoma katika kipindi cha miaka hiyo mitatu.

Alejandra na Beatrice wanapanga kuja na vitabu kadhaa vya vijana chipukizi, ili kama wazazi watapenda kuvitazama na kuvisoma. Ikiwa hamjajifahamisha vizuri na vitabu hivi, itawasaidia kama mtachukua muda kidogo kusoma hadithi nyingi kadri muwezavyo — hii itawawezesha kufuatilia vizuri zaidi mazungumzo tofauti yanayokunjuka katika jumuiya. Wakati huohuo, mnatiwa moyo kujadiliana kikamilifu pamoja na washiriki wengine katika kikundi chenu cha mafunzo, mawazo yaliyowasilishwa hapo juu, ambayo yameongelewa kwa kina zaidi katika Kitabu cha 5. Kama, baada ya kusoma kitabu hicho, mnaamua kutoa huduma kama wahuishaji wa kikundi cha vijana chipukizi, mtafanya ziara za kiimpangilio kwa familia za wanakikundi na kuchunguza pamoja nao mawazo kama haya na mengine yanayofanana. Lakini hata sasa, kama Beatrice, pengine mngependa kuambatana na mtu mwenye uzoefu zaidi katika ziara chache kwa familia za vijana chipukizi katika jumuiya yenu.

## SEHEMU YA 15

Siku inayofuata, Alejandra na Beatrice wanatembelea nyumba za vijana chipukizi watatu ambao watajiunga na kikundi kipya ambacho kinaundwa katika ujirani. Beatrice amefurahi kuona shauku waliyoonesha wazazi wakati wa kushiriki katika mazungumzo juu ya programu ya uwezeshwaji wa kiroho. Hadi kufika jioni, alikuwa amepata uhakika kuwa angependa kumsaidia Alejandra pamoja na kikundi cha vijana chipukizi na kujifunza kuhudumia kama mhuishaji wa kikundi kipya yeye mwenyewe, pengine katika mwaka huo huo. Yeye anatambua, bila shaka, kuwa bado anahitaji kusoma vitabu vingine vichache vya taasisi. Lakini amedhamiria kuendelea kuvisoma kwa kasi ileile imara iliyomfikisha hadi hapo.

Hivyo ndivyo ilivyo kuwa, kwa msaada endelevu na hamasa kutoka kwa Alejandra, Beatrice anasonga mbele kwenye njia ya huduma. Tutapitia tena hadithi yake, baada ya miezi michache, ambapo atakuwa karibu anamaliza Kitabu cha 3. Mkufunzi wa kikundi chake cha mafunzo amemuomba Maribel, mwalimu wa darasa la watoto, kumualika Beatrice na washiriki wenzake kuambatana naye, kwa zamu, kwenye ziara kwa wazazi wa watoto walio katika darasa jipya la Daraja la 1. Beatrice anahisi ameshajifunza mengi kutokana na kusoma Kitabu cha 3. Na anajua kutoka kwa Alejandra, ambaye amemwambia hivyo mara chache kuwa umaizi alioupata kutoka kitabu utamwongezea uwezo wa kuhudumia kama mhuishaji.

Wao wanapokutana, Maribel anamwambia Beatrice kuwa wangemtembelea mama yake Emma. "Yeye ni mtoto mdogo mzuri sana anayependa kujifunza," Maribel anasema. "Mimi tayari nimeshawatembelea wazazi wake mara moja na nimewaeleza asili ya Darasa la Kibahá'í la watoto. Wao wamefurahi kumruhusu Emma ashiriki. Mama yake alieleza shauku ya kupata taarifa zaidi juu ya darasa, na mimi nilimwahidi kuwa ningerudi kumwambia zaidi juu ya mawazo ya kielimu kwenye msingi wa zana tunazofundisha. Mimi kwa kweli nimeandika vipengele vya kunikumbusha kwa ajili yangu mwenyewe. Kama unapenda tunaweza kuvipitia pamoja na kuviongelea." Beatrice anakubali. Haya ndiyo madokezo wanayo yajadili:

- Kwanza, nitamwambia Bi. Martinez jinsi nilivyofurahi kuwa Emma yumo katika darasa na nitamtajia baadhi ya sifa zake nzuri za ajabu.

- Kwa minajili ya kuanza majadiliano pengine ni bora kusoma pamoja naye teuzi hili kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh:

**"Mfikirie mtu kama chimbo la madini lililojaa vito vya thamani. Elimu, pekee, ndiyo inayoweza kufichua hazina zake, na kumwezesha binadamu kunufaika kutoka humo."**[37]

- Halafu ninaweza kushirikiana naye mawazo machache kuhusu namna ambavyo kauli hii imenihamasisha mimi kama mwalimu. Moyo wangu hujawa na furaha, nitasema, wakati wowote ninapowaangalia watoto darasani na kuwafikiria kama machimbo yaliyojaa vito vya thamani isiyo kadirika. Kila mmoja wao anao uwezo uliojificha wa kuonesha sifa za mbinguni. Kila mmoja ana vipaji ambavyo vinaweza kugundulika na kukuzwa. Kila mmoja wao anaweza kukua na kuwa mwanajamii bora na kuchangia katika uboreshaji wa ulimwengu.

- Halafu, pengine ningetoa mifano ya vito ambavyo elimu lazima ijitahidi kuonesha katika kila mtoto. Ninaweza kutaja baadhi ya uwezo wa kiakili, kwa mfano, kugundua sheria za kiasili, kutengeneza kazi nzuri sana za kisanii, na kueleza mawazo yao bora. Nitaeleza kuwa, watoto wanaweza kuanza kukuza uwezo wote huu, pale wanapopata elimu sahihi. Lakini, ili hili litokee, lazima wapate sifa fulani tangu wakiwa na umri mdogo. Kwa mfano, lazima wajifunze kuwa makini, kufanya kazi kwa juhudi pale inapohitajika na kutilia maanani kile wanacho kifanya. Wanapaswa kukua kama watu binafsi ambao wanajali maslahi na ustawi wa wengine na ambao wanapenda kuhudumia jumuiya. Ndiyo maana ni muhimu kufuatilia maendeleo ya tabia zao tangu umri mdogo.

- Hapa ni mahali pazuri pa kumwambia Bi. Martinez atuambie mawazo yake machache juu ya aina ya mtu ambaye angependa binti yake awe akiwa mkubwa. Ni zipi baadhi ya tabia ana fikiri ni muhimu Emma awe nazo?

- Miongoni mwa sifa anazozitaja, baadhi bila shaka, zitaangukia katika kundi la sifa za kiroho, ambayo ni mada ifuatayo nitakayoitambulisha. Zipo baadhi ya sifa ambazo lazima mtu awe nazo, nitasema, ambazo ni za msingi kwa maisha ya binadamu. Sifa hizo ni za roho ya binadamu. Tunazikuza kadri tunavyong'arisha kioo cha mioyo yetu ili kiweze kuakisi sifa za Mungu. Hizi ndizo tunaziita sifa za kiroho, na masomo tunayofundisha katika madarasa yetu katika Daraja la 1 yanalenga zaidi juu ya sifa hizi.

- Ninafikiri nitaendelea kuziorodhesha sifa za kiroho chache zilizoongelewa katika masomo ya Daraja la 1 katika Kitabu cha 3 na kushirikiana naye mateuzi yanayowiana nazo. Nitaeleza kuwa Emma atakariri mateuzi haya na kwamba anaweza kumuomba binti yake kughani mateuzi hayo kwake, hali kadhalika sala atakazojifunza:

  – Upendo:

    **"Ewe Rafiki! Katika bustani ya moyo wako usipande kingine ila waridi la upendo . . ."**[38]

– Haki:

**“Kanyageni njia ya haki, kwa kuwa hii, hakika, ndiyo njia iliyonyooka.”[39]**

– Ukweli:

**“Ukweli ndio msingi wa njema zote za binadamu.”[40]**

– Furaha:

**“Ewe Mwana wa mtu! Shangilia katika furaha ya moyo wako ili uweze kustahili kukutana Nami, na kama kioo kuonesha uzuri Wangu.”[41]**

Maribel na Beatrice wanaamua kwamba mawazo yaliyopo hapo juu yanatosha kwa ziara moja. Hivi punde ninyi wenyewe mtaingia kwenye usomaji wa Kitabu cha 3 na mtapata fursa ya kutafakari juu ya baadhi ya kanuni ambazo zinaunda programu ya miaka sita ya taasisi ya Ruhi kwa ajili ya elimu ya kiroho ya watoto. Ikiwa, kabla ya hapo, itajitokeza fursa ya kuwatembelea wazazi wachache pamoja na mwalimu wa darasa la watoto, mawazo yaliyoandikwa hapa yatathibitisha kuwa yenye msaada, na mnapaswa kuyajadili sasa hoja kwa hoja katika kikundi chenu cha mafunzo.

## SEHEMU YA 16

Hapo mapema tulisoma maneno yafuatayo ya ‘Abdu’l-Bahá: “Kadri yalivyo yenye nguvu zaidi mafundo ya udugu na mshikamano miongoni mwa watu, ndivyo utakavyo kuwa mkubwa zaidi uwezo wa kujenga na kukamilisha katika sura zote za shughuli zote za wanadamu.” Nyumba ya Haki ya Ulimwengu inatuambia kuwa, kwa kufanya ziara za nyumbani na kwa kualika wengine nyumbani kwetu, “tunaunda mafundo ya udugu wa kiroho ambao hulea hisia ya jumuiya.” Hatupaswi kudharau basi, athari ya desturi hii juu ya utamaduni wa jumuiya yetu inayoendelea kukua.

Katika sehemu zilizotangulia tumeangalia aina mbali mbali za mazungumzo ambayo yanaweza kufanyika wakati wa kutembeleana nyumbani kwa mmoja na mwingine. Sisi sote, kadiri tutembeavyo katika njia ya huduma, tutashiriki katika mazungmzo ya panukayo katika kijiji, mji au ujirani wetu juu ya utumiaji wa mafundisho ya Bahá’u’lláh katika maisha yetu binafsi na ya pamoja. Wakati mwingine hili litatokea katika mlolongo wa ziara rasmi zilizopangwa ili kuwawezesha idadi iongezekayo ya watu kuongeza kina cha ufahamivu wao wa mafundisho haya. Katika matukio mengine lukuki, programu za kielimu za taasisi, malengo yake na maudhui, vitakuwa mada za majadiliano. Mialiko ili kuwahusisha watu katika mchakato wa ujenzi wa jumuiya itatolewa kwa majirani na marafiki wengi zaidi na zaidi. Hivyo kadri muutazamavyo wakati ujao, na njia ya huduma ambayo inakunjuka mbele yenu, mtapaswa kufanya kila juhudi kujifunza vizuri maudhui yaliyowasilishwa katika kitengo hiki, mjipatie uzoefu wa kuzungumzia kila dhima, na, bila shaka, kuendelea kuongeza kina cha ufahamivu wenu wenyewe wa mafundisho ya Bahá’u’lláh. Ndivyo itakavyokuwa furaha yenu isiyo na kikomo ya kushirikiana Neno la Mungu na wengine.

# MAREJEO


1. Bahá’u’lláh, *Maneno Yaliyofichwa* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 2003, 2012 kuchapishwa), Kiarabu na. 4, uk. 4.

2. Bahá’u’lláh, katika *Sala za Kibahá’í: Chaguo la Sala Zilizofunuliwa na Bahá’u’lláh, Báb, na ‘Abdu’l-Bahá* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 2002, 2017 kuchapishwa), uk. 4.

3. *Makusanyo kutoka Maandiko ya Bahá’u’lláh* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 1983, 2017 kuchapishwa), IV, aya. 1, uk. 5.

4. Kama hapo juu., V, aya. 2, ku. 6–7.

5. ‘Abdu’l-Bahá, katika *Sala za Kibahá’í*, uk. 81.

6. Kama hapo juu., uk. 111.

7. Kama hapo juu.

8. Kutoka hotuba iliyotolewa mnamo 16 Agosti 1912, iliyochapishwa katika *Uenezaji wa Amani ya Ulimwengu: Mazungumzo Yaliyowasilishwa na ‘Abdu’l-Bahá wakati wa Safari Zake Amerika na Canada mwaka 1912* (Wilmette:Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 2012), aya. 23, uk. 364.

9. ‘Abdu’l-Bahá, katika *Sala za Kibahá’í*, uk. 130.

10. *Makusanyo kutoka Maandiko ya Bahá’u’lláh*, XLV, aya. 1, ku. 111–12.

11. ‘Abdu’l-Bahá, ilinukuliwa na Shoghi Effendi, *Utaratibu wa Ulimwengu wa Bahá’u’lláh: Barua Zilizochaguliwa* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 1991, 2012 kuchapisha), uk. 139.

12. *Makusanyo kutoka Maandiko ya Bahá’u’lláh*, V, aya. 5, uk. 8.

13. Kutoka hotuba iliyotolewa na ‘Abdu’l-Bahá mnamo 5 Mei 1912, iliyochapishwa katika *Uenezaji wa Amani ya Ulimwengu*, aya. 4, uk. 128.

14. Kutoka hotuba iliyotolewa mnamo tarehe 21 Oktoba 1911, iliyochapishwa katika *Mazungumzo ya Paris: Yaliyowasilishwa na ‘Abdu’l-Bahá 1911* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 2006, 2016 kuchapisha), na. 6.7–8, uk. 22.

15. *Makusanyo kutoka Maandiko ya Bahá’u’lláh*, CXLVI, aya. 1, uk. 357.

16. Kutoka hotuba iliyotolewa na ‘Abdu’l-Bahá mnamo 5 Mei 1912, iliyochapishwa katika *Uenezaji wa Amani ya Ulimwengu*, aya. 4, uk. 128.

17. *Maneno Yaliyofichwa*, Kiajemi na. 44, uk. 37.

18. Kama hapo juu., Kiajemi na. 66, uk. 45.

19. Kutoka Waraka wa ‘Abdu’l-Bahá. (tafsiri iliyoruhusiwa)

20. Kutoka hotuba iliyotolewa na ‘Abdu’l-Bahá mnamo 25 Septemba 1912, iliyochapishwa katika *Uenezaji wa Amani ya Ulimwengu*, aya. 2, ku. 478–79.

21. *Machaguo kutoka Maandiko ya ‘Abdu’l-Bahá* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 2010, 2015 kuchapisha), na. 43.1, uk. 125.

22. Kama hapo juu., na. 207.3, uk. 360.

23. Bahá’u’lláh, katika *Mikutano ya Kibahá’í: Dondoo kutoka Maandiko ya Bahá’u’lláh, ‘Abdu’lBahá, na Shoghi Effendi*, zilizotayarishwa na Idara ya Utafiti ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 1976, 1980 kuchapisha), uk. 3.

24. Kama hapo juu.

25. *Nyaraka za Abdul-Baha Abbas* (New York: Kamati ya Uchapishaji ya Kibahá’í, 1916, 1930 kuchapisha), juz. 3, uk. 631. (tafsiri iliyoidhinishwa)

26. Bahá’u’lláh, katika *Kitáb-i-Aqdas: Kitabu Kitakatifu Kabisa* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 1993, 2013 kuchapisha), aya. 57, uk. 41.

27. *Machaguo kutoka Maandiko ya ‘Abdu’l-Bahá*, na. 48.1, uk. 130.

28. Kutoka barua ya tarehe 27 Agosti 1989, iliyochapishwa katika *Jumbe kutoka Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, 1986–2001: Muhula wa Nne wa Zama za Utungo* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 2010), na. 69.2, ku. 132–33.

29. Kama hapo juu., na. 69.9–10, uk. 135.

30. *Maneno Yaliyofishwa*, Kiajemi na. 82, uk. 51.

31. Kama hapo juu., Kiajemi na. 80, uk. 51.

32. ‘Abdu’l-Bahá, *Siri za Ustaarabu Mtakatifu* (Wilmette: Uchapishaji wa Kibahá’í, 2007, 2016 kuchapisha), aya. 46, uk. 33.

33. *Maneno Yaliyofichwa*, Kiajemi na. 49, uk. 39.

34. Shoghi Effendi, ilivyonukuliwa katika *Habari za Kibahá’i*, na. 13 (Septemba 1926), uk. 1.

35. Kutoka hotuba iliyotolewa na ‘Abdu’l-Bahá mnamo 17 Novemba 1912, iliyochapishwa katika *Uenezaji wa Amani ya Ulimwengu*, aya. 3, uk. 617.

36. Kutoka ujumbe wa tarehe 21 Aprili 2010, uliyochapishwa katika *Muundo kwa ajili ya Utendaji: Jumbe Zilizochaguliwa za Nyumba ya Haki ya Ulimwengu na Zana za Ziada, 2006–2016* (West Palm Beach: Palabra Publications, 2017), na. 14.16, uk. 82.

37. *Makusanyo kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh*, CXXII, aya. 1, uk. 294.

38. *Maneno Yaliyofichwa*, Kiajemi na. 3, uk. 23.

39. *Makusanyo kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh*, CXVIII, aya. 1, uk. 283.

40. 'Abdu'l-Bahá, yalinukuliwa na Shoghi Effendi, *Majilio ya Haki Takatifu* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2006, 2018 kuchapisha), aya. 40, uk. 39.

41. *Maneno Yaliyofichwa*, Kiarabu na. 36, uk. 12.